Kikao cha Ishirini na Sita - Tarehe 19 Julai, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2013/2014 - Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, nomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili liweze kupokea, kujadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Spika, Kwanza kabisa nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutujaalia kwa mara nyengine kukutana hapa katika Baraza hili Tukufu tukiwa na afya njema.

Mhe. Spika, kupitia Baraza lako Tukufu napenda kuchukua nafasi hii adhimu kumshukuru na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa uongozi wake wenye busara, hekima na uadilifu, ambao umekuwa dira katika harakati za kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi wa Zanzibar. Hapana shaka wananchi wa Zanzibar wanaendelea kuwa na imani na uongozi wake, ambao kwa kweli umetoa matumaini katika kipindi chote tangu ameanza kushika dhamana hiyo. Jitihada zake zinaonekana wazi na zimeleta maendeleo makubwa ya kisiasa, kiuchumi na kijamii, pamoja na kuendeleza amani na utulivu nchini.

Mhe. Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharif Hamad na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi kwa mashirikiano wanayotupa katika utekelezaji wa majukumu yetu, chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Aidha, miongozo yao imesaidia kufanikisha shughuli za Wizara yangu. Pia napenda kuchukua nafasi hii adhimu kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika kwa kuendelea kuliongoza Baraza hili Tukufu kwa hekima, busara na uadilifu. Uongozi wako makini katika kuliendesha Baraza hili, umeisaidia Serikali kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, naishukuru sana Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza lako Tukufu iliyokuwa ikiongozwa na Mhe. Asha Bakari Makame kwa ushirikiano, ushauri, miongozo na maelekezo yake ambayo yamesaidia sana katika kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu.

Aidha, nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Mlinde Mabrouk Juma kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari, pamoja na Wajumbe wote wapya waliochaguliwa kwenye Kamati hiyo. Ni matumaini yangu kwamba tutaendelea kushirikiana katika kufanikisha majukumu yetu. Pia nachukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu, kwa miongozo na michango yao wanayoitoa, ambayo nayo imesaidia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu .

MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika, bajeti na mpango kazi wa Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2013/2014 imelenga kuchangia katika ufikiaji wa malengo ya Dira ya Maendeleo ya 2020; Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar kwa mwaka 2010 - 2015 (MKUZA II); Malengo ya Milenia 2015; Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2010 - 2015, Sera husika za kisekta na Mpango Mkakati wa Wizara. Aidha, mpango kazi na bajeti, imelenga katika kutanua fursa za wananchi kujiajiri na kuajiriwa, (mkazo zaidi ukielekezwa kwa vijana) pamoja na kuimarisha utekelezaji wa sheria za kazi.

Mhe. Spika, wizara kwa kipindi cha mwaka 2013/2014 imepanga kuendelea kutekeleza malengo makuu yafuatayo:

1. Kuongeza upatikanaji wa fursa za ajira za heshima kwa wananchi wanaume na wanawake, hususan vijana;
2. Kuongeza na kutanua programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi;
3. Kuimarisha utekelezaji wa sheria za kazi;
4. Kuimarisha uhusiano kazini na utekelezaji wa viwango vya kazi;

5. Kuimarisha utekelezaji wa Sheria Nambari 8 ya mwaka 2005 juu ya Usalama na Afya Kazini ili kuhakikisha hali bora ya usalama na afya katika sehemu za kazi;
6. Kusimamia na kuratibu uandaaji pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa sera, mipango na programu za Wizara;
7. Kuimarisha uwezo wa watendaji na mazingira ya kazi ili kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa nichukue fursa hii nitoe maelezo juu ya mapato na matumizi na utekelezaji wa malengo kwa mwaka wa fedha uliopita wa 2012/2013, pamoja na kuwasilisha malengo na makadirio ya bajeti kwa mwaka 2013/2014.

MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2012/2013

Mhe. Spika, Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2012/2013, ilipangiwa kukusanya jumla ya Shilingi Milioni Tisini na Tatu (T. Shs. 93,000,000/=) kutokana na vyanzo vya mapato vifuatavyo:

(i) Vibali vya kazi kwa wafanyakazi wa kigeni;
(ii) Ukaguzi wa mikataba ya kazi;
iii) Usajili wa vyama vya ushirika; na Huduma za ukaguzi wa vyama vya ushirika.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2013, jumla ya Shilingi Milioni Mia Moja Thelathini na Saba, Laki Saba Elfu Themanini na Sita, Mia Saba Themanini na Saba **(**T.Shs.137,786,787/=) zimekusanywa, sawa na asilimia 148 ya makadirio (Angalia Kiambatanisho Nam. 1).

Mhe. Spika, katika mwaka huo wa fedha wa 2012/2013, Wizara yangu ilitengewa jumla ya Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Tatu Kumi na Nne, Laki Tano Elfu Sitini na Tano na Mia Saba (T.Shs. 2,314,565,700/=) kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo, Shilingi Bilioni Moja na Milioni Themanini (T.Shs. 1,080,000,000/=) zilitengwa kwa ajili ya mishahara, mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na posho za wafanyakazi; Shilingi Milioni Mia Mbili na Arobaini na Nane (T.Shs. 248,000,000/=) ni ruzuku kwa ajili ya Idara ya Mikopo; na Shilingi Milioni Mia Tisa Themanini na Sita, Laki Tano Elfu Sitini na Tano na Mia Saba (T.Shs. 986,565,700/=) zilitengwa kwa matumizi mengineyo. Bajeti hii ni baada ya mkato uliofanywa kwa Wizara zote kwa kugharamia ununuzi wa meli.

Mhe. Spika, jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Nne na Hamsini na Tano, Laki Nane na Elfu Sitini na Moja (T.Shs. 1,455,861,000/=) zilitengwa kwa kazi za maendeleo. Kati ya hizo, Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia

Moja na Arobaini (T.Shs. 1,140,000,000/=) ni fedha za Serikali kwa kugharamia utekelezaji wa Programu ya Ajira kwa Vijana, Mradi wa Kupambana na Ajira Mbaya za Watoto na Mradi wa Kuimarisha Sekta ya Ushirika; na Shilingi Milioni Mia Tatu Kumi na Tano, Laki Nane na Elfu Sitini na Moja (T.Shs. 315,861,000/=) ni fedha kutoka kwa wahisani (*IFAD* na *AfDB*) kwa kugharamia shughuli za uimarishaji wa huduma za kifedha vijijini, kupitia Programu ya Miundo Mbinu ya Soko, Uongezaji Thamani ya Mazao ya Kilimo na Huduma za Fedha Vijijini. Aidha, Wizara ilitegemea kupata Shilingi Milioni Mia Sita na Moja, Laki Saba Elfu Arobaini na Moja, Mia Nane Tisini na Sita (T.Shs. 601,741,896/=) kutoka Shirika la Kazi Duniani (*ILO*), kupitia Programu ya Msaada wa Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (*UNDAP*).

Mhe. Spika, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2013, Wizara imeingiziwa jumla ya Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Moja Ishirini na Nane, Laki Tatu Elfu Ishirini na Tano, Mia Nne Themanini na Mbili. (T. Shs. 2,128,325,482/=) kwa matumizi ya kawaida.

Kati ya hizo, Shilingi Bilioni Moja, Milioni Arobaini na Nane, Laki Sita Elfu Saba na Mia Nne (T. Shs. 1,048,607,400/=) ni kwa ajili ya mishahara, mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na posho za wafanyakazi; Shilingi Milioni Mia Nane na Arobaini, Laki Nane Elfu Arobaini na Tatu, Mia Mbili Arobaini na Mbili (T.Shs. 840,843,242/=) kwa matumizi mengineyo yasiyokuwa mishahara ambayo ni sawa na asilimia 85 ya fedha zilizotengwa kwa ajili hiyo; na Shilingi Milioni Mia Mbili Thelathini na Nane, Laki Nane Elfu Sabini na Nne, Mia Nane na Arobaini (T.Shs.238,874,840/=) ni kwa ajili ya ruzuku kwa Idara ya Mikopo. Kiambatanisho Nam.2 kinatoa ufafanuzi kuhusu fedha zilizotengwa na kutolewa kwa matumizi ya kawaida ya Wizara hadi kufikia mwishoni mwa mwezi wa Juni 2013.

Mhe. Spika, fedha zilizopatikana kutoka mfuko wa Serikali kwa kazi za maendeleo hadi kufikia kipindi hicho ni Shilingi Milioni Mia Tatu Hamsini na Nne, Sitini na Mbili Elfu, Mia Tatu Sitini na Tisa (T. Shs. 354,062,369/=), sawa na asilimia 31 ya fedha zilizotengwa kwa mwaka 2012/2013. Kwa upande wa mchango wa wahisani, fedha zilizopatikana ni Shilingi Milioni Mia Moja Hamsini na Nane, Laki Tisa Elfu Tisini na Moja, Mia Tatu Sabini na Tano (T. Shs. 158,991,375/=), sawa na asilimia 17 ya makisio ya mwaka. Kati ya fedha hizo zilizotolewa na wahisani, Shilingi Milioni Hamsini na Moja, Laki Sita Elfu Sabini na Tisa (T. Shs. 51,679,000/=) ni kwa uimarishaji wa huduma za fedha vijijini kupitia Programu ya Miundombinu ya Soko, Uongezaji Thamani ya Mazao ya Kilimo na Huduma za Fedha Vijijini na Shilingi Milioni Mia Moja na Saba, Laki Tatu Elfu Kumi na Mbili, Mia Tatu Sabini na Tano (T.Shs. 107,312,375/=) zilitolewa na *ILO* kwa utekelezaji wa

shughuli zinazohusiana na ukuzaji wa kazi za staha kupitia Programu ya Msaada wa Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (*UNDAP*).

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA 2012/2013 NA MALENGO KWA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika inatekeleza majukumu yake kupitia Kamisheni moja na Idara saba zifuatazo:

1. Kamisheni ya Kazi;
2. Idara ya Ajira;
3. Idara ya Usalama na Afya Kazini;
4. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
5. Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
6. Idara ya Uendelezaji na Uratibu wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
7. Idara ya Ushirika; na
8. Idara ya Mikopo

Ofisi Kuu Pemba inasimamia shughuli zote za Wizara, ikiwa pamoja na majukumu ya Kamisheni na Idara hizo, kwa upande wa Pemba. Utekelezaji wa malengo kwa mwaka 2012/2013 na malengo kwa mwaka 2013/2014 kwa kila Idara ni kama ifuatavyo:

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika, Katika mwaka 2012/2013, Idara hii ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa Wizara;
2. Kuimarisha uratibu na upangaji wa programu za Wizara;
3. Kuimarisha uwezo wa Wizara katika kufanya tafiti;
4. Kuimarisha mazingira ya kisera na kisheria kwa utekelezaji wa masuala ya usalama na afya kazini na uwezeshaji wananchi kiuchumi;
5. Kuimarisha mashirikiano baina ya Wizara na wahusika wengine; na
6. Kuingiza masuala mtambuka katika sera, programu na mipango ya Wizara.

Utekelezaji wa Malengo ya Idara ya Mipango, Sera na Utafiti

Mhe. Spika, katika taasisi yoyote, suala la ufuatiliaji na tathmini lina nafasi muhimu katika kuhakikisha mipango inayotekelezwa inaleta matokeo

yanayotarajiwa. Hii inahitaji kuweko kwa mfumo makini wa ufuatiliaji na tathmini ya shughuli zinazotekelezwa. Kwa kutambua hilo, Wizara yangu kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imetayarisha Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa shughuli inazozisimamia. Mfumo huu utaiwezesha Wizara kukusanya taarifa mbali mbali kuhusiana na shughuli zinazotekelezwa na hatimae kupima mafanikio yanayopatikana kutokana na shughuli hizo.

Ili mfumo huo uweze kutumika ipasavyo, jumla ya watendaji thelathini (30) wamepatiwa mafunzo ya awali juu ya ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa na namna ya kuzitumia katika kupanga na kufanya maamuzi yanayohusu sera, mikakati na programu. Aidha, Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini kimeimarishwa kwa kupatiwa vitendea.
Mhe. Spika, Katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Wizara imekuwa ikiratibu na kutekeleza miradi na programu zifuatazo:

Programu ya Ajira kwa Vijana
Mhe. Spika, programu hii ilianza kutekelezwa rasmi mwezi wa Oktoba 2012. Kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013, programu hii ililenga kuzalisha nafasi za ajira kwa vijana 950 wanawake na wanaume, Unguja na Pemba, kupitia miradi mbali mbali iliyo chini yake. Utekelezaji wa programu hii inayoratibiwa na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, unahusisha pia Wizara zinazoshughulikia masuala ya Vijana, Utalii, Mifugo na Uvuvi, na Ofisi ya Rais inayoshughulikia masuala ya Tawala za Mikoa kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi.

Mhe. Spika, katika kipindi cha 2012/2013, programu hii imetekeleza yafuatayo:

- Kupitia Wizara inayoshughulikia masuala ya Vijana, programu imesaidia uanzishwaji wa mashamba ya kilimo cha maua ya “rosella” katika maeneo ya Tunguu, Unguja na Mbuzini, Pemba. Jumla ya vijana 50 (25 Unguja na 25 Pemba) kwa kuanzia, wamelengwa kupatiwa ajira kupitia mashamba haya. Lengo ni kuyafanya mashamba haya kuwa ni mashamba darasa kwa ajili ya kuvipatia vikundi vya vijana mafunzo ya vitendo juu ya kilimo bora na cha kisasa, pamoja na ujasiriamali, ili hatimaye waweze kujiajiri. Hatua iliyofikiwa kwa sasa ni uandaaji wa mashamba hayo, ikiwemo kusafishwa, kuwekewa uzio na miundombinu ya maji.

- Jumla ya vijana 152 (Unguja 76 na Pemba 76) wanaojishughulisha na shughuli za utembezaji watalii, wamepatiwa mafunzo juu ya historia ya Zanzibar na utaratibu wa uendeshaji wa shughuli hiyo, ili waweze kuifanya kwa umahiri zaidi. Kati ya vijana hao, vijana 128 (64 Unguja na 64 Pemba) wameweza kupatiwa usajili katika Jumuia ya Watembezaji Watalii Zanzibar

na hivyo kutambuliwa rasmi. Utekelezaji wa shughuli hii umesimamiwa na Wizara inayoshughulikia masuala ya Utalii.

- Kupitia Wizara inayoshughulikia masuala ya Mifugo na Uvuvi, jumla ya vijana 80 (40 Unguja na 40 Pemba) wamepatiwa mafunzo ya ufugaji wa kuku kupitia mashamba darasa manne yaliyoanzishwa katika Shehia za Kibeni na Kikobweni katika Wilaya ya Kaskazini A Unguja na Shehia za Ukutini na Mjimbini katika Wilaya ya Mkoani Pemba. Jumla ya kuku 800 walitolewa kwa vijana hao 80 (Unguja wanawake 20 na wanaume 20; na Pemba wanawake 19 na wanaume 21) ili wajiendeleze kiuchumi. Kila kijana mmoja amepatiwa kuku 10 (jogoo mmoja na majike 9).

- Kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi, programu imegharamia ujenzi wa masilabi mawili (2) ya kuhifadhi taka ngumu katika Shehia za Tomondo na Mbweni. Kila silabi moja linatarajiwa kutoa ajira kwa vijana 25 katika shughuli za kukusanya na kuhifadhi taka. Lengo kwa mwaka 2012/2013 lilikuwa ni kujenga masilabi kumi (10) ambayo yangetoa ajira kwa vijana 250. Hata hivyo, lengo hilo halikuweza kufikiwa kutokana na wananchi, katika baadhi ya maeneo yaliyokuwa yameainishwa, kuzuia ujenzi wa masilabi hayo. Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi inaendelea kutoa taaluma kwa wananchi wa maeneo hayo, ili ujenzi wa masilabi yaliyobaki.

- Kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, jumla ya vijana 60 (30 Unguja na 30 Pemba) wamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali, ikiwemo mbinu za ushindani wa biashara. Lengo ni kuwafanya wachangamkie njia mbadala za ajira kwa kuwawezesha kutumia fursa zilizopo kujiajiri, badala ya kusubiri kazi za kuajiriwa. Pia vijana 43 waliomaliza mafunzo ya ufundi wamepatiwa mafunzo maalum ya kuwashajiisha kubadili mitazamo yao kuhusu ajira. Mafunzo hayo yalihusisha,pamoja na mambo mengine, masuala yanayohusu huduma kwa wateja na ujasiriamali. Utaratibu unafanywa kuwapatia vijana hao elimu ya vitendo. Wizara tayari imewasiliana na taasisi mbali mbali za sekta ya umma na binafsi na baadhi yao, ikiwemo Kiwanda cha Sukari Mahonda, Mamlaka ya Maji, Shirika la Umeme, Shirika la Bandari na Melia Hotel zimekubali kuwapatia mafunzo ya vitendo kupitia utaratibu wa elimu kazi.

Matarajio ni kwamba, kupitia utaratibu huu wa elimu kazi, baadhi yao wataweza kushawishi waajiri kuwaajiri na wengine wataweza kujiajiri katika kazi za utoaji wa huduma za kiufundi, kupitia vyama vya ushirika.

Programu ya Kazi Nje Nje

Mhe. Spika, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) inaendelea kutekeleza Programu ya Kazi Nje Nje. Programu hiyo iliyoanza

kutekelezwa rasmi mwezi Machi 2011 inalenga kuwawezesha vijana kuwa na muamko wa kujiajiri wenyewe badala ya kutegemea ajira za kuajiriwa. Katika kipindi cha mwaka 2012/2013, vijana wa Kazi Nje Nje wameweza kuhamasisha na kutoa elimu ya ujasiriamali kwa vijana 901 (wanawake 549 na wanaume 352) Unguja na Pemba. Vijana hao wamepatiwa mafunzo juu ya ujasiriamali, ikiwemo namna ya kubuni wazo la biashara. Wengi wa vijana waliopatiwa mafunzo walikuwa tayari wana biashara zao, hivyo mafunzo hayo yamewasaidia katika kuimarisha biashara hizo.

Mhe. Spika, katika kuimarisha utekelezaji wa programu hii, *ILO* imetoa vitendea kazi ikiwemo kompyuta 3, 'scanner' na printa ambazo vijana wa Kazi Nje Nje wanatumia katika kufanikisha shughuli zao. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na *ILO* imekusudia kuongeza idadi ya wakufunzi wa Kazi Nje Nje kwa kuwapatia mafunzo vijana walioko Pemba, ili waweze kushajiisha na kutoa elimu ya ujasiriamali kwa vijana wenzao walioko huko.

Programu ya *UNDAP*

Mhe. Spika, kupitia programu hii, Shirika la Kazi Duniani limekuwa likiisaidia Wizara kutekeleza shughuli mbalimbali ili kufikia malengo iliyojiwekea katika kukuza ajira na kuendeleza kazi za staha. Katika kipindi cha mwaka 2012/2013, programu hii imetekeleza shughuli zifuatazo:

- Imefanya tathmini ya kuangalia hali halisi ya usalama na afya katika sehemu za kazi, pamoja na kutayarisha Sera ya Usalama na Afya Kazini.
- Imefanya tathmini juu ya programu zilizopo za uwezeshaji wananchi kiuchumi ili kubaini mafanikio, mapungufu na changamoto zake. Ripoti ya matokeo ya tathmini hiyo inatumika katika kutayarisha Sera ya Zanzibar ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

- Imekamilisha Sera ya Elimu Kazi na kuanza mchakato wa kutayarisha Mpango Mkakati wa utekelezaji wa sera hiyo. Kukamilika kwa Mpango huo kutaweka misingi imara ya utekelezaji wa sera hiyo.

- Imegharamia watendaji wawili wa sekta ya ushirika kushiriki katika ziara ya mafunzo nchini Japan ili kujifunza masuala ya ushirika. Mafunzo yaliyopatikana yamesaidia katika kuimarisha mikakati ya kuendeleza Sekta ya Ushirika.

- Imetoa mafunzo kwa wajumbe 150 (38 wanawake, 112 wanaume) wa Kamati za Wilaya za Ajira, Unguja na Pemba, juu ya utayarishaji wa Mipango Kazi inayohusisha uzalishaji wa ajira. Kupitia mafunzo hayo,

Kamati hizo zimeweza kuandaa mipango kazi ya kuzalisha ajira kwa kuzingatia fursa zilizomo katika maeneo yao.

- Imetoa mafunzo kwa Maafisa 32 wanaohusika na mipango na bajeti kutoka Wizara 16 za Serikali, juu ya uingizaji wa masuala ya ajira na kazi za staha katika mipango yao ya kazi na matumizi. Mafunzo hayo yamelenga kuzisaidia taasisi hizo kuweza kuibua na kuyafanyia kazi maeneo ya kuzalisha ajira katika shughuli za taasisi zao.

- Imefanya mapitio ya Mpango wa Ajira kwa Vijana, shughuli ambayo ilihusisha mashauriano na washirika mbalimbali kwa lengo la kubainisha mapungufu na changamoto kuhusiana na suala la ajira kwa vijana. Taarifa zinazotokana na zoezi hili zitatumika katika kuandaa Mpango mpya wa ajira kwa vijana, utaozingatia mapungufu na changamoto zilizojitokeza.

- Imesaidia kukiimarisha Kitengo cha Taarifa za Ajira kwa kuandaa mfumo wa kukusanya na kuhifadhi taarifa za ajira. Pia watendaji wa kitengo hicho, pamoja na maofisa kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali wamepatiwa mafunzo juu ya utumiaji wa mfumo huo pamoja na uchambuzi wa taarifa za ajira. Vile vile kupitia programu hii, Kitengo cha Taarifa za Ajira kimepatiwa vitendea kazi zikiwemo kompyuta tano na printa moja.

- Imewapatia mafunzo watendaji sita (6) wa Kitengo cha Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro ya Kazi. Mafunzo hayo yameongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao. Aidha, watendaji 15 wakiwemo wajumbe wa Kamati ya Utatu wamepatiwa mafunzo juu ya usuluhishi wa migogoro ya kazi.

- Imetoa mafunzo kwa viongozi wa ngazi ya juu katika Sekta ya Kazi, juu ya majadiliano ya pamoja katika masuala ya kazi. Mafunzo hayo yaliwahusisha viongozi 16 kutoka Wizara zinazoshughulikia masuala ya Kazi na Utumishi wa Umma pamoja na Jumuia ya Waajiri na Shirikisho laVyama Huru vya Wafanyakazi.

- Imefanya tathmini ya hali ya UKIMWI na Kifua Kikuu katika sehemu za kazi. Tathmini hiyo ilihusisha sekta za umma na sekta binafsi, ikiwemo sekta ya uvuvi, kilimo cha karafuu, ujenzi, usafiri, hoteli na biashara ndogo ndogo. Matokeo ya tathmini hiyo yatasaidia kuweka mikakati ya kupambana na tatizo la UKIMWI na kifua kikuu katika sehemu za kazi.

Mradi wa Uimarishaji wa Huduma za Fedha Vijijini.
Mhe. Spika, mradi huu ni sehemu ya Programu ya Miundombinu ya Soko, Uongezaji Thamani ya Mazao ya Kilimo na Huduma za Fedha Vijijini, unaosimamiwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili na kugharamiwa na Shirika la Maendeleo ya Kilimo (*IFAD*) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AFDB*). Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika ni miongoni mwa watekelezaji wa programu hii, ikiwa na jukumu la kusimamia shughuli za uimarishaji wa huduma za fedha vijijini, kupitia Idara yake inayoshughulikia masuala ya ushirika.

Mhe. Spika, lengo la programu katika eneo hili ni kuimarisha upatikanaji wa huduma za fedha kwa wajasiriamali wadogo na wa kati vijijini. Katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Mradi wa Uimarishaji wa Huduma za Fedha Vijijini kupitia Programu hii, umetekeleza yafuatayo:

- Umesaidia kufanya mapitio ya rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Ushirika ili kuingiza masuala yanayohusu huduma za fedha vijijini.

- Imetoa mafunzo ya utambulisho kuhusu huduma za fedha vijijini kwa jumuiya za *JOCDO* (*Jozani Credit and Development Organisation*) na *PESACA* (*Pemba Saving and Credit Association*). Jumla ya washiriki 60 (wanawake 26 na wanaume 34) Unguja na Pemba wamepatiwa mafunzo hayo.

- Imesaidia kuandaa miongozo ya upekuzi na ukaguzi wa vyama vya ushirika.

- Imegharamia mafunzo ya muda mrefu kwa watendaji watano (watatu Unguja na wawili Pemba) wa Idara ya Ushirika. Watendaji watatu kati ya hao, wanachukua mafunzo ya ngazi ya Diploma katika fani ya huduma za mikopo midogo midogo kwenye Chuo Kikuu cha Ushirika na Stadi za Biashara, Tawi la Kizumbi – Shinyanga na wawili wanachukua mafunzo ya ngazi ya cheti katika fani ya "*Computerized Accounting*" kwenye Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar.

- Ziara ya kufuatilia utekelezaji wa shughuli za mradi Unguja na Pemba imefanyika. Matokeo ya ufuatiliaji yameonesha kuwa baada ya mafunzo, jumuiya za *PESACA* na *JOSACA* zimeendeleza uhamasishaji wa asasi ndogo ndogo za fedha ili kuanzisha *SACCOS* kwenye maeneo ya Chake Chake na Chokocho kwa Pemba na Kitogani kwa Unguja. Jumla ya Shehia 27 (Unguja 16 na Pemba 11) zimefikiwa katika uhamasishaji huu. Aidha, jumla ya viongozi 770 (550 Unguja na 220 Pemba) kutoka asasi ndogo ndogo za fedha wamehamasishwa na wameonesha ridhaa ya kuunda *SACCOS*.

Mradi wa Kupambana na Ajira za Watoto
Mhe. Spika, mradi huu unagharamiwa na Jumuiya ya Ulaya kupitia Save the Children. Utekelezaji wake unahusisha Wizara zinazoshughulikia masuala ya Kazi, Elimu na Ustawi wa Jamii pamoja na taasisi za kiraia (*TAMWA, COWPZ, PIRO* na *KUHAWA*). Lengo la mradi ni kuwanusuru watoto 5,000 katika Wilaya zote za Unguja na Pemba dhidi ya ajira za watoto.

Mradi huu ambao utekelezaji wake umeanza mwaka 2012, unatekelezwa katika Shehia 50 za Zanzibar (Shehia 25 Unguja na 25 Pemba). Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2012/2013, mradi huu umefikia jumla ya Shehia 16 zikiwemo Shehia za Micheweni, Mjini Kiuyu, Majenzi, Kangagani, Ndagoni, Wesha, Vitongoji na Uwandani kwa upande wa Pemba na Kijini, Nungwi, Pwani Mchangani, Mkokotoni, Marumbi, Uzini, Charawe na Chwaka kwa upande wa Unguja.

Mhe. Spika**,** katika awamu ya mwanzo, mradi ulilenga kuwatoa watoto 1,200 katika ajira za watoto. Mradi umeweza kuwabaini watoto 1,553 (wanaume 1,014 na wanawake 539) walio katika mazingira magumu. Kati ya hao, watoto 398 waliokuwa tayari wamo katika ajira za watoto walitolewa katika ajira hizo na kurejeshwa skuli, pamoja na kupatiwa vifaa mbalimbali ikiwemo mabuku, sare za skuli na viatu. Jumla ya familia 381 za watoto waliorejeshwa skuli na za watoto walio katika mazingira hatari ya kujiingiza katika ajira za watoto ziliwezeshwa kwa kusaidiwa kuanzisha shughuli za kiuchumi, zikiwemo biashara na ufugaji.

Katika awamu ya pili, mradi umelenga kushughulikia tatizo la ajira za watoto katika Shehia za Chumbuni, Shaurimoyo, Mwembe Makumbi, Mwanakwerekwe, Kizimkazi na Jambiani kwa upande wa Unguja na Shehia za Wambaa, Muwambe, Mtangani, Mbuyuni, Selemu, Shumba mjini, Mitiulaya na Msuka kwa Pemba.

Napenda kutoa wito kwa wazazi kushirikiana na Serikali katika kupambana na ajira hizi mbaya za watoto ili tuweze kujenga jamii bora ya baadae.

Mhe. Spika, ili kuongeza ufanisi katika uratibu na upangaji wa programu za Wizara, mafunzo juu ya uandishi wa miradi, mbinu za kutafuta rasilimali fedha na mbinu za kujadiliana na wahisani yamefanyika. Jumla ya watendaji 30 wa idara zilizo chini ya Wizara hii wamepatiwa mafunzo hayo, ambayo yamelenga katika kujenga uwezo wa kuandaa miradi yenye viwango bora na kushajihisha upatikanaji wa fedha za kusaidia utekelezaji wake.

Pia watendaji hao wamepatiwa mafunzo juu ya utayarishaji wa bajeti katika mfumo wa programu. Mafunzo hayo yamesaidia katika kuandaa bajeti na mpango kazi wa Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, ambapo jumla ya programu nne zinazohusu shughuli kuu za Wizara ziliandaliwa. Pogramu hizo ni (i) Utengenezaji na Uendelezaji wa Ajira; (ii) Usimamizi wa Utekelezaji wa Sheria za Kazi; (iii) Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; na (iv) Sera, Mikakati na Uendeshaji wa Masuala ya Kazi na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Mhe. Spika, Wizara yangu pia imeendelea kuzingatia uhusishaji wa masuala mtambuka katika shughuli zake za kila siku. Masuala mtambuka yanayozingatiwa katika shughuli za Wizara ni pamoja na utawala bora; mapambano dhidi ya UKIMWI na dawa za kulevya; uwiano wa jinsia; uhifadhi wa mazingira; na uzingatiaji wa makundi ya watu wenye mahitaji maalum, wakiwemo watu wenye ulemavu. Katika kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI katika sehemu za kazi, Wizara imetayarisha Mpango Mkakati wa UKIMWI kwa lengo la kuzuia maambukizi mapya, kuondosha unyanyapaa na kuzuia vifo vinavyotokana na UKIMWI katika sehemu za kazi.

Pia Wizara imeingiza masuala yanayohusu UKIMWI katika miongozo ya ukaguzi wa masuala ya usalama na afya katika sehemu za kazi. Aidha, wanawake, vijana, watu wenye ulemavu na wanaoishi na virusi vya UKIMWI wamekuwa miongoni mwa makundi yanayofaidika na programu za uwezeshaji, ambazo Wizara imekuwa ikizitekeleza.

Malengo ya Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa mwaka 2013/2014
Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014, Idara hii imekusudia kuendeleza utekelezaji wa malengo yafuatayo:

1. Kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za Wizara;
2. Kuimarisha uratibu na upangaji wa programu za Wizara;
3. Kuimarisha ufanyaji wa tafiti zinazohusu maeneo ambayo Wizara inayafanyia kazi;
4. Kuimarisha mazingira ya kisera na kisheria kwa utekelezaji wa masuala ya usalama na afya kazini na uwezeshaji wananchi kiuchumi;
5. Kuimarisha mashirikiano baina ya Wizara na wahusika wengine wa masuala ya kazi, uwezeshaji wananchi kiuchumi na ushirika; na
6. Kusimamia na kuimarisha uingizwaji wa masuala mtambuka katika sera, programu na mipango ya Wizara.

Mhe. Spika, ili Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2013/2014, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Mia Moja Kumi na Nane na Elfu Themanini na Tatu (T.Shs.118,083,000/=) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi Bilioni Moja na Milioni Mia Moja (T.Shs 1,100,000,000/=) kwa kazi za maendeleo.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ya Uendeshaji na Utumishi ilipangiwa kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kuwapatia mafunzo wafanyakazi 18 ili waweze kutekeleza vyema majukumu yao;
2. Kuimarisha mazingira ya kazi;
3. Kuimarisha usalama wa majengo na mazingira yanayozunguka Wizara;
4. Kuimarisha kitengo cha Habari na Mawasiliano (ICT Unit) cha Wizara;
5. Kuimarisha mfumo wa usimamizi wa fedha na manunuzi;
6. Kutoa taarifa juu ya utekelezaji wa shughuli za Wizara ili kuelimisha na kujenga taswira nzuri kwa umma; na
7. Kusimamia upatikanaji wa haki na maslahi ya wafanyakazi.

Utekelezaji wa Malengo ya Idara ya Uendeshaji na Utumishi

Mhe. Spika, katika kufanikisha malengo iliyojiwekea, Idara imetekeleza yafuatayo:

1) Imelipia gharama ya masomo ya muda mrefu kwa wafanyakazi 22 (wanawake 8 na wanaume 14) Unguja na Pemba. Kati ya hao, wafanyakazi tisa (9) ni wale ambao walikuwa wanaendelea na masomo yao kutoka mwaka uliopita na kumi na tatu (13) ni wafanyakazi walioanza masomo yao katika mwaka wa fedha wa 2012/2013. Miongoni mwa wafanyakazi 22 waliogharamiwa, wafanyakazi 12 wamemaliza masomo yao katika fani za Mipango na Sera; Sheria; Uhasibu; Usimamizi wa Manunuzi; Ushirika; Usimamizi wa Rasilimali Watu, Uandishi wa Habari; na Ukatibu Muhtasi. Wafanyakazi kumi (10) waliobaki wanaendelea na masomo katika fani za Mipango, Sheria, Masoko, Maendeleo ya Jamii, Uchumi,

Usimamizi wa Manunuzi na Ukatibu Muhtasi (Angalia Kiambatanisho Nam. 3a na 3b).

2) Imewapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi 21 (wanawake 7 na wanaume 14) Unguja na Pemba katika fani ya Udereva, Ukaguzi wa Hesabu, Uandishi wa Sheria, Ukatibu Muhtasi, Kompyuta, Usalama na Afya Viwandani, Uwezeshaji na Maendeleo ya Ujasiriamali, Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii, Teknolojia ya Habari (*IT*) na masuala ya kupambana na ajira mbaya za watoto. Kati ya hao, wafanyakazi wanane (wanawake watatu na wanaume watano) wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi nchini China, India na Korea, kupitia Ofisi ya Rais (Utumishi wa Umma na Utawala Bora); mfanyakazi mmoja mwanamke amepata mafunzo nchini Italy, kupitia Shirika la Kazi Duniani na mwengine mwanamke amehudhuria mafunzo nchini Marekani, kupitia msaada wa *USAID*.

3) Imetoa mafunzo ya ndani ya utunzaji kumbukumbu kwa wafanyakazi 24 (wanawake 16 na wanaume 8). Mafunzo hayo yaliwahusisha wafanyakazi wa sehemu ya Masjala, Makatibu Muhtasi na Kalamazoo. Lengo la mafunzo hayo ni kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu za Wizara. Aidha, mafunzo ya kompyuta yametolewa kwa wafanyakazi 20 (wanawake 13 na wanaume 7) kutoka Idara zinazoshughulikia masuala ya Mikopo, Ushirika na Utumishi/Uendeshaji ili waweze kutekeleza kazi zao kwa ufanisi.

4) Imetoa elimu ya usalama na afya kwa wafanyakazi wote wa Wizara na kutoa fursa kwa wafanyakazi wanane (wanawake watatu na wanaume watano) wanaotarajiwa kustaafu, kupima afya zao kikamilifu. Lengo hasa ni kujua afya zao, ikiwemo kuweza kugundua kama kuna matatizo ya kiafya yaliyosababishwa na kazi au mazingira yao ya kazi, ili hatua zinazofaa ziweze kuchukuliwa.

5) Jumla ya taarifa 21 zilizohusu shughuli mbali mbali zinazotekelezwa na Wizara, zilirushwa hewani kupitia televisheni ya *ZBC*, 23 kupitia *STAR TV* na 39 kupitia Redio ya *ZBC*. Aidha, taarifa 67 zilitolewa kupitia kipindi cha Mawio na taarifa 75 zilichapishwa katika gazeti la Zanzibar Leo. Taarifa hizo zilitayarishwa na Kitengo cha

Mawasiliano cha Wizara kwa lengo la kuwapatia taarifa wananchi, juu ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani za pekee kwa uongozi na watendaji wa vyombo hivi, kwa mashirikiano yao ya dhati kwa Wizara yangu.

6) Katika jitihada ya kutoa taarifa zaidi kwa jamii, Wizara imefungua tovuti yake (*www.mlec.go.tz*), ambapo hotuba hii pia inapatikana.

7) Ili kuimarisha ulinzi wa mali za Serikali, Wizara imeweza kufunga uzio wa umeme katika kuta zilizozunguka majengo ya Wizara.

Ofisi ya Waziri

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/2013, Ofisi ya Waziri ilipokea wageni wa aina mbalimbali, wakiwemo wananchi wa kawaida, Mabalozi na wawakilishi kutoka Mashirika na Taasisi za ndani na za kimataifa. Jumla ya wananchi 1,896 kutoka sehemu mbalimbali za Zanzibar walifika Ofisini kumuona Waziri kwa shughuli mbali mbali. Pia Waziri alipata fursa ya kutembelewa na kufanya mazungumzo na Balozi Mdogo wa China, Balozi Mdogo wa India, Meneja wa *"National Insurance Fund Tanzania*", Mtendaji Mkuu wa *ZANTEL*, Uongozi wa Muungano wa Vyama vya Ushirika Zanzibar, Uongozi wa Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi, ujumbe kutoka Shirika la Kazi Duniani, ujumbe kutoka Ras al Khayma, na ujumbe kutoka Kampuni ya Simu ya *VODACOM*.

Mhe. Spika, Ofisi hii vile vile imeratibu shughuli mbali mbali za maendeleo na za kijamii ambazo Waziri alishiriki. Jumla ya shughuli 54 alishiriki akiwa mgeni rasmi, miongoni mwao ni ufungaji wa Mkutano wa Chama cha Walimu cha Afrika Mashariki, uzinduzi wa Programu ya Kazi Nje Nje na kukabidhi fedha kutoka Mfuko wa Zakka kwa vikundi mbalimbali vya ushirika kwenye Wilaya zote za Zanzibar.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Waziri alipata nafasi ya kushiriki katika mikutano mbali mbali, ikiwemo Mkutano wa 102 wa Kimataifa wa Masuala ya Kazi uliofanyika Geneva, Switzerland, mwezi wa Juni 2013. Aidha, alipata fursa ya kufanya ziara za kikazi katika nchi mbalimbali zikiwemo Falme za Kiarabu, India, Oman, Vietnam, Zambia, Namibia, Switzerland na Ufaransa.

Malengo ya Idara ya Uendeshaji na Utumishi kwa mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara hii imekusudia kuendeleza utekelezaji wa malengo yafuatayo:

1. Kujenga uwezo wa wafanyakazi 29 waweze kutekeleza vyema majukumu yao;
2. Kuimarisha usalama wa majengo na mazingira yanayozunguka Wizara;
3. Kuimarisha kitengo cha utunzaji kumbukumbu;
4. Kuimarisha Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano;
5. Kimarisha mfumo wa usimamizi wa fedha na manunuzi;
6. Kutoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Wizara ili kuelimisha na kujenga taswira nzuri kwa umma; na Kusimamia haki na upatikanaji wa maslahi ya wafanyakazi;

Mhe. Spika, Ili Idara ya Uendeshaji na Utumishi iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2013/2014, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Mia Tano na Sabini na Moja (571,000,000/=) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi Milioni Mia Tisa Themanini na Tatu, Laki Nane na Elfu Ishirini na Sita (T.shs. 983,826,000/=) kwa ajili ya mishahara, mchango wa ZSSF na posho za wafanyakazi.

IDARA YA UENDELEZAJI NA URATIBU WA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

Mhe. Spika, kwa mwaka 2012/2013 Idara hii ilipanga kutekeleza yafuatayo:

1. Kujenga utamaduni wa ujasiriamali na kuimarisha uwezo wa wajasiriamali, hususan vijana, katika wilaya 10 za Zanzibar;

2. Kuimarisha usimamizi, ufuatiliaji na tathmini shirikishi ya shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi;
3. Kutanua soko la bidhaa za wajasiriamali wadogo wadogo; na

Kuijengea uwezo wa kiutendaji Idara ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2012/2013 Idara imetekeleza yafuatayo:

1) Imetoa mafunzo kwa vijana 120 (60 Unguja na 60 Pemba). Mafunzo hayo yalikusudia kushajihisha utamaduni wa

ujasiriamali kwa vijana ili waweze kujiajiri kwa kuanzisha biashara. Baadhi ya vijana waliopatiwa mafunzo hayo, wameweza kujiendeleza katika shughuli mbalimbali za kujipatia kipato na wengine wameanzisha kikundi cha ushirika kinachoitwa "*Graduate Entrepreneurs Consultancy Services Providers*" kinachotoa huduma za kibiashara, sheria na kazi za ufundi.

2) Imetoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wajasiriamali 150 (100 Unguja na 50 Pemba) kuhusu ufungashaji wa bidhaa, ubunifu wa mbinu za masoko na usimamizi wa biashara. Kutokana na mafunzo hayo, Wizara imeweza kuiunganisha Jumuia ya Wakulima wa mboga mboga (*UWAMWIMA*) kuuza mazao yao katika baadhi ya hoteli za mjini zikiwemo Maru Maru, Mtoni Marine, *Zanzibar Coffee, Green Garden* na Mkahawa wa Dolphin. Jumla ya wakulima 250 ambao ni wanachama wa Jumuia hiyo, wamenufaika na mpango huo na vijana 12 wamepata ajira ya kusambaza bidhaa katika mahoteli hayo.

3) Imeshirikiana na Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Tanzania kuwaunganisha wajasiriamali katika utaratibu wa kongano (*clusters*). Jumla ya kongano 5 (Unguja 3 na Pemba 2) zimeanzishwa, nazo ni: Kongano la mbogamboga, matunda na mazao ya viungo; Kongano la kuku; na Kongano la utalii kwa Unguja na Kongano la mbogamboga, matunda na mazao ya viungo na la ufugaji wa samaki kwa upande wa Pemba. Lengo la kuanzishwa kongano hizo ni kuimarisha mashirikiano miongoni mwa wajasiriamali ili waweze kusaidiana katika shughuli za uzalishaji na kutatua kwa pamoja changamoto zinazowakabili. Utaratibu huu pia utasaidia kuwafikia kwa urahisi wajasiriamali, ili kuwapatia huduma muhimu za kuwawezesha kuhimili ushindani na kutanua fursa za soko kwa bidhaa zao.

4) Jumla ya wajasiriamali 23 (wanawake 14 na wanaume 9) wamewezeshwa kushiriki katika maonesho ya Juakali/Nguvukazi yaliyofanyika Bujumbura nchini Burundi. Maonesho hayo yamewasaidia kutangaza biashara zao na kubadilishana uzoefu na wajasiriamali wenzao kutoka nchi mbali mbali za Jumuia ya Afrika Mashariki, walioshiriki katika maonesho hayo.

5) Katika kushughulikia changamoto ya soko kwa bidhaa za wajasiriamali wadogo wadogo, Idara iliandaa kongamano

kujadili changamoto hiyo. Masuala mbali mbali yanayohusiana na upatikanaji wa masoko yalijadiliwa yakiwemo uzalishaji, ubora wa bidhaa, viwango, vifungashio, pamoja na hati za uthibitisho, usajili na umiliki wa bidhaa. Aidha, changamoto kadhaa zinazokwaza upatikanaji wa soko kwa bidhaa za wajasiriamali ziliibuliwa, ikiwemo uwezo mdogo wa uzalishaji, kiwango hafifu cha ubora wa bidhaa na ukosefu wa huduma za msaada kwa kuendeleza biashara. Kufuatia kongamano hili, Kamati maalum imeundwa, ikijumuisha wajumbe kutoka Wizara zinazoshughulikia masuala ya Kazi, Biashara na Kilimo; Jumuia ya Wafanyabiashara, Wakulima, na Wenye Viwanda; Jumuia ya Wakulima wa Mboga Mboga; pamoja na wajasiriamali. Miongoni mwa majukumu ya kamati hii, ni kusaidia katika kushajihisha ushughulikiaji wa changamoto za upatikanaji wa soko kwa bidhaa za wajasiriamali wadogo wadogo. Mbali na kuundwa kwa Kamati hiyo, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika inaendelea kushirikiana na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko katika kuzishughulikia changamoto mbali mbali zinazokwaza maendeleo ya wajasiriamali wadogo wadogo, ikiwemo upatikanaji wa soko kwa bidhaa zao.

6) Jumla ya vikundi 35 na wajasiriamali 18 wanaojishughulisha na shughuli mbalimbali za kiuchumi, wamefuatiliwa na kupatiwa huduma za ushauri, ili kuwasaidia kukuza biashara zao.

7) Katika kuratibu shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi, Wizara imefanya mikutano minne (4) ya Kamati ya Kitaifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Mikutano hiyo inayofanywa katika kila kipindi cha miezi mitatu, huwa inajadili, pamoja na mambo mengine, utekelezaji wa mipango na shughuli za kuwawezesha wananchi kiuchumi katika sekta mbali mbali. Pia mikutano minne (4) ya Kamati za Uwezeshaji za Wilaya imefanyika. Kupitia mikutano hiyo, Kamati zimepatiwa miongozo kuhusu utayarishaji wa mipango kazi na jinsi ya kupata taarifa mbali mbali za shughuli za kiuchumi zinazofanywa na vijana na jamii kwa jumla. Aidha, mkutano mmoja uliowashirikisha waratibu wa programu na miradi mbali mbali inayolenga kuwawezesha wananchi kiuchumi ulifanyika. Programu/miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo; Mradi wa Usimamizi wa

Mazingira ya Ukanda wa Pwani; Programu ya Miundombinu ya Soko, Uongezaji Thamani ya Mazao ya Kilimo na Huduma za Fedha Vijijini; Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo; na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*). Mkutano huo ulielekeza kuweko utaratibu wa kupata taarifa za utekelezaji wa programu hizo katika masuala ya kuwawezesha wananchi kiuchumi. Hii itasaidia kujua nani anafanya nini na wapi, ili kuepuka migongano na kuweka taratibu juu ya namna ya kushirikiana. Aidha, itasaidia kupeana uzoefu juu ya mikakati inayofanya kazi vizuri na namna ya kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa programu na shughuli za kuwezesha wananchi.

8) Katika kuongeza hamasa juu ya masuala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, Wizara imekuwa ikiandaa maadhimisho ya Wiki ya Uwezeshaji kila mwaka. Kwa mwaka 2012/2013, maadhimisho hayo yalihusisha shughuli mbalimbali zikiwemo makongamano, utoaji wa fedha za Mfuko wa Zaka kwa kusaidia vikundi vya ushirika na vya wajasiriamali na mashindano ya uandishi wa Mpango wa Biashara. Lengo la maadhimisho haya vile vile ni kuihamasisha jamii kuhusu masuala ya uwezeshaji, ushirika, kazi na ajira, pamoja na kujenga uelewa wa jamii kuhusu kazi na majukumu ya Wizara.

Mhe. Spika, katika jitihada za kuimarisha masuala ya kuwawezesha wananchi kiuchumi, Serikali kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, imeajiri Mtaalamu wa masuala ya ujasiriamali kutoka India. Mtaalamu huyo amekuwa akitumiwa na taasisi mbali mbali katika kutoa mafunzo na ushauri juu ya masuala mbali mbali yanayohusiana na maendeleo ya ujasiriamali. Kupitia Mtaalamu huyo wizara imeweza kufanya mambo yafuatayo:

- Imefanya utafiti mdogo kuangalia uwezekano na namna ya kuanzisha vituo vya kulelea wajasiriamali nchini;

- Imeandaa Mpango wa kuanzisha vituo vya kulelea wajasiriamali na kuwasiliana na wahisani mbalimbali wa ndani na nje kusaidia utekelezaji wa mpango huo; na

- Imeandaa mapendekezo ya mradi ili kupata wahisani wa kuchangia uanzishwaji wa vituo vya kulelea wajasiriamali.

Kamisheni ya Sayansi na Teknolojia ya Tanzania imeonesha mwelekeo wa kusaidia suala hilo.

Mhe. Spika, Wizara yangu pia imekuwa ikishirikiana na taasisi nyengine katika juhudi za kuwawezesha wananchi kiuchumi. Kwa kushirikiana na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, jumla ya Shilingi Milioni Mia Tatu na Tatu (T.Shs. 303,000,000/=) kutoka Mfuko wa Zakka, zimetolewa kwa vyama vya ushirika na vikundi vya wajasiriamali 199 Unguja na Pemba. Lengo ni kusaidia kukuza shughuli zao za kiuchumi kwa madhumuni ya kuwapunguzia umasikini wanachama wao, ili nao hatimae waweze kutoa zakka.

Malengo ya Idara ya Uendelezaji na Uratibu wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka 2013/2014, Idara hii imekusudia kuendeleza utekelezaji wa malengo yafuatayo:

1. Kujenga utamaduni wa ujasiriamali na kuimarisha uwezo wa wajasiriamali, hususan vijana, katika Wilaya 10 za Zanzibar;
2. Kuimarisha usimamizi, huduma za ushauri, ufuatiliaji na tathmini shirikishi ya shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi;
3. Kutanua soko la bidhaa za wajasiriamali wadogo wadogo; na
4. Kuijengea Idara uwezo wa kiutendaji ili iweze kutekeleza majukumu yake.

Mhe. Spika**,** Ili Idara ya Uendelezaji na Uratibu wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2013/2014, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Themanini na Sita, Laki Tisa na Elfu Sabiini na Moja (T.Shs. 86,971,000/=) kwa matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA MIKOPO

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka 2012/2013, Idara hii ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kutoa mikopo 1,000 kwa vikundi vya kiuchumi na watu binafsi/mjasiriamali mmoja mmoja;
2. Kuongeza kiwango cha marejesho ya mikopo kutoka asilimia 85 hadi asilimia 95;
3. Kuimarisha uwekaji wa kumbukumbu za mikopo ;

4. Kuimarisha mashirikiano na mitandao na washirika wengine wanaojishughulisha na utoaji wa mikopo midogo midogo;
5. Kuanzisha fursa mpya za mikopo na kuimarisha miongozo ya usimamiaji mikopo;
6. Kuimarisha uwezo wa watendaji ili kuongeza ufanisi wa kazi;
7. Kuimarisha mazingira ya kazi; na
8. Kusimamia upatikanaji wa haki na maslahi ya wafanyakazi wa Idara.

Utekelezaji wa Malengo ya Idara ya Mikopo

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2012/2013, utekelezaji wa malengo kwa Idara hii ulikuwa kama ifuatavyo:

1) Jumla ya mikopo 193 (Unguja 142 na Pemba 51) yenye thamani ya Shilingi Milioni Mia Moja na Hamsini na Sita (Tshs. 156,000,000/=) imetolewa kupitia Mfuko wa Kujitegemea. Kati ya hizo, Shilingi Milioni Mia Moja na Kumi na Mbili (TShs. 112,000,000/=) zimetolewa Unguja na Shilingi Milioni Arobaini na Nne (TShs. 44,000,000/=) zimetolewa Pemba. (Angalia Kiambatanisho Nam. 4).

2) Idara imeendelea kuratibu shughuli za Mfuko wa JK/AK unaosimamiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar. Jumla ya mikopo 12 yenye thamani ya Shilingi Milioni Arobaini na Saba (TShs. 47,000,000/=) ilitolewa kwa wakopaji wa kuendelezwa (Angalia Kiambatisho Nam. 5).

3) Ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo umefanywa katika Wilaya zote za Unguja na Pemba. Hadi kufikia mwezi wa Juni 2013, jumla ya Shilingi Milioni Mia Moja Thelathini na Sita, Laki Moja Elfu Arobaini na Nne, Mia Moja na Hamsini (T.shs 136,144,150/=) zimerejeshwa katika Mfuko wa Kujitegemea Unguja na Pemba. Kati ya hizo, Unguja zimerejeshwa Shilingi Milioni Tisini na Sita, Laki Saba Elfu Kumi na Saba, Mia Moja na Hamsini (TShs. 96,717,150/-) na Pemba Shilingi Milioni Thelathini na Tisa, Laki Nne Elfu Ishirini na Saba (39,427,000/=), kama inavyooneshwa katika Kiambatisho Nam. 6. Kwa upande wa Mfuko wa JK/AK, jumla ya Shilingi Milioni Hamsini, Laki Tatu Elfu Sitini na Sita, Mia Sita Arobaini na Nane (T.shs. 50,366,648/=) zimerejeshwa kwa Unguja na Pemba (Angalia Kiambatisho Nam. 7).

4) Wakopaji wapya wamepatiwa mafunzo kuhusiana na urejeshaji wa mikopo, uwekaji wa kumbukumbu za hesabu, namna ya kujiwekea akiba na utafutaji wa masoko. Mafunzo haya yalitolewa ili kuwawezesha kufanya matumizi sahihi ya mikopo waliyopewa, kusimamia vizuri biashara zao na hatimae waweze kurejesha mikopo waliyochukua.

5) Shughuli za uchangishaji fedha kwa ajili ya kutunisha mfuko wa mikopo zimeendelezwa. Kamati iliyoundwa kwa ajili ya kusimamia shughuli hiyo imeendelea kukutana ili kufuatilia utekelezaji wa ahadi zilizotolewa. Hadi kufikia mwezi wa Juni 2013, asilimia 90 ya fedha zilizoahidiwa zimekusanywa na shughuli ya uchangiaji inaendelea. Natoa shukrani za dhati kwa wale wote waliochangia katika utunishaji wa Mfuko huu.

6) Ili kuimarisha uratibu katika utoaji wa mikopo midogo midogo, Idara imeanzisha mtandao wa taasisi zinazotoa huduma za kifedha kwa wajasiriamali wadogo. Mtandao huo umejumuisha taasisi mbali mbali zinazotoa mikopo midogo midogo, zikiwemo *WEDTF*, *YOSEFO*, *CRDB*, Changamoto, Meli Nne *SACCOS* na Jumuia ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima Zanzibar. Lengo la mtandao huo ni kubadilishana taarifa za wakopaji, ili kuweza kutathmini idadi ya watu wanaofikiwa kwa huduma za mikopo na pia kuimarisha mashirikiano katika utoaji wa huduma hizo. Hii itasaidia pia kubainisha thamani na aina ya mikopo ambayo hutolewa na taasisi mbali mbali kwa wajasiriamali.

7) Ili kupata uzoefu katika masuala ya mikopo, watendaji wanne wa Idara wamefanya ziara za kujifunza kwa taasisi zinazotoa mikopo huko Tanzania Bara. Taasisi zilizotembelewa ni *FINCA* na *BLUE* Finance zilizoko Dar es Salaam. Pia ziara za ndani kwa wafanyakazi wa Idara baina ya Unguja na Pemba zilifanyika kwa lengo la kubadilishana uzoefu.

8) Wafanyakazi watatu (Unguja wawili na Pemba mmoja) wamegharamiwa kuchukua mafunzo ya muda mrefu katika fani ya mikopo na ujasiriamali; utawala; na usimamizi wa rasilimali watu (kwa ngazi ya shahada ya kwanza, cheti na diploma). Pia wafanyakazi watatu (Unguja mmoja na Pemba wawili) wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

MALENGO YA IDARA YA MIKOPO KWA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara hii imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kutoa mikopo 1,000 kwa vikundi vya kiuchumi na watu binafsi/mjasiriamali mmoja mmoja yenye thamani ya TShs. 300,000,000/=;
2. Kuongeza kiwango cha marejesho ya mikopo kutoka asilimia 85 hadi zaidi ya asilimia 95;
3. Kuimarisha uwekaji wa kumbukumbu za mikopo; na
4. Kuimarisha mashirikiano na uratibu wa shughuli za mikopo nafuu hapa nchini;

Mhe. Spika**,** Ili Idara ya Mikopo iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2013/2014, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe Shilingi Milioni Mia Moja Tisini na Nane, Laki Moja Elfu Sabini na Nne (T.Shs. 198,174,000/=) kwa matumizi ya kawaida.

IDARA YA USHIRIKA

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2012/2013 Idara ya Ushirika ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kuanza maandalizi ya kuanzisha Benki ya Ushirika Zanzibar;
2. Kuimarisha uwezo wa kiutendaji wa vyama vya ushirika 200;
3. Kusimamia utekelezaji wa sheria katika uendeshaji wa vyama vya ushirika;
4. Kuimarisha utawala bora katika uendeshaji wa vyama vikuu 6 vya ushirika na Shirikisho la Vyama vya Ushirika *(Cooperative Union of Zanzibar - CUZA);*
5. Kuimarisha ushirikiano na washirika wa masuala ya ushirika; na
6. Kuimarisha mazingira ya kazi, ikiwemo mafunzo kwa wafanyakazi na upatikanaji wa vifaa.

Utekelezaji wa Malengo ya Idara ya Ushirika

Mhe. Spika**,** katika mwaka wa fedha wa 2012/2013**,** Idara ya Ushirika imetekeleza mambo yafuatayo:

1) Imefanya tathmini juu ya uwezekano wa kuanzisha Benki ya Ushirika Zanzibar. Tathmini hiyo imebainisha umuhimu wa kuwepo kwa benki ya ushirika, ingawa sekta ya ushirika peke yake haitoshi kugharamia mtaji wa uanzishwaji wake.

Mapendekezo ya tathmini hiyo ni kuhusisha washirika wengine kwa utaratibu wa ubia, ili kuchangia mtaji wa uanzishwaji wa benki hiyo. Wizara imeelekezwa kushirikiana na Ofisi ya Rais (Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo) na Wizara inayoshughulikia masuala ya Wanawake (ambayo nayo ilikuwa na dhamira ya kuanzisha Benki ya Wanawake), ili kulifanyia kazi suala hili, kwa mtazamo wa kuanzisha Benki ya Jamii, itayotoa huduma kwa wanawake, vyama vya ushirika na wajasiriamali wengine.

2) Katika kusimamia utekelezaji wa sheria kwenye vyama vya ushirika, Idara imefanya upekuzi na kutoa mafunzo ya vitendo kwa vyama vya ushirika 1,222 (844 Unguja na 378 Pemba). Aidha, vyama vya ushirika 191 (139 Unguja na 52 Pemba) vimefanyiwa ukaguzi wa hesabu. Kati ya vyama hivyo vilivyofanyiwa ukaguzi wa hesabu, 49 ni SACCOS na 142 ni vyama vya uzalishaji mali na huduma. Lengo la ukaguzi huo ni kutambua hali halisi ya kifedha ya vyama hivyo na kutoa ushauri wa kitaalamu. Matokeo ya kaguzi hizo yameonesha kuwa bado kunahitajika elimu zaidi ya kuimarisha utendaji na udhibiti wa raslimali, ili kuleta tija kwenye vyama vya ushirika.

3) Ili kutanua huduma za kifedha kwa shughuli za kiuchumi miongoni mwa wananchi, mijini na vijijini, Idara ya Ushirika imesajili *SACCOS* Benki 8 Unguja na Pemba. Hii inafanya jumla ya *SACCOS* Benki kuwa 17 (10 Unguja na 7 Pemba), zikiwa na mtaji wa jumla ya Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Mbili na Sita, Laki Tatu Elfu Arobaini na Moja na Mia Tatu Sabini na Saba (T.Shs. 2,206,341,377/=).

4) Jumla ya vyama vya ushirika 50 vimepatiwa mafunzo shirikishi ya uandaaji wa mipango ya biashara. Mipango hiyo ya biashara imekamilika na tayari vyama husika vimeunganishwa na taasisi za kifedha kwa ajili ya kupata mikopo ya kuiendeleza. Miradi iliyoandikiwa kupitia mipango hiyo ya biashara, imehusisha shughuli za kilimo cha mbogamboga, ufugaji wa kuku, ukamuaji wa mafuta, utengenezaji wa mapambo yanayotokana na kombe za chaza, uvuvi, kazi za mikono na ushonaji.

5) Ili kuimarisha utawala bora katika uendeshaji wa vyama vikuu vya ushirika na Shirikisho la Ushirika Zanzibar, viongozi 40

wa vyama vikuu na wa Shirikisho hilo wamepatiwa mafunzo kuhusu masuala ya utawala bora. Mafunzo hayo yamesaidia kuvihuisha vyama vikuu hivyo, ambapo vimeitisha mikutano ya vyama na wanachama wao, vimefanya mapitio ya sheria zao ndogo ndogo pamoja na kufanya chaguzi za viongozi kwa mujibu wa sheria.

6) Mafunzo ya kuandaa Mpango Mkakati yametolewa kwa viongozi wa Vyama Vikuu 6 (vinne Unguja na viwili Pemba) pamoja na viongozi wa Shirikisho la Ushirika Zanzibar. Jumla ya viongozi 30 (wanawake watano na wanaume ishirini na tano) wamepatiwa mafunzo hayo. Kutokana na mafunzo hayo, vyama hivyo vimeweza kuandaa mipango mikakati ya vyama vyao. Mipango mikakati hiyo imeonesha dira na dhamira ya vyama vikuu hivyo, pamoja na malengo wanayotarajia kuyafikia kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo (2013 hadi 2015).

7) Viongozi wa vyama vikuu 6 na wa Shirikisho la Ushirika Zanzibar wamepatiwa mafunzo ya uongozi pamoja na mafunzo juu ya ubunifu, mbinu za ushindani wa biashara, utafutaji masoko, uanzishaji wa kongano na mitandao ya kutanua fursa za biashara. Pia walipatiwa mafunzo yanayohusu mbinu za kuongeza tija katika uzalishaji na utoaji huduma; ufuatiliaji na tathmini; na uandishi wa ripoti za utekelezaji wa shughuli zao. Jumla ya viongozi 29 walishiriki katika mafunzo hayo. Matokeo yameonesha kuimarika upeo na mitizamo ya viongozi wa vyama vikuu na wa Shirikisho la Ushirika, hali iliyowezesha kuipitia upya mipango mikakati ya vyama vyao.

8) Idara imeratibu maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani. Miongoni mwa shughuli zilizofanyika ni kongamano lililojadili maendeleo na changamoto zinazoikabili sekta ya ushirika Zanzibar. Changamoto zilizoibuliwa zimeanza kufanyiwa kazi kwa kutoa mafunzo ya kuimarisha mbinu za uongozi katika vyama vya ushirika, kuviwezesha vyama vya ushirika kuandaa miradi ya kiuchumi na kuviunganisha na taasisi zinazotoa mikopo, kutoa mafunzo yanayohusu ubunifu na mbinu za ushindani wa biashara kwa vyama vikuu vya ushirika pamoja na kuvishirikisha vyama vya ushirika vya uzalishaji katika maonesho ili kutangaza biashara zao.

Malengo ya Idara ya Ushirika kwa Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika**,** kwa kipindi cha mwaka 2013/2014, Idara hii imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kuongeza uelewa wa wanachama 3,000 juu ya wajibu, haki na ushiriki katika vyama vya ushirika;
2. Kusimamia utekelezaji wa sheria katika uendeshaji wa vyama vya ushirika 1,200;
3. Kuwezesha uanzishwaji wa vyama viwili vya ushirika vya uzalishaji vinavyohusisha vijana;
4. Kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa kuendeleza vyama vya ushirika;
5. Kuimarisha utendaji wa vyama vikuu 6 na Shirikisho la Vyama vya Ushirika (*CUZA*);
6. Kuimarisha mahusiano na washirika wa sekta ya ushirika; na
7. Kuimarisha mazingira ya kazi, ikiwemo mafunzo kwa wafanyakazi na upatikanaji wa vifaa.

Mhe. Spika**, i**li Idara ya Ushirika iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2013/2014, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi Milioni Hamsini na Tano, Laki Nane Sabiini na Saba Elfu (T.Shs. 55,877,000/=) kwa matumizi ya kazi za kawaida.

KAMISHENI YA KAZI

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/2013 Kamisheni ya Kazi ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kusimamia utekelezaji wa sheria za kazi, sera na programu zinazohusu masuala ya kazi;
2. Kujenga uwezo katika usimamizi wa utekelezaji wa mikataba ya kimataifa ya kazi;
3. Kuimarisha mfumo wa usuluhishi na uamuzi wa migogoro ya kazi;
4. Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Kupambana na Ajira za Watoto;
5. Kuimarisha uhusiano na majadiliano ya pamoja katika sehemu za kazi; na
6. Kuimarisha mashirikiano ya kitaifa, kikanda na kimataifa kuhusu masuala ya kazi.

Utekelezaji wa Malengo ya Kamisheni ya Kazi

Mhe. Spika**,** katika kipindi cha mwaka 2012/2013, shughuli zifuatazo zimetekelezwa kupitia Kamisheni ya Kazi:

1) Kanuni tano (5) za Sheria ya Ajira Nambari 11 ya mwaka 2005 zimetayarishwa na kuanza kutumika. Kanuni hizo zinahusu maslahi ya wafanyakazi katika sekta binafsi, usajili na utendaji kazi wa Vyama vya Wafanyakazi, mikataba, likizo bila ya malipo na makundi maalum ya wafanyakazi. Kukamilika kwa kanuni hizi kutarahisisha utekelezaji wa Sheria za Kazi katika maeneo yaliyotajwa.

2) Elimu juu ya sheria, kanuni za kazi na miongozo imetolewa kupitia vipindi vya redio na televisheni. Jumla ya vipindi kumi na nne (14) vya redio viliandaliwa na kurushwa hewani, kumi (10) kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar na vinne (4) kupitia redio binafsi ya Bomba FM. Vipindi vya redio kupitia Bomba FM vilirushwa hewani moja kwa moja, ambapo wananchi walipata nafasi ya kuuliza masuala mbali mbali juu ya sheria za kazi na kupatiwa majibu papo hapo. Kwa upande wa vipindi vya televisheni, jumla ya vipindi sita (6) vilirushwa hewani kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar. Aidha, taasisi kumi (10) zimetembelewa na kupatiwa elimu ya sheria za kazi. Taasisi hizo ni *SHA High School, Al-Hidaya Islamic High School*, Skuli ya Mbarali, Hoteli ya Karafuu, Hoteli ya Bwawani, *Coconut Beach Hotel*, *Africa Hotel, Tantax Co. Ltd, Zainab Bottlers* na *Zanzibar Bottlers*. Lengo ni kunyanyua uelewa wa wafanyakazi, waajiri na jamii kwa jumla juu ya sheria, kanuni, miongozo na masuala ya kazi kwa jumla.

3) Jumla ya taasisi 240 (200 Unguja na 40 Pemba) zimefanyiwa ukaguzi kazi. Miongozo imetolewa juu ya mapungufu yaliyobainika na kuagiza kurekebishwa kasoro hizo. Aidha hatua mbalimbali za kisheria zimechukuliwa dhidi ya wale waajiri ambao walionekana kukiuka Sheria za Kazi kwa makusudi, licha ya ushauri uliotolewa awali wa kurekebisha kasoro hizo. Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na kuwapeleka mahakamani, ambapo kesi mbili zilifunguliwa katika Mahakama ya Wilaya ya Mwanakwerekwe. Hatua hizi zimesaidia kuwakumbusha waajiri na waajiriwa juu ya kutimiza wajibu wao kama inavyoelekezwa katika sheria za kazi.

4) Mafunzo juu ya utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ya Shirika la Kazi Duniani yametolewa. Mafunzo hayo yalishirikisha washiriki kutoka Jumuiya ya Waajiri Zanzibar,

Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi Zanzibar, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na taasisi nyengine mbali mbali za Serikali. Lengo la mafunzo hayo ni kujenga uwezo wa taasisi hizo juu ya utekelezaji wa Mikataba ya Shirika la Kazi Duniani, ambayo nchi yetu imeridhia.

5) Kitengo cha Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro ya Kazi kimeimarishwa kwa kupatiwa vitendea kazi vinavyohitajika, ili kiweze kufanya kazi zake kwa ufanisi. Katika kipindi cha Julai 2012 hadi Juni 2013, jumla ya migogoro 179 imepokelewa kwa ajili ya usuluhishi. Kati ya migogoro hiyo, migogoro 136 (sawa na asilimia 76) imesuluhishwa. Aidha, migogoro 16 (sawa na asilimia 9) imeamuliwa na migogoro 27 (sawa na asilimia 15) inaendelea kusikilizwa. Kuwepo kwa kitengo hiki ndani ya Wizara kumesaidia kupunguza mrundikano mkubwa wa kesi katika Mahakama ya Kazi, kwani tokea kuanzishwa kwake Mahakama ya Kazi haijapokea kesi mpya. Hii ni kwa sababu migogoro yote ya kazi sasa inaanza kushughulikiwa katika kitengo hiki. Mahakama ya Kazi huwa inafanya mapitio tu katika kesi ambazo pande husika hazikuridhika na maamuzi ya Kitengo cha Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro. Vile vile, kuimarika kwa kitengo hiki kumesaidia kuharakisha utatuzi wa migogoro. Kati ya migogoro 179 iliyosajiliwa katika kitengo hicho, jumla ya migogoro 40 sawa na asilimia 22 imetatuliwa ndani ya kipindi kisichozidi wiki tatu baada ya kusajiliwa. Hali hii imesaidia pia katika upatikanaji wa haki kwa haraka na kuimarisha mahusiano mema kazini.

6) Kikao cha pamoja cha Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya Kupambana na Ajira Mbaya za Watoto (*Zanzibar Child Labour Stearing Committee*) kilifanyika. Lengo la kikao hicho lilikuwa ni kuandaa mikakati ya kuimarisha utekelezaji wa Mpango wa Kupambana na Ajira Mbaya za Watoto Zanzibar kwa kipindi cha 2009/2005. Kamati hiyo inazihusisha taasisi za Serikali zinazohusika na masuala haya, Jumuiya ya Waajiri Zanzibar, Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi Zanzibar na asasi mbalimbali za kiraia.

7) Jumla ya vikao vinne vya Bodi ya Ushauri wa Mambo ya Kazi vimefanyika. Bodi hii inayoundwa kwa mfumo wa UTATU, imekutana na kujadili mambo mbalimbali yanayohusiana na masuala ya kazi, ikiwemo taarifa za

utendaji kazi za kila robo mwaka za Kamisheni ya Kazi, changamoto zinazoikabili sekta ya kazi na mbinu za kupambana nazo. Vikao viwili vya Kamati ya Utatu (*Tripartite Committee*) pia vimefanyika na kujadili juu ya utendaji kazi wa Kitengo cha Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro ya Kazi. Bodi ya Ushauri wa Mambo ya Mishahara nayo pia imekutana ambapo, pamoja na mambo mengine, imejadili juu ya utekelezaji wa ulipaji wa kima cha chini cha mishahara katika sekta binafsi.

8) Jumla ya matawi tisa (9) ya vyama vya wafanyakazi Unguja na Pemba na Jumuiya ya Waajiri Zanzibar yametembelewa kupitia Ofisi ya Mrajis wa Vyama vya Wafanyakazi, kwa lengo la kuwakumbusha juu ya umuhimu wa kufuata sheria ya mahusiano kazini katika utekelezaji wa shughuli zao za kila siku. Madhumuni ya msingi ni kusaidia katika kujenga mahusiano mema kazini na kuimarisha Utawala Bora katika vyama vya wafanyakazi.

9) Katika kuimarisha mashirikiano juu ya masuala yanayohusu sekta ya kazi, uongozi wa Wizara pamoja na wawakilishi kutoka Jumuia ya Waajiri na Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi walishiriki katika Mkutano wa 102 wa Shirika la Kazi Duniani, uliofanyika Geneva nchini Uswisi, mwezi wa Juni 2013. Mkutano huo, pamoja na mambo mengine, umejadili masuala mbali mbali ikiwemo ukuzaji wa ajira na utekelezaji wa mikataba ya kimataifa inayohusu masuala ya kazi. Ushiriki wa Zanzibar katika mkutano huo ni muhimu katika kuendeleza mashirikiano kati ya Zanzibar na Shirika la Kazi Duniani pamoja na nchi nyengine wanachama wa Shirika hilo.

Malengo ya Kamisheni ya Kazi kwa Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, katika kutekeleza majukumu yake kwa kipindi cha mwaka 2013/2014, Kamisheni ya Kazi imepanga kuendeleza utekelezaji wa malengo yafuatayo:

1. Kuimarisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikataba minane (8) ya kimataifa inayohusu masuala ya kazi pamoja na mapendekezo ya Shirika la Kazi Duniani;
2. Kukuza uelewa wa sheria za kazi kwa jamii;
3. Kuimarisha usuluhishi na uamuzi wa migogoro ya Kazi;

4. Kuimarisha uhusiano na majadiliano ya pamoja katika sehemu za kazi;
5. Kuendeleza mashirikiano ya kikanda, kitaifa na kimataifa katika masuala yanayohusu sekta ya kazi; na
6. Kuratibu utekelezaji wa Programu ya Kupambana na Ajira Mbaya za Watoto.

Mhe. Spika, **i**li Kamisheni ya Kazi iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2013/2014, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi Milioni Mia Moja Arobaini na Saba na Elfu Kumi na Mbili (T.Shs. 147,012,000/=) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi Milioni Hamsini (T.Shs. 50,000,000/=) kwa kazi za maendeleo.

IDARA YA AJIRA

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2012/2013 Idara hii ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji na uwekaji wa taarifa za soko la ajira;
2. Kuzalisha ajira zipatazo 2,000 kupitia sekta mbali mbali za umma na binafsi;
3. Kushajihisha jamii kuchukuwa hatua juu ya masuala ya ajira kwa vijana;
4. Kurasimisha ajira isiyo rasmi kwa kuanzia na sekta ya usafirishaji wa umma kwa kushirikiana na taasisi husika; na
5. Kuimarisha mtandao na mashirikiano na washirika mbalimbali juu ya masuala ya ajira.

Utekelezaji wa Malengo ya Idara ya Ajira

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2012/2013, shughuli zifuatazo zimetekelezwa kupitia Idara hii:

1) Katika kuimarisha upatikanaji wa taarifa za soko la ajira, Idara imeandaa mfumo wa ukusanyaji na utoaji wa taarifa hizo, chini ya utaalamu elekezi wa Shirika la Kazi Duniani na Chuo cha Ustawi wa Jamii cha Dar-es-salaam. Mfumo huo ambao uko katika hatua za mwisho kukamilishwa, utawezesha kufuatilia na kukusanya taarifa mbali mbali zinazohusu ajira, ikiwemo fursa za ajira katika sekta za umma na binafsi. Mkutano uliohusisha taasisi mbalimbali za umma na binafsi ulifanywa ili kupata maoni juu ya kuufanyia kazi mfumo huo.

2) Kupitia Programu ya Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali (inayosimamiwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali), Idara pia imetoa mafunzo ya siku sita ya nadharia juu ya mfumo wa taarifa za soko la ajira. Mafunzo hayo yalishirikisha watendaji 22 (wanaume 13 na wanawake 9) wa taasisi zinazohusiana na ukusanyaji wa taarifa za kazi/ajira. Lengo lilikuwa ni kujenga uwezo juu ya utumiaji wa mfumo huo, pamoja na kujenga misingi ya ushirikiano katika kufanikisha utekelezaji wake. Aidha, mafunzo ya siku sita ya vitendo juu ya ukusanyaji wa taarifa za ajira, yalitolewa kwa kamati ya kitaalamu yenye watendaji 13 (wanaume 8 na wanawake 5) iliyotokana na mafunzo ya awali. Vile vile, watendaji sita (6) wa Wizara walifanya ziara ya mafunzo nchini Afrika ya Kusini kwa lengo la kujifunza zaidi jinsi ya kuendesha mfumo wa ukusanyaji na utoaji wa taarifa za soko la ajira.

3) Kwa mashirikiano na taasisi mbali mbali, Wizara kupitia Idara ya Ajira, imeendelea kuishughulikia changamoto ya upatikanaji wa ajira. Katika mnasaba huo, imeendelea na shughuli ya kuorodhesha watafuta kazi ikiwa ni pamoja na juhudi za kuwaunganisha na waajiri. Jumla ya vijana 464 wameorodheshwa, ambapo vijana 350 wamefanikiwa kuajiriwa ndani na nje ya nchi. Aidha, kutokana na taarifa zilizokusanywa kutoka kwa waajiri wa baadhi ya taasisi na Mawakala Binafsi wa Ajira, katika kipindi cha Julai 2012 hadi Machi 2013, jumla ya vijana 1,529 wameajiriwa katika taasisi binafsi na vijana 215 wamepata ajira nje ya nchi (Angalia Viambatanisho Nam. 8a na 8b).
4) Idara imetoa mafunzo kwa vijana 60 (wanawake 28 na wanaume 32) wenye elimu ya ngazi ya Diploma na Shahada ya Kwanza, juu ya kubadilisha mitizamo yao kuhusu ajira na wawe na tabia ya kujituma na kutochagua kazi. Mafunzo hayo pia yalilenga kuwaraghabisha vijana hao watumie fursa zilizopo kujiajiri. Kati ya vijana 60 waliopatiwa mafunzo, vijana 32 waliraghibika ndani ya kipindi cha mafunzo hayo na waliomba kupatiwa mafunzo zaidi. Baadhi yao tayari wameanzisha kazi za ujasiriamali na wanaendelea kufuatiliwa kwa kupatiwa ushauri zaidi.
5) Katika kutanua fursa za ajira, Wizara imefanya mawasiliano na nchi za Oman na Qatar kuhusu mashirikiano ya kupeleka wafanyakazi kwenye nchi zao. Rasimu za mikataba na nchi hizo ziko tayari na wakati wowote zitasainiwa.

6) Katika juhudi za kushajihisha jamii kuchukuwa hatua juu ya masuala ya ajira kwa vijana, idara imeandaa jumla ya vipindi 13 vya redio na vitano (5) vya televisheni vilivyozungumzia masuala ya ajira. Vipindi hivyo vimerushwa hewani kupitia redio na televisheni za Shirika la Utangazaji la Zanzibar na redio ya "*Hits FM*".
7) Idara imeanza mchakato wa kurasimisha shughuli za sekta isiyo rasmi, kwa kuanzia na sekta ya usafiri wa umma. Lengo la hatua hii ni kutengeneza ajira rasmi, ambazo zitachangia kuongeza fursa za kazi za staha, kuinua pato la taifa pamoja na kukuza uchumi kwa ujumla. Mkutano mmoja ulioshirikisha viongozi kutoka sekta ya usafiri wa umma na taasisi za huduma ikiwemo Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Bodi ya Mapato ya Zanzibar, Manispaa, Bima na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano umefanywa. Mkutano huo, pamoja na mambo mengine, ulijadili namna ya kurasimisha sekta hii ili iweze kuchangia katika kukuza ajira za staha na uchumi wa taifa. Wajumbe wa mkutano huo walikubaliana kuwa, kwa kuanzia, kuwepo na mikataba ya kazi kwa wafanyakazi wa sekta ya usafirishaji pamoja na kujiunga na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Aidha, Idara imetoa taaluma juu ya Sera ya Ajira na Sheria za Kazi kwa wamiliki wa taxi, daladala, gari za abiria za shamba na gari za mizigo bandarini pamoja na wawakilishi kutoka Idara inayosimamia leseni na usafiri, Jeshi la Polisi, Bodi ya Mapato ya Zanzibar na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.
8) Idara imefanya makongamano mawili yaliyowahusisha waajiri na Kamati za Kukuza Ajira za Wilaya. Makongamano hayo yalizihusisha Wilaya za Kaskazini B, Kusini na Magharabi kwa Unguja na Wilaya za Chake Chake na Mkoani kwa Pemba. Lengo la makongamano hayo ilikuwa ni kukuza mashirikiano katika masuala ya uzalishaji ajira, ambapo waajiri walikubali kuwa na mikutano ya mara kwa mara na kamati hizo, ili kujadili namna ya ukuzaji wa ajira katika wilaya zao.
9) Ili kuimarisha mashirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi juu ya masuala ya ajira, Idara imetoa mafunzo kwa taasisi sita za wakala binafsi wa ajira zilizosajiliwa na kupatiwa leseni. Lengo la mafunzo hayo ilikuwa ni kuwajulisha kuhusu mikataba ya kimataifa juu ya uwakala wa ajira, sera na sheria zinazohusu kazi na ajira na wajibu wa Wakala wa Ajira katika kukuza ajira. Katika mafunzo hayo, Wakala hao pia walieleweshwa kuhusu mipango ya Serikali katika kukuza ajira, pamoja na umuhimu wa Wakala katika suala la uadilifu juu ya mahusiano na waomba kazi.

10) Katika kuimarisha mashirikiano na washirika wa masuala ya ajira ndani na nje ya nchi, Idara ilishiriki katika mikutano mbalimbali, ikiwemo inayohusu utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki na inayohusu mashirikiano na nchi nyengine katika masuala ya ajira.

Malengo ya Idara ya Ajira kwa Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka 2013/2014 Idara hii imekusudia kuendelea kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji na uwekaji wa taarifa za soko la ajira;
2. Kuzalisha ajira zipatazo 2,000 kwa vijana kwa kushirikiana na sekta binafsi;
3. Kushajihisha jamii kuhusu masuala ya ajira kwa vijana;
4. Kukamilisha utaratibu wa kurasimisha sekta isiyo rasmi ya usafirishaji kwa kushirikiana na taasisi nyengine zinazohusika;
5. Kuimarisha mashirikiano na sekta binafsi na nchi marafiki katika ukuzaji wa ajira;
6. Kuimarisha mtandao na mashirikiano na washirika mbali mbali juu ya masuala ya ajira; na
7. Kuimarisha uwezo wa Idara iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mhe. Spika, **i**li Idara ya Ajira iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka 2013/2014, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Mia Moja Ishirini, Laki Nne na Elfu Tisini na Nane (T.Shs. 120,498,000/=) kwa matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA USALAMA NA AFYA KAZINI

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2012/2013 Idara hii ilipanga kutekeleza malengo matano yafuatayo:

1. Kuimarisha mfumo wa ukaguzi wa hali ya usalama na afya katika sehemu za kazi;
2. Kukuza uelewa wa waajiri, wafanyakazi na jamii kwa jumla juu ya Sheria Nambari 8 ya Usalama na Afya Kazini ya mwaka 2005;
3. Kuimarisha utendaji kazi wa Kamati ya Usalama na Afya Kazini;

4. Kujenga uwezo wa watendaji wa Idara katika kusimamia utekelezaji wa Sheria Nambari 8 ya Usalama na Afya Kazini ya mwaka 2005; na
5. Kuimarisha mashirikiano na uratibu wa masuala ya usalama na afya kazini.

Utekelezaji wa Malengo ya Idara ya Usalama na Afya Kazini

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Idara ya Usalama na Afya Kazini imetekeleza shughuli zifuatazo:

1) Imezisajili jumla ya sehemu za kazi 71 (62 Unguja na 9 Pemba) ili kuzitambua na kuweka taarifa zao kwenye daftari la usajili wa sehemu za kazi. Hii itarahisisha shughuli za ukaguzi kwa kutambua mapema mazingira ya kazi zao, hatari zinazoweza kutokea katika sehemu hizo na hivyo kutoa ushauri na maelekezo yanayofaa, kabla ya kutokea tatizo.
2) Imezikagua sehemu za kazi 186 (135 Unguja na 51 Pemba) ili kuangalia hali ya usalama na afya katika maeneo hayo. Ushauri ulitolewa juu ya kurekebisha kasoro zilizobainika. Ufuatiliaji uliofanywa baada ya ukaguzi, umeonesha kuwa kasoro nyingi zimerekebishwa baada ya kufuatwa ushauri uliotolewa.
3) Imekamilisha rasimu ya muongozo juu ya masuala ya usalama na afya kazini, inayojumuisha mambo ya UKIMWI, pamoja na rasimu ya muongozo wa kupima afya za wafanyakazi. Miongozo hii itasaidia kuweka utaratibu mzuri wa kusimamia masuala haya kwenye sehemu za kazi. Pia Idara imeendelea na matumizi ya 'checklist' kwenye ukaguzi wa masuala ya usalama na afya kwenye sehemu za kazi, ili kuhakikisha kuwa masuala yote yanayohitajika kukaguliwa yanaangaliwa kwa kina.
4) Katika kukuza uelewa wa masuala ya usalama na afya kazini, Idara imeandaa na kurusha hewani kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar jumla ya vipindi vitatu (3) vya radio na vipindi viwili (2) vya televisheni. Pia Idara imetayarisha vipeperushi vyenye mada tofauti na kuvisambaza kwenye maeneo ya kazi na kwa jamii. Vile vile Idara imetoa mafunzo kwa waratibu 50 (33 Unguja na 17 Pemba) wa masuala ya usalama na afya kazini kutoka kwenye Wizara na taasisi za umma. Pamoja na hayo, imetoa mafunzo kwa wajumbe wanne (mwanamke mmoja na wanaume watatu) wa Kamati ya Usalama na Afya Kazini ili kuwaongezea uwezo wa kusimamia majukumu yao.

5) Katika kujenga uwezo wa kusimamia utekelezaji wa Sheria Nambari 8 ya Usalama na Afya Kazini ya mwaka 2005, Idara imewapatia mafunzo ya vitendo ya muda mfupi wafanyakazi wawili wanaume, kwenye Mamlaka ya Usalama na Afya Kazini ya Tanzania Bara.
6) Ili kukuza mashirikiano na uratibu wa masuala ya usalama na afya kazini, Idara ilifanya mkutano na washirika wanaohusika na masuala haya. Washiriki wa mkutano huo walikubaliana kuendeleza mashirikiano na kubadilishana taarifa. Pia vikao vinne (4) vya Kamati ya Usalama na Afya Kazini, yenye sura ya utatu, vimefanyika kama inavyotakiwa. Vikao hivyo, pamoja na mambo mengine, vilijadili taarifa za utekelezaji wa shughuli mbali mbali za Idara.

Malengo ya Idara ya Usalama na Afya Kazini kwa mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Idara hii imepanga kuendelea kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kuimarisha utekelezaji wa Sheria Nambari 8 ya mwaka 2005 ya Usalama na Afya Kazini;
2. Kukuza uelewa wa waajiri, wafanyakazi na jamii kwa jumla juu ya Sheria Nambari 8 ya Usalama na Afya Kazini ya mwaka 2005;
3. Kusimamia sehemu za kazi ili kuhakikisha kuwa zinafuata na kutekeleza sheria, kanuni na miongozo ya Usalama na Afya Kazini;
4. Kuimarisha uwezo wa Idara ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo; na
5. Kuimarisha mashirikiano na uratibu wa masuala ya usalama na afya kazini.

Mhe. Spika, ili Idara ya Usalama na Afya Kazini iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2013/2014, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi Milioni Themanini na Mbili, Laki Mbili na Elfu Hamsini na Moja (Tshs 82,251,000/=) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

OFISI KUU PEMBA

Mhe. Spika, Ofisi Kuu Pemba inasimamia shughuli zote za Wizara kwa upande wa Pemba. Hivyo, utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hii kwa mwaka 2012/2013 na malengo ya utekelezaji kwa mwaka 2013/2014 ni kama ambavyo imeainishwa katika maelezo yaliyotolewa kwa kila Idara, ambayo yamehusisha pia na Pemba.

Mhe. Spika, ili kuiwezesha Ofisi Kuu Pemba kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Mia Mbili Ishirini na Nne, Laki Tatu Elfu Nane (T.Shs. 224,308,000/=) kwa kazi za kawaida na Shilingi Milioni Mia Mbili (T.Shs. 200,000,000/=) kwa ajili ya mishahara, mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na posho za wafanyakazi.

SHUKRANI

Mhe. Spika, wizara yangu inatambua na kuthamini michango ya Washirika wa Maendeleo katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, itaendeleza mashirikiano na washirika hao katika kufanikisha dhamira na malengo yake. Napenda kuchukua nafasi hii adhimu kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuwashukuru kwa dhati washirika wetu wa maendeleo waliosaidia kwa namna mbali mbali katika kufanikisha utekelezaji wa mipango ya kuendeleza kazi za staha, kukuza ajira na kuwawezesha wananchi kiuchumi. Washirika hao wa maendeleo ni pamoja na nchi wahisani, ikiwemo China, India, Marekani, Ufaransa na Afrika Kusini na Mashirika ya Kimataifa, yakiwemo Shirika la Kazi Duniani (*ILO*); Mashirika ya Umoja wa Mataifa; *IFAD*; *AFDB* na *Save the Children*.

Mhe. Spika, Katika utekelezaji wa majukumu yake, Wizara yangu pia ilishirikiana kwa karibu na Wizara na taasisi nyengine za Serikali, pamoja na sekta binafsi na taasisi za kijamii, ambazo kwa namna moja ama nyengine, zinachangia katika masuala ya kazi, ajira na uwezeshaji wananchi kiuchumi. Napenda pia kuchukua fursa hii kuzishukuru taasisi hizo kwa mashirikiano waliyotupatia na naziomba tuendeleze mashirikiano haya kwa maslahi ya wananchi wetu na taifa kwa jumla.

Taasisi hizo ni pamoja na Jumuiya ya Waajiri Zanzibar (*ZANEMA*); Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi (*ZATUC*); Jumuiya ya Wawekezaji wa Sekta ya Utalii (*ZATI*), Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*); Benki Kuu ya Tanzania; Benki ya Watu wa Zanzibar; *CRDB*; Jumuiya ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima Zanzibar; na "Tanzaniaa *Private Sector Foundation*". Pia nazishukuru taasisi za elimu na utafiti ikiwemo Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Tanzania; Chuo Kikuu cha Tunguu na *REPOA* kwa kusaidia kujenga uwezo wa watendaji katika nyanja mbali mbali, ikiwemo utafiti na mipango.

Aidha, natoa shukurani kwa taasisi zisizokuwa za Serikali ambazo nazo zimechangia katika juhudi za Serikali za kuwawezesha wananchi wa Zanzibar, kwa lengo la kuwaletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Vile vile, natoa shukrani maalum kwa Ofisi za Mikoa, Wilaya na Shehia kwa

mchango wao katika usimamizi na ufuatiliaji wa masuala ya kazi na programu za ukuzaji ajira na uwezeshaji wananchi katika maeneo yao.

Mhe. Spika, shukrani zangu pia ziende kwa Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi ya Ushauri wa Mambo ya Kazi, Bodi ya Mishahara, Kamati ya Utatu na Kamati ya Usalama na Afya Kazini kwa michango na ushauri wao katika utekelezaji wa majukumu yangu. Namshukuru pia Mwenyekiti na watendaji wa Mahkama ya Kazi kwa mashirikiano yao ya karibu na Kitengo cha Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro ya Kazi, kilicho chini ya Wizara yangu.

Mhe. Spika, Natoa shukrani maalum kwa wafanyabiashara waliochangia kutunisha Mfuko wa Rais kwa lengo la kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Mhe. Spika, vyombo vya habari navyo vimetoa mchango muhimu katika kuhamasisha, kutangaza na kuelimisha jamii juu ya matukio na masuala mbali mbali yaliyohusiana na wizara yangu. Nachukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa viongozi na watendaji wa vyombo hivyo vya habari, zikiwemo televisheni, redio na magazeti, kwa mashirikiano wanayoyatoa kwa wizara yangu.

Mhe. Spika, **s**hughuli zote nilizozieleza, zimetekelezwa kwa ushirikiano wa hali ya juu wa watendaji wakuu na wafanyakazi wote wa wizara yangu. Napenda nitumie nafasi hii kuwashukuru wote kwa juhudi kubwa waliyoonesha katika kutekeleza majukumu yangu pamoja na Taifa.

Namshukuru sana Katibu Mkuu Asha Ali Abdalla, Kamishna, Wakurugenzi, Afisa Mdhamini na wafanyakazi wote wa wizara kwa ushirikiano wanaonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu, pamoja na michango yao iliyowezesha kuandaa hotuba hii. Sina shaka wataendelea kufanya kazi kwa bidii zaidi ili kufanikisha malengo tuliyoyapanga kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014.

Mhe. Spika, pia natumia fursa hii kuwashukuru sana wananchi wote wa Jimbo la Makunduchi kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kufanikisha kazi zangu za uwakilishi wa jimbo hilo. Ni imani yangu wataendelea kunipa ushirikiano, ili kwa pamoja tufanikishe yale tuliyoyapanga katika kuliletea taifa maendeleo pamoja na jimbo letu.

Pia naishukuru sana familia yangu kwa jinsi walivyokuwa wastahamilivu na kuendelea kunisaidia katika shughuli zangu za kila siku.

HITIMISHO

Mhe. Spika, ili Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2013/2014, kwa heshima na taadhima nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wapokee, wajadili, watupe ushauri na maelekezo, na hatimae wapitishe na kuidhinisha matumizi ya jumla ya Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Saba na Themanini na Nane (T.Shs. 2,788,000,000/=) kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Moja Themanini na Tatu, Laki Nane na Elfu Ishirini na Sita (T.Shs. 1,183,826,000/=) ni kwa ajili ya mishahara, mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na posho za wafanyakazi na Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Sita na Nne, Laki Moja na Elfu Sabini na Nne (T.Shs. 1,604,174,000/=) ni kwa matumizi mengineyo.

Vile vile naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Nne Thelathini na Saba (T.Shs 1,437,000,000 /=) kwa kazi za maendeleo, ambapo kati ya hizo, Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Moja Hamsini (T.Shs.1,150,000,000 /=) zitatolewa na Serikali na Shilingi Milioni Mia Mbili Themanini na Saba (T.Shs.287,000,000/=) zitatolewa na wahisani.

Aidha, wizara inategemea kupata Shilingi Milioni Mia Tano Ishirini na Moja, Laki Sita (T. Shs. 521,600,000/=) kutoka *ILO* kupitia Mradi wa *UNDAP*. Pia naomba idhini ya kukusanya mapato ya Shilingi Milioni Mia Nane na Thelathini (T.Shs.830,000,000/=) kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Spika, kabla sijamaliza naomba niwajulishe wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba hotuba hii ya Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika inapatikana katika mitandano na iko tayari hivi sasa kuangaliwa.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri kwa kuwasilisha hotuba hiyo ya makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, kwa muda wa dakika 40 tu, kumbe inawezekana. Lakini sasa nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii na Uwezeshaji na Habari, Mhe. Mlinde Mbarouk Juma, karibu sana.

Waheshimiwa Wajumbe, ukenda kwenye viriri hivi kuna mikogo yake bwana. *(Makofi/Vicheko).*

Mhe. Mwenyekiti, karibu.

VIAMBATANISHO

Kiambatanisho Nambari 1: Mapato Yaliyokusanywa Kuanzia Julai 2012 – Juni 2013

Idara	Kasma		Makadirio (Tshs)	Fedha Zilizokusanywa (Tshs)	Asilimia
Kamisheni ya Kazi	142212	Malipo ya Vibali vya Kazi.	80,000,000	104,651,787	**131%**
	142213	Malipo ya Ukaguzi Sehemu za Kazi/Mikataba.	3,000,000	22,720,000	**758%**
Idara ya Ushirika	142239	Ada ya Uandikishaji Vyama.	6,000,000	7,345,000	**122%**
	142240	Ada ya Ukaguzi wa Vyama na Huduma.	4,000,000	3,070,000	**76%**
Jumla Kuu			**93,000,000**	**137,786,787**	**148%**

Kiambatanisho Nam.2: Fedha Zilizotengwa na Zilizoingizwa za Matumizi ya Kawaida kwa Mwezi wa Julai 2012 Hadi Juni 2013

NAM	IDARA	MAKADIRIO 2012/2013	FEDHA ZILIZOPATIKANA/ MATUMIZI 2012/2013	ASILIMIA
1	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	100,000,000.00	65,757,500.00	65.76%
2	Idara ya Utumishi na Uendeshaji	1,285,000,000.00	1,198,252,389.00	93.30%
3	Idara ya Uendelezaji na Uratibu wa Program za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi	80,000,000.00	72,586,920.00	90.80%
4	Idara ya Ushirika	55,000,000.00	38,847,000.00	70.70%
5	Idara ya Mikopo	248,000,000.00	238,874,840.00	96.32%
6	Kamisheni ya Kazi	110,000,000.00	108,700,000.00	98.90%
7	Idara ya Ajira	65,000,000.00	52,422,500.00	80.70%
8	Idara ya Usalama na Afya Kazini	75,000,000.00	44,053,050.00	58.80%
9	Afisi Kuu Pemba	306,277,000.00	306,277,000.00	100.90%

NAM	IDARA	MAKADIRIO 2012/2013	FEDHA ZILIZOPATIKANA/ MATUMIZI 2012/2013	ASILIMIA
	Jumla	**2,324,277,000.00**	**2,125,771,199.00**	**92.00%**

Kiambatanisho Nam 3a: Idadi ya Wafanyakazi Waliopo Masomoni (Mafunzo ya Muda Mrefu) Ambao Wanagharamiwa na Wizara kwa Mwaka 2012/2013

UNGUJA:					
Aina ya Mafunzo/Fani	**Idara**	**Daraja/Kiwango**	**Jinsia**		**a**
			M'me	**M'ke**	
Mipango	Mipango, Sera na Utafiti	Shahada ya Kwanza	0	1	1
	Kamisheni ya Kazi	Shahada ya Pili	0	1	1
Maendeleo ya Sera	Mipango, Sera na Utafiti	Shahada ya Pili	1	0	1
Manunuzi na Ugavi	Uendeshaji na Utumishi	Shahada ya Kwanza	1	0	1
Sheria	Kamisheni ya Kazi	Shahada ya Pili	0	2	2
Uchumi	Uwezeshaji	Shahada ya Uzamivu	1	0	1

UNGUJA:					
Aina ya Mafunzo/Fani	**Idara**	**Daraja/Kiwango**	**Jinsia**		**a**
			M'me	**M'ke**	
		(PhD)			
Usuluhishi na Upatanishi	Kamisheni ya Kazi	Stashahada ya Uzamili	0	1	1
Ushirika	Ushirika	Shahada ya Kwanza	1	0	1
Uhasibu	Uendeshaji na Utumishi	Stashahada ya Uzamili	2	1	3
Uandishi wa Habari	Uendeshaji na Utumishi	Shahada ya Pili	1	0	1
Katibu Muhtasi	Uendeshaji na Utumishi	Cheti	0	1	1
		Stashahada	0	1	1
Jumla Ndogo			**7**	**8**	**15**

PEMBA:					
Aina ya Mafunzo/Fani	**Idara**	**Daraja/Kiwango**	**Jinsia**		**Jumla**
			M'me	**M'ke**	
Rasilimali Watu	Mikopo	Stashahada	2	0	2
	Kamisheni ya Kazi				
Masoko	Mikopo	Shahada ya Kwanza	1	0	1

UNGUJA:					
Aina ya Mafunzo/Fani	**Idara**	**Daraja/Kiwango**	**Jinsia**		**a**
			M'me	**M'ke**	
Ustawi wa Jamii	Uwezeshaji	Shahada ya Kwanza	1	0	1
Manunuzi	Uendeshaji na Utumishi	Stashahada	1	0	1
Uhasibu	Uendeshaji na Utumishi	Shahada ya Kwanza	1	0	1
Uchumi	Mipango, Sera na Utafiti	Shahada ya Pili	1	0	1
Jumla Ndogo			**7**	**0**	**7**
Jumla Kuu (Unguja na Pemba)			**14**	**8**	**22**

Kiambatanisho Nam 3b: Aina ya Mafunzo ya Muda Mfupi Yaliyotolewa kwa Wafanyakazi wa Wizara kwa Mwaka 2012/2013

UNGUJA:				
	Pahala	**Idara**	**Jinsia**	**Jumla**

Aina ya Mafunzo/Fani			**M'me**	**M'ke**	
Sheria	Unguja, Zanzibar.	Uendeshaji na Utumishi	1	1	2
		Kamisheni ya Kazi	1	0	1
Uhasibu	Tanzania Bara	Uendeshaji na Utumishi	1	0	1
Udereva	Tanzania Bara	Uendeshaji na Utumishi	1	0	1
Katibu Muhtasi	Unguja	Uendeshaji na Utumishi	0	1	1
Afya na Usalama Viwandani	China	Afya na Usalama Kazini	1	1	2
Teknolojia ya Habari	India	Afya na Usalama Kazini	1	0	1
Uwezeshaji Vijijini	China	Ushirika	1	0	1
Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii	China	Uendeshaji na Utumishi	0	1	1
Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi	Korea	Uwezeshaji	0	1	1
Uwezeshaji Kiuchumi na Ujasiriamali	Swaziland	Uwezeshaji	1	0	1
Kupambana na Ajira za Watoto	Italy	Kamisheni ya Kazi	0	1	1

UNGUJA:					
Aina ya Mafunzo/Fani	**Pahala**	**Idara**	**Jinsia**		**Jumla**
			M'me	**M'ke**	
Maendeleo ya Wanawake	Marekani	Uwezeshaji	0	1	1
Jumla Ndogo			**8**	**7**	**15**

PEMBA:					
Aina ya Mafunzo/Fani	**Pahala**	**Idara**	**Jinsia**		**Jumla**
			M'me	**M'ke**	
Kompyuta	Pemba, Zanzibar.	Mikopo	2	0	2
		Kamisheni ya Kazi	1	0	1
		Uwezeshaji	1	0	1
Usalama na Afya Viwandani	China	Afya na Usalama Kazini	1	0	1

Uwezeshaji Vijijini	China	Ushirika	1	0	1
Jumla Ndogo			**6**	**0**	**6**
Jumla Kuu (Unguja na Pemba)			**14**	**7**	**21**

Kiambatanisho Nam 4: Utoaji wa Mikopo Kupitia Mfuko wa Kujitegemea kwa Kipindi cha Mwaka 2012/2013

NO	WILAYA	JINSI		JUMLA	VIKUNDI	FEDHA
		W'KE	W'ME			
1	MJINI	23	13	36	1	26,800,000.00
2	MAGHARIBI	17	21	38	1	28,100.000.00
3	KASKAZINI "A"	11	28	39	0	23,000,000.00

NO	WILAYA	JINSI		JUMLA	VIKUNDI	FEDHA
		W'KE	W'ME			
4	KASKAZINI"B"	7	13	20	0	11,400,000.00
5	KUSINI	12	8	20	0	14,600,000.00
6	KATI	6	3	9	2	8,100,000.00
Jumla Ndogo Unguja						**112,000,000**
7	MKOANI	4	3	7	1	9,600,000.00
8	CHAKE – CHAKE	9	10	19	1	15,400,000.00
9	WETE	6	12	18	5	14,800,000.00
10	MICHEWENI	5	1	6	1	4,200,000.00
Jumla Ndogo Pemba						**44,000,000.00**
Jumla Kuu (Unguja na Pemba)		**100**	**112**	**212**	**12**	**156,000,000.00**

Kiambatanisho Nam 5: Utoaji wa Mikopo Kupitia Mfuko wa JK/AK Kuanzia Julai 2012 Hadi Juni, 2013

Nam.	Wilaya	Fedha Zilizokopwa/Zilizotolewa
1.	Kaskazini ‘A’	5,000,000.00
2.	Kaskazini ‘B’	17,000,000.00
3.	Magharibi	16,000,000.00
4.	Mjini	9,000,000.00
Jumla		**47,000,000.00**

Kiambatanisho Nam. 6: Marejesho ya Fedha za Mikopo Kupitia Mfuko wa Kujitegemea Julai, 2012 – Juni, 2013

NO	WILAYA	JULAI	AGOSTI	SEPT	OCT	NOV	DIS	JAN	FEB	MACHI	APRIL	MEI	JUNI	JUMLA
1	MJIN	3,55	2,81	2,42	2,41	1,98	1,52	2,38	2,26	1,158,	1,086,	3,04	1,386,	**26,04**

NO	WILAYA	JULAI	AGOSTI	SEPT	OCT	NOV	DIS	JAN	FEB	MACHI	APRIL	MEI	JUNI	JUMLA
	I	6,000	7,500	5,500	2,000	7,450	6,000	2,000	6,000	000	000	5,000	000	**7,450**
2	MAGHARIB	2,157,00	1,783,000	1,783,000	1,668,000	2,159,000	1,407,000	1,854,000	2,521,000	1,131,00	1,471,500	3,358,000	210,700	**21,462,700**
3	KASKAZINI “A”	1,703,500	857,000	1,532,500	1,178,000	1,312,500	1,376,000	1,892,500	1,471,000	1,015,000	1,248,000	2,140,500	955,000	**16,681,500**
4	KASKAZINI “B”	382,000	345,500	1,534,500	694,500	1,255,000	343,500	961,000	523,000	391,000	349,000	575,000	495,000	**7,849,000**
5	KUSINI	1,703,000	1,419,500	1,145,500	2,016,000	1,646,500	990,000	1,815,000	1.115.000	920,000	1,100,000	2,203,000	243,000	**16,361,000**
6	KATI	1,054,500	793,000	290,000	485,500	518,000	732	882,500	1,294,000	690,500	694,000	995,000	106,000	**8,315,000**

NO	WILAYA	JULAI	AGOSTI	SEPT	OCT	NOV	DIS	JAN	FEB	MACHI	APRIL	MEI	JUNI	JUMLA
7	MKOANI	438,000	424,000	512,000	544,500	700,000	809,500	1.154,000	514,000	900,000	805,000	481,000	600,000	**7,882,000**
8	CHAKE - CHAKE	1,513,500	1,619,000	1,809,500	1,540,500	1,922,000	1,465,000	1,148,500	1,703,500	1,200,000	1,094,000	1,599,000	1,400,000	**18,014,500**
9	WETE	368,000	155,000	196,000	636,500	885,500	956,500	940,000	954,000	700,000	666,000	747,500	742,500	**7,947,500**
10	MICHEWENI	57,250	537,250	490,000	492,2501,	457,750	390,000	377,500	435,000	500,000	235,000	920,000	691,500	**5,583,500**
	JUMLA	**12,976,750**	**10,750,000**	**11,678,000**	**11,667,750**	**12,843,700**	**9,995,500**	**13,187,500**	**12,796,500**	**8,605,500**	**8,748,500**	**16,064,000**	**6,829,700**	**136,144,650**

Kiambatanisho Nam 7: Utoaji na Urejeshaji wa Mikopo Kupitia Mfuko wa JK/AK Hadi Juni, 2013

UNGUJA:						
Mkoa	**Wilaya**	**Idadi ya walioko pa**	**Fedha zilizokopwa**	**Fedha Zilizolipwa Hadi Mei 2013**	**Deni lililosalia Hadi Mei 2013**	**Fedha Zilizolipwa Kuanzia Julai 2012 hadi Mei 2013**
KASKAZINI	KASKAZINI "A"	58	103,800,000.00	72,855,000.00	30,945,000.00	4,747,271.00
	KASKAZINI "B"	59	166,388,575.35	88,016,218.00	78,372,357.00	3,682,529.00
	Jumla Kaskazini	**117**	**270,188,575.35**	**160,871,218.00**	**109,317,357.00**	**8,429,800.00**
KUSINI	KATI	23	53,700,000.00	30,126,911.00	23,573,089.00	3,375,318.00
	KUSINI	84	139,900,000.00	89,073,302.00	50,126,698.00	7,780,529.00
	Jumla	**107**	**192,900,000.00**	**119,200,213.0**	**73,699,787.00**	**11,155,847.0**

	Kusini			**0**		**0**
MJINI MAGHARIBI	MAGHARIBI	159	392,900,000.00	212,283,569.00	180,486,431.00	12,387,993.00
	MJINI	148	219,176,156.20	111,080,932.00	108,325,324.00	9,486,231.00
	Jumla Mjini Magharibi	**307**	**612,176,256.20**	**323,364,501.00**	**288,811,755.00**	**21,874,224.00**
JUMLA UNGUJA		**531**	**1,075,264,831.55**	**603,435,932.00**	**471,828,899.00**	**41,459,871.00**

PEMBA:						
MKOA	**WILAYA**	**Idadi ya waliokopa**	**Fedha Zilizokopwa**	**Fedha Zilizolipwa Hadi Mei 2013**	**Deni lililosalia**	**Fedha Zilizolipwa Kuanzia Julai 2012 hadi Mei 2013**
	WETE	47	104,270,000.00	40,611,907.00	63,658,093.00	2,322,432.00

KASKAZINI	MICHEWENI	49	84,500.000.00	32,087,278.00	52,412,722.00	0
	Jumla Kaskazini	**96**	**188,770,000.00**	**72,699,185.00**	**116,070,815.00**	**2,322,432.00**
KUSINI	MKOANI	41	62,600,000.00	45,171,142.00	17,428,858.00	2,311,256.00
	CHAKE	83	226,850,000.00	122,920,989.00	103,929,011.00	4,273,089.00
	Jumla Kusini	**124**	**289,450,000.00**	**168,092,131.00**	**121,357,869.00**	**6,584,345.00**
JUMLA PEMBA		**220**	**478,220,000.00**	**291,013,120.00**	**237,428,684.00**	**8,906,777.00**
JUMLA KUBWA UNGUJA NA PEMBA		**751**	**1,553,484,831.55**	**844,227,248.00**	**709,257,583.00**	**50,366,648.00**

Kiambatanisho Nam 8a: Vijana Waliopata Ajira Katika Taasisi za Binafsi Kwa Kipindi cha Julai 2012– Machi, 2013

Nam.	Taasisi Binafsi Zilizoajiri	Jinsia		Jumla
		W'me	W'ke	
1	Reyle Company Ltd	1		1
2	Vera Club Znz Ltd	8	4	12
3	Swahili Beach Resort	17	7	24
4	Ocean Tours	2	1	3
5	Magima Ltd	8	6	14
6	Paradise Beach Bungalows	12	5	17
7	Samaki Lodge	11	9	20
8	Palumbo Reef Hotel	17	8	25
9	The Palms Zanzibar	2	2	4
10	Marie Stope Znz	0	1	1
11	Savana International (Z) Ltd	12	1	13
12	Chumbe Island Coral	2	0	2

Nam.	Taasisi Binafsi Zilizoajiri	Jinsia		Jumla
		W'me	W'ke	
13	Shalom Nursery School	0	1	1
14	Memories Of Zanzibar	0	5	5
15	Willey Academy	3	5	8
16	Lootah Group (Drop Of Zanzibar)	6	0	6
17	Baraza Resort & Spa	9	4	13
18	Breezes Beach Club & Spa	23	2	25
19	Hotel & Property Dvt (Kendwa)	19	9	28
20	Zan Air Ltd	4	1	5
21	Chavda Hotel Ltd	25	19	44
22	Al-Rahma Hospital	4	3	7
23	H.S.E Security Tasks Ltd	10	0	10
24	Prime Time Promotion Co. Ltd	7	5	12
25	Maisha-Essque Zalu Zanzibar	127	44	171

Nam.	Taasisi Binafsi Zilizoajiri	Jinsia		Jumla
		W'me	W'ke	
26	Zanzibar Milling Cor' Ltd	4	0	4
27	Zee Comunications Ltd	1	0	1
28	Gapco Zanzibar Ltd	2	1	3
29	Maruhubi Beach Villas	2	3	5
30	Mina Hospital	0	6	6
31	Zanzibar Ocean View	66	34	100
32	Galaxy Security Serv.Co.Ltd	0	2	2
33	Mombasa Medical Centre	4	3	7
34	Sha High School	21	19	40
35	S & C General Ltd	1	0	1
36	Mapenzi Beach Club	17	16	33
37	Skuli ya High View Int	28	31	59
38	Al-Haramayn International School	2	1	3
39	Island Tours Ltd	1	0	1

Nam.	Taasisi Binafsi Zilizoajiri	Jinsia		Jumla
		W'me	W'ke	
40	Umoja Wa Maaskari Wastaafu	398	2	400
41	Danaos Zanzibar	393	0	393
	Jumla	**1,248**	**281**	**1,529**

Kiambatisho Nam 8b: Waliopata Ajira Nchi za Nje Kuanzia Julai 2012 Hadi Machi 2013

Nchi	Jinsia		Jumla
	W'me	W'ke	
OMAN	14	134	148
DUBAI	38	16	54
QATAR	3	5	8
DJIBOUT	0	5	5

JUMLA	**55**	**160**	**215**

Mhe. Mlinde Mabrouk Juma:(Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari: Mhe. Spika, napenda kusoma hotuba ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, kuhusu Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Spika, awali ya yote, nachukua fursa hii muhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zake zisizo na ukomo kwetu, ikiwa ni pamoja na kutujaalia uhai na afya njema kiasi kwamba tumemudu kukutana hapa leo, ili kujadili mambo mbali mbali yenye manufaa kwetu binafsi na kwa wananchi wetu kwa ujumla. Kwa hakika kama si taufiki na rehma za Mwenyezi Mungu juu yetu basi huenda muda huu tusingekuwa hapa tukipitia Bajeti za Wizara za Serikali.

Mhe. Spika, pili napenda kuendeleza shukrani zangu za dhati kwako binafsi kwa kuniruhusu nitowe mchango kwa niaba ya Kamati ya Mifugo, Utalii,Uwezeshaji na Habari na pia kwa niaba ya wananchi wa

Jimbo la Bumbwini. Aidha, naomba nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa heshima na busara zake za kuiongoza nchi yetu ya Zanzibar, kwa kuheshimu Utawala Bora.

Mhe. Spika, naomba pia nimpongeze Mhe. Waziri na Watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu, kwa kujitahidi kutekeleza malengo na majukumu yao kwa bidii kubwa katika kipindi cha mwaka 2012/2013, lakini pia kwa mashirikiano yao mazuri waliyotupa wakati Kamati ilipokua ikitekeleza kazi zake za kawaida.

Mhe. Spika, nitakuwa mtovu wa fadhila nisipowapongeza wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi kwa imani yao kubwa juu yangu iliyowapelekea kunichagua mimi kuwa ndio mwenyekiti wao na pia kwa ushirikiano wao mkubwa waliouonesha wakati wote ambao Kamati ilipofanya kazi za ufuatiliaji, ikiwa ni pamoja na kuihoji serikali na kutoa maoni yao kwa lengo la kuimarisha utendaji na kukuza uwajibikaji katika Serikali.

Mhe. Spika, naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa kuwataja kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Abdalla Mohammed Ali	-	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Asha Bakar Makame	-	Mjumbe
4.	Mhe. Mussa Ali Hassan	-	Mjumbe

5.	Mhe. Kazija Khamis Kona	-	Mjumbe
6.	Mhe. Amina Iddi Mabrou	-	Mjumbe
7.	Mhe. Asaa Othman Hamad	-	Mjumbe
8.	Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali	-	Mjumbe
9.	Ndg. Maryam Hussein Rajab	-	Katibu
10.	Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi	-	Katibu

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo napenda sasa nitoe maoni ya Kamati ya Kudumu ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hii kwa mwaka wa fedha 2013/2014 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika inajukumu la kusimamia na kuratibu utekelezaji wa sheria za kazi, programu za uendelezaji wa miradi, uwezeshaji wa miradi na uwezeshaji wananchi kiuchumi hususan wananchi wenye kipato cha chini, ili kuwapunguzia makali ya umasikini pamoja na kusimamia maendeleo ya ushirika.

Mhe. Spika, kamati inaipongeza Wizara hii kwa juhudi na jitihada wanazozichukua katika kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kufanikiwa kuwatoa watoto 398 katika ajira mbaya, kutoka katika maeneo tofauti ndani ya Zanzibar na kuwarudisha Skuli ikiwa ni pamoja na kuwapatia vifaa mbali mbali kama viatu, madaftari na Sare za Skuli ili waweze kubakia maskulini kwalengo la kupata elimu ambayo itawasaidia katika maisha yao.

Mhe. Spika, mpango huu umetayarishwa kwa lengo la kuwapa watoto haki yao ya kusoma ili waweze kufanya kazi zenye tija pindi watakapomaliza masomo yao. Kutokana na juhudi hizo Kamati inawashauri wazazi ambao bado wanawaruhusu watoto wao kufanya kazi zisizoeleweka waache mara moja tabia hiyo, kwani hicho ni kitendo kibaya ambacho kinawanyima watoto haki zao za msingi za kuishi katika nchi yao.

Mhe. Spika, hii ni wizara mpya kwahivyo kuna umuhimu kwa kupewa kipaumbele na serikali hasa ukizingatia kazi za Wizara hii ni kutoka nje zaidi na sio kubakia ofisini kwa hivyo vifaa kama Honda,Vespa na magari kwa lengo la kuzidisha ufanisi wa Wizara hii. Mhe. Spika, Kamati imesikitishwa mno na fungu lililotengwa kwa ajili ya ununuzi wa Mashine na Zana kwa Afisi Kuu ya Wizara iliyoko Pemba kwa mwaka huu wa fedha ambalo ni jumla ya shilingi ya Kitanzania 11,650,00/=.

Mhe. Spika, Wizara hii kazi zake nyingi ni za kupeleka huduma kwa wananchi, kwa mnasabaha huu basi usafiri ni kitu cha lazima kwa watendaji wa wizara hii ila cha kushangaza kasma nambari 311203 ambayo imewekewa shilingi 5,000,000 ambayo ndio ya ununuzi wa vyombo vya maringi mawili haiwezi kukidhi mahitaji ya wizara hii, pesa ambazo hata Honda moja ya kazi yenye uwezo wa kufika hadi mabondeni huwezi kulinunua. Hivyo, tunaishauri serikali kuengeza pesa katika fungu hili ili wizara iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi kama ilivyojipangia**.**

Mhe. Spika, tunaishukuru wizara kwa kuendelea kuratibu vyema mfuko wa Zakka, ambao lengo lake ni kuwanasua kiuchumi wananchi hususan wale wenye kipato cha chini, ili kuwapunguzia makali ya

umasikini kwa lengo la kuleta maendeleo katika nchi yetu. Mhe. Spika pamoja na hayo kamati inaishauri wizara kuzidi kutoa elimu kuhusiana na fedha hizo za Zakaa, maana kumejitokeza tatizo kwa baadhi ya wananchi kutorudisha fedha hizo kwa wakati, katika nchi hii kuna wananchi wengi ambao wanazitegemea pesa hizo ili wenzao watakaporudisha halafu wapewe wao.

Mhe. Spika kamati pia inaishauri wizara iwe inatoa pesa hizo kwa vikundi vichache, ili wapate pesa nyingi kuliko kutoa pesa chache kwa vikundi vingi hatimae pesa zinaliwa bila ya kufanyika lolote na pia kamati inashauri Ofisi ya Wakfu isimamie zoezi hili kwavile ni wazoefu na sio Wizara.

Mhe. Spika, kamati inaishauri Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kujenga tabia ya kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi pindi inapotembelea wajasiriamali wake kwani kumejitokeza tatizo la wajasiriamali wingi hususani wale wanaojishughulisha na kazi za ufugaji wa samaki kutofahamu kuwa kuna wataalamu wa kizalendo ambao wanapatikana hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, Kamati pia imeridhishwa na kiwango cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya kutumika katika Idara Uendelezaji na Uratibu wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Mhe. Spika naomba ieleweke kwamba miongoni mwa malengo ya idara hii ni kujenga utamaduni wa ujasiriamali na kuimarisha uwezo wa wajasiriamali hususan vijana katika Wilaya 10 za Zanzibar. Kwa kiwango hicho cha fedha walichoekewa wataweza kutimiza malengo yao kwa ufanisi. Hata hivyo, Kamati inashauri Wizara ya Fedha kujenga tabia ya kuingiza fedha kwa wakati ili Idara iweze kutekeleza vyema shughuli zake kiufanisi na kwa muda iliyojipangia.

Mhe. Spika, Kamati inaipongeza Idara ya Mikopo kwa malengo mazuri waliyojiwekea kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ikiwa pamoja na kuimarisha uwekaji wa kumbukumbu za mikopo. Mheshimiwa Spika kwakweli idara hii ina kazi ngumu sana hasa katika upande wa kutunza kumbukumbu kwa vile vikundi vilivyowahi kuchukua mikopo vingi husambaratika na hatimae pesa hupotea na kutorudi tena serikalini kwa lengo la kuwakopesha wananchi wengine ili na wao wafaidike na huduma hiyo. Kamati inaishauri Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kuwaingizia fedha zao kwa wakati ili Idara iweze kufanya kazi zake kwa umakini zaidi kwani pindi itakapokua inachelewa kuvipitia vikundi vyake na kukusanya marejesho yake ndio upotevu wa pesa utakapojitokeza.

Mhe. Spika, Kamati imebaini kuwepo kwa tatizo la ukosefu wa taarifa za kutosha juu ya fursa za mikopo kwa vikundi mbali mbali vya ushirika. Hayo yamebainika wakati kamati ilipokua ikifanya Kazi zake za ufuatiliaji ikabahatika kukutana na baadhi ya vikundi ambavyo vinaendesha shughuli zake katika mazingira magumu. Hali hii hupelekea vikundi vingi kubakia na umasikini wakati fursa zipo za kuwawezesha kiuchumi.

Mhe. Spika, kamati inaishauri wizara kwa kupitia Idara yake ya Mikopo katika mipango yake ya mwaka 2013/2014 wajikite zaidi katika kutoa taarifa kwa kupitia vyombo vya habari mbali mbali ambavyo vina idadi kubwa ya wasikilizaji na watazamaji ili wananchi waweze kuzitambua fursa zinazopatikana katika wizara hii.

Mhe. Spika, Idara ya Ushirika ilifanya tathmini juu ya uwezekano wa kuanzisha Benki ya Ushirika Zanzibar na kubaini kuwa upo umuhimu wa kuwa na Benki ya Ushirika Zanzibar. Mhe. Spika, ingawa sekta ya ushirika pekee haitoshi kugharamikia mtaji wa uanzishwaji wake huo wa kuanzisha benki, Kamati inaiomba serikali kuhimiza agizo lake la kuwepo kwa ushirikiano baina ya uanzishwaji wa benki ya wanawake na Benki ya Ushirika lifanyiwe kazi haraka iwezekanavyo, ili benki ianze kutoa huduma zake kwa lengo la kutuletea nchi yetu maendeleo kwani wananchi watafaidika kwa uwepo wa beanki hiyo Zanzibar.

Mhe. Spika, Kamati imeridhishwa na kazi inayofanywa na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika ya kuendeleza zoezi la kutoa mafunzo maalum kwa kuwapatia taaluma watendaji wake inayohusiana na utekelezaji wa mikataba ya kimataifa ya Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) ambayo yametolewa kwa lengo la kuwaelimisha watendaji juu ya wajibu wao wa kufanyakazi kwa mujibu wa miongozo ya Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) ambayo Nchi yetu imeridhia.

Mhe. Spika, kutokana na hali mbaya wanayokumbana nayo wajasiriamali walioko katika masoko, Kamati inawashauri wajasiriamali hao waliopo katika vikundi waunde ushirika au *SACCOS* katika maeneo yao ya kazi ili waweze kupata maendeleo zaidi ya kiuchumi kutokana na kufaidika na fursa za watakayopatiwa. Aidha, kupitia vyama hivyo watawezakuyatatua matatizo mbalimbali yanayowakumba kwavile vyama hivyo vitakuwa na nguvu na sauti kutokana na kusajiliwa na kutambuliwa kisheria. Kufanya hayo pia kutachangia kwa kiasi kikubwa kufanikiwa kwa azma muhimu ya serikali hii ya awamu ya saba ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Mhe. Spika, Kamati yetu imetiwa moyo na utekelezaji wa majukumu ya Kamisheni ya Kazi kwa kufanikisha na kuanza kazi kwa kanuni mbili za Sheria ya Ajira nambari 11 ya mwaka 2005 zinazohusu maslahi ya wafanyakazi katika sekta binafsi na Kanuni ya Usajili na utendaji kazi wa Vyama vya Wafanyakazi. Mhe. Spika, adhma ya Serikali yetu tukufu ni kuhakikisha wananchi wake wanapata haki zao za msingi kama inavyoelekeza Katiba ya Zanzibar kifungu cha 21(4) toleo la 2010. Hivyo, kwa kutumia kanuni hizi ambazo zinatoa miongozo juu ya maslahi kwa wafanyakazi katika sekta binafsi nina imani zile kero ambazo kila siku zilikua zikifikishwa hapa Barazani juu ya maslahi ya wafanyakazi wa sekta binafsi pamoja na mambo ya mikataba kwa wafanyakazi kwa sasa zimepata mkombozi.

Mhe. Spika, shukurani za dhati tunazitoa kwa fungu lililotengwa kwa ajili ya Kamisheni ya Kazi. Ni dhahiri kuwa mgao huo umefanywa kutokana na majukumu makubwa inayobeba Kamisheni.

Mhe. Spika, Kamati inaiomba wizara ifanyejitihada za kuwawezesha na kuwapa elimu kina Mama hususan walioko vijijini, kupata miradi watakaweza kuimudu kwani kuna baadhi ya miradi ya kinamama hao inaonekana kuwatesa kama vile mradi wa mwani ambapo faida inayopatikana haiendani na nguvu zinazotumika. Vile vile kutokana na kutokua na elimu ya kuuhifadhi mwani huo hupelekea mwani huo kushuka kiwango kinachohitajika katika soko la kimataifa.

Mhe. Spika, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea Ofisi Kuu Pemba na idara zake inazoziratibu na kujionea hali halisi ya mazingira magumu ya utendaji kazi kwa watumishi wake na hata Afisa Mdhamin. Kamati

inaishauri serikali kuona haja ya kutafutiwa jengo la ofisi pamoja na vitendea kazi ambavyo kamati iliishauri wizara vipatikane kwa haraka ili kuweza kuratibu kazi zao kwa ufanisi zaidi, Pia kamati imeridhika baadhi ya malengo ya ofisi hii iliyojipangia kwa mwaka mpya wa fedha kama vile kuongeza upatikanaji wa fursa za ajira za heshima kwa wananchi, kuimarisha na kuongoza program za uwezeshaji wananchi kiuchumi na kusimamia utekelezaji wa sheria za kazi.

Mhe. Spika, serikali imeweka milango wazi kwa wawekezaji wa ndani na nje kuanzisha miradi yao mbalimbali hapa nchini kwa lengo la kuinua uchumi wa nchi yetu ikiwa ni pamoja na kupatikana kwa fursa mbali mbali za ajira kwa vijana wetu. Kamati imefurahishwa kuona mawakala binafsi wa ajira za nje wamesajiliwa rasmi na wamepewa mikataba maalumu kwa lengo la kuwalinda Wazanzibari. Pia Kamati imeridhika kusikia kua Balozi zetu zilizokua nchi mbali mbali duniani zinahusika katika kupitia mikataba ya kazi kabla haijafika huku Zanzibar ili wananchi wetu wasipate mashaka pindi watakapokuwepo huko ugenini. Mhe. Spika, kimsingi Kamati inaishauri Wizara itafute kwa kina upatikanaji wa kazi nje na sio kuwaachia mawakala pekeyao.

Hitimisho

Mhe. Spika, napenda sasa kuwashukuru wajumbe wote kwa kunisikiliza kwa makini na utulivu, pia napenda kukushukuru kwa mara nyengine tena wewe binafsi kwa kuniruhusu kutoa maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo napenda kutamka kwa niaba ya kamati ya Mifugo, Utalii Uwezeshaji na Habari na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Bumbwini ninaunga mkono hoja ya Mhe. Waziri wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Aidha, nawaomba wajumbe wote wachangie na kuunga mkono makadirio ya bajeti ya wizara hii kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu na malengo waliyojipangia**.**

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, maoni ya kamati yamewasilishwa na hoja imeungwa mkono. Sasa kwa wachangiaji wa jumla naomba nimkaribishe Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi asubuhi ya leo kutia fat-ha hii katika Wizara hii ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Mhe. Spika, mimi niende kwenye ukurasa wa 6 ambapo hapa *heading* kubwa inasema kwamba muhtasari wa mapato na matumizi kwa mwaka huu wa 2012/2013 na halafu vianzio vyenyewe hapa vimeoneshwa vibali vya kazi vya kigeni na ukaguzi wa mikataba ya kazi. Mhe. Spika, naomba nianzie hapa.

Kwa kweli inawezekana Mhe. Spika, kwamba ukaguzi huo unafanyika lakini sio kwa wote naweza kusema hivyo, kwa sababu wapo wengine hawakaguliwi na ndio maana inawapelekea ndugu zetu wafanyakazi

kudhalilishwa kutokana na kuwa hakuna ule utaratibu uliozoeleka kwa mujibu wa sheria zao za wizara ilivyoweka kuweza kukaguliwa. Mhe. Spika, ninao ushahidi tosha.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, maana ya kusema hakukaguliwi mikataba kwa sababu kuna wengine wanafanyiwa misingi au utaratibu. Kwanza tatizo moja linatukuta Mhe. Spika, kwamba Zanzibar tunatumia lugha ya Kiswahili lakini mikataba inakuwa ya Kiingereza, na hili ni kosa moja hivi kwa nini wasifanye *exchange*, maana yake siku hizi kuna mtandao wa kisasa kwamba tafsiri ya Kiingereza basi chini yake inakuja tafsiri ya Kiswahili. Sasa hili lingefanyika kwenye mikataba, basi ingekuwa hakuna tatizo lakini hilo halifanyiki na wala hawasimamii ipasavyo kutokana na kuwa kulinda haki za mfanyakazi ambaye ameajiriwa pamoja na muajiri mwenyewe.

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Spika, niingie kwa hawa wenzetu vituo vya *petrol* na kwanza niseme *Zanzibar Petroleum* hawana mikataba kabisa. Sasa mimi leo nikisikia kwamba kuna sentensi inasema ukaguzi wa mikataba ya kazi na mimi hapa ndipo ninapopata *pressure*, kwa sababu Mhe. Spika ni dhahiri hasa inaoneshwa kuwa wengine wanakaguliwa na wengine hawakaguliwi.

Kwa mfano, *Zanzibar Petroleum* kuna watu hawana mikataba, wengine wanafukuzwa kiholela bila ya kuwa na *security* yoyote ambayo inawalinda. Kwa kweli hapa mimi ndipo ninapoanza kusikitika na hii ni ardhi yetu na tumewaita watu waje kuwekeza, lakini kwa misingi ya sheria za nchi lakini leo tunawaachia wanafanya wanavyotaka wao wenyewe tu na wala haiwezekani hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika hii *Zanzibar Petroleum* kuna mtu ametoka nje ya nchi anawasumbua ndugu zetu wa Kizanzibari anawadhalilisha na wizara husika ipo na inatizama tu, hivi kesi ngapi ziko kule na hakuna hata moja ambayo imefikia mwisho. Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho, basi aje anisaidie aniambie kwamba huyu anayo kesi, mtu anatoka Kenya anakuja kutuonea huku na tunasema kuwa vyombo vya sheria vipo lakini havifanyi kazi yake.

Mhe. Spika, mshahara wa Mhe. Waziri nitamnyang'anya hapa na sitounga mkono na nitaondoa mshahara wake, kwa sababu hichi kitu si mchezo na tumeshasema sana lakini hakina ufuatiliaji. Vile vile kwenye ukurasa wa 14 kuna *program* ya ajira ya vijana. Mhe. Spika, kila siku tuna *program* tu lakini utekelezaji wake hauonekani na siku hizi imekuwa *slogan* ya kuzungumza kwamba *program* yenyewe utendaji wake kwa vijana haiwezekani na wala haitekelezeki. *(Makofi).*

Jambo hili ni la kusikitisha sana hili. Kwa mfano, humu tumeoneshwa kwamba kuna mifugo, uvuvi pamoja na mambo mengine. Leo ukenda huko mitaani au ukisema upate asilimia la lile lengo lenyewe la wavuvi au wafugaji ni wangapi katika ajira hizi za vijana, basi hupati *total amount* ambayo *exactly* kabisa ambayo inayoonesha asilimia kwamba kweli tumefika malengo si kweli Mhe. Spika. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, vijana hao ni wangapi ambao wamefaidika na hivi sasa wangapi wao kwenye *process* ya kufaidika ili tuweze kuona hali halisi ilivyo. *(Makofi).*

Mhe. Spika, nikiingia kwenye ukurasa wa 16 na leo naomba sana dakika zangu 30 nitambe, kwa sababu hii ni wizara kubwa sana hii ambayo inahusu haki za wananchi wetu. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Spika,

tena kwa unyenyekevu, basi uniachie dakika zangu 30 kwa ajili ya kuweka sawa. Mhe. Spika, najua ombi langu limepita kwa maana umetikisha kichwa na Mwenyezi Mungu akubariki kwa Ramadhani hii ya leo. *(Makofi).*

Mhe. Spika, hapa kuna kinukta na wala hakikuandikwa ni kifungu gani ukurasa wa 16, naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Ukurasa wa 16 unaeleza hivi:-

> "Kupitia Wizara inayoshughulikia masuala ya Mifugo na Uvuvi, jumla ya vijana 80 (40 kutoka Pemba na 40 Unguja) wamepatiwa mafunzo …"

Je, mafunzo haya zimetolewa fedha na kweli hawa walengwa imeingia ndani ya nyoyo zao kweli na wamesimamiwa, wamepewa *income* zenyewe za kutekeleza wajibu. Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri aje anifahamishe kuhusiana na suala hili ili niweze kufahamu.

Mhe. Spika, ukurasa wa 18 wizara pia inasema tayari imewasiliana na taasisi mbali mbali za sekta za umma binafsi, baadhi yao ikiwemo Kiwanda cha Sukari hii! Mhe. Spika, Kiwanda cha Sukari kiko wapi? maiti. Kwa kweli hapa Mhe. Waziri ametupiga changa la macho kwa sababu Kiwanda cha Sukari kimekufa na mpaka leo hii bado kipo kipo tu. Kwa hivyo, hili namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha ambaye ni mpenda maendeleo ya nchi, basi hawa watu sasa ni *disqualify* wamefeli kabisa katika kuleta maendeleo

katika nchi, yaani kuleta ajira pamoja na kupata mapato ambayo yatakayoiwezesha nchi yetu kupiga hatua ya maendeleo nchi yetu. Kutokana na hali hiyo, Mhe. Spika hawa waondolewe mara moja na wala hakuna mzaha hivi sasa isipokuwa tunaleta viwanja ambavyo vitakavyotoa ajira kwa vijana wetu pamoja na serikali kupata kodi ya mapati. Mhe. Spika, nina wasi wasi sijui kama wanakulipa kodi ya mapato Mhe. Waziri.

Sasa ninamuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba hawa watu awaondoe, kwa sababu wanatuwekea mzigo tu na kila siku hakuna kinachoendelea na vijana hawapati ajira wanahangaika tu. Kwa hivyo, ninamuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha na ninamuamini sana, na yeye ni miongoni mwa wajumbe wa kamati ambayo inayotaka kuleta maendeleo katika nchi hii.

Mhe. Spika, sasa naomba niingie kwenye fungu la Idara ya Mipango ya Sera. Kwa kweli kwenye fungu hili nasema tena kwamba hapa ndipo nitakapoanza kulizuia katika utekelezaji wa kazi zake, isipokuwa Mhe. Waziri anipe sababu na hasa sababu zenyewe zinazotokana na Idara yake ya Kamisheni ya Kazi na hapa mimi ndipo ninapolia sana. Mhe. Spika, maafisa wake Mhe. Waziri bado hawajakuwa kwenye *street* ya kuweza kufanyakazi kwa mujibu wa utaratibu, ninakataa sana. Hata hivyo, kama tunakumbuka vizuri nilizungumza kuhusu suala la *Zan Tour*. Mhe. Waziri nadhani hakunifahamu kwa sababu nikisema kitu yaumu shaka, ina maana sina uhakika wa jambo.

Lakini wale wenye *investors* ndio wanaosema kwamba jamani eeh! nyinyi nendeni kokote na Waziri, Kamishna pamoja na watendaji wenyewe pia wamewaweka kwenye mkono na wanasema hivyo, kwa

sababu tayari ameshajiona kuwa kweli hakuna sababu ya kuzuiliwa na kwa kuwa sheria tunaziona, lakini hazitekelezi na lazima Mhe. Spika, watasema hivyo na ukubali tu.

Mhe. Spika, ninao mfano ambao ni mzuri sana, hivi karibuni walikuja vijana kama 20 walikuwa na matatizo ya hoteli ambapo wamefukuzwa na kwa bahati nzuri mimi nikatoka nao na nikenda mpaka Mkoa wa Kaskazini na nipofika kule nikamtafuta ofisa wake Mhe. Waziri na walikuwa hawapo ofisini na hili nakwambia ukweli na kama wapo wenyewe waseme kama kweli au uongo. Baadae pale nikapewa *number* nikawapigia na kwa bahati mbaya ikawa wakati ule hawakuweza kupokea.

Mimi nikatoka nikenda Idara ya Uhamiaji tena hao niseme ninawapongeza tena nawapa nafasi ya pekee kuwashukuru sana Mhe. Spika, kwa kweli niseme wako *active*, lakini kila mtu ana sheria zake. Kwa hivyo, kutokana na ile hali halisi basi wakaniambia Mheshimiwa watafute hawa na sisi tutawatafuta na tukiwapata tu, basi tutashirikiana na wewe katika kulitatua tatizo hili.

Mhe. Spika, tumekwenda *as a teamwork* wametoka kweli na wala sisemi uongo lakini walipofika kule wameona ile zahama na yule jamaa alikuwa ameshazoea kuwapa watu rambaramba, yaani anawapa *buffer*, lakini *buffer* Mhe. Spika itatuweka pabaya sana kuwadhalilisha wananchi wetu. Kwa kweli afisi anapewa *buffer* basi anaona tayari ameshafika anaacha kumtetea yule mzalendo ambaye anayedhalilishwa pale.

Jambo jengine Mhe. Spika, hebu twendeni na sheria, kwa sababu mtu anafika na sheria ni miaka 6 lakini mtu anafika miaka 8 bado hupo hapa na anaendelea kutudhalilisha tu. Kwa mfano, *United Petroleum* yupo

yule Mhindi ambaye ameshaondolewa nyuma huko na baadaye amerejeshwa tena pale pale na tutizame hivi sasa anavyowadhalilisha wananchi.

Mhe. Spika, tunawaweka tu jamani, nadhani ni vyema tumsaidie Mhe. Rais amekuchagueni nyinyi mawaziri kwa lengo la kumsaidia. Sasa Mhe. Rais anaongoza wananchi wakiwemo wanyonge, matajiri, mafukara na kadhalika. Kwa hivyo, Waheshimiwa Mawaziri wasiongeze matatizo haya, isipokuwa jambo na busara ni kumsaidia Mhe. Rais kwa kutekeleza zile sera ambazo Mhe. Rais mwenyewe anataka kuzitekeleza. Lakini inasikitisha sana kwamba mtu hivi sasa ana miaka 8 yupo Zanzibar na hawa watoto wetu tunaowasomesha imekuwa hawafai Mhe. Spika. Kwa kweli uwezo tunao, kwani tunao watu wahasibu wazuri wenye *diploma* na leo utakuta kazi za kukosha vyombo analetwa mtu kutoka nchi za nje *why*? Hivi ni sababu gani zinatufanya tuwe namna hiyo, inasikitisha sana. *(Makofi).*

Kutokana na hali hiyo, mimi naomba sana sasa tuwe *strict* kweli, pia ninasema sana na Mhe. Rais atusikie kwamba waziri ambaye hawajibiki basi amuondoe na atafute watu wengine ambao wanaoweza kufanyakazi na wala si mchezo Mhe. Spika, kwa sababu ni kazi ambayo ya kumtetea mwananchi, tena ni dhima hata kwa Mwenyezi Mungu na mwezi huu wa Ramadhani kwa kweli ni kazi kubwa.

Kwa mfano, leo utakuta *PO* anatoka Kenya wakati Mzanzibari amesoma, tunacho Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar. Vile vile Wazanzibari tumeambiwa au tunadharauliwa kwamba hatuwezi kazi, nani amekwambieni kwamba hatuwezi kazi? Mhe. Spika, nani amesema kwamba Wazanzibari hatuwezi kazi

isipokuwa munatuonea tu na wala hamtaki kutupa kazi kwa sababu watu wanapata maslahi yao, lakini Wazanzibari wote wanaweza kazi tunaonewa na tuseme ukweli Mhe. Spika. *(Makofi).*

Mhe. Spika, hivi Mzanzibari gani ambaye hawezi kufanya kazi au ambaye hajasoma, tumesoma lakini leo nenda kwenye mahoteli, Wazanzibari ni watatu na sera hii tumeleta wenyewe kwa ajili ya kujinufaisha katika ardhi yetu wenyewe, ili kupata uchumi. Mhe. Spika, inasikitisha sana kwa sababu tunadhalilishwa na watu kutoka nje. *(Makofi)*
Mhe. Spika, naomba siku moja twende tukafanye *visit site* kule kwa ajili ya kwenda kukagua, *wallahi* ni aibu umwambie wewe lete hicho cheti chako na halafu mtafute Mzanzibari anacho cheti kuliko kule na ukiuliza umepata vipi kazi haijulikani. Kwa kweli kitengo kinachohusika kinazembea na hii Mhe. Spika, tuseme ukweli ulivyo na ndio maana tunakuwa wakali Waheshimiwa. *(Makofi).*

Kwa mfano, wananchi wa Kiwengwa wamefunga mikataba na wawekezaji ili wapate kufunga njia wawekezaji wafanikiwe pamoja na wale wananchi wa Kiwengwa. Lakini jambo la kusikitisha Mhe. Spika, hivi sasa ni wakati wa kuajiri basi wamefukuzwa, yaani wameondoshwa na tunakwenda wapi Mhe. Spika? Sasa wafungue mipaka tuvamie, kwa sababu ni haki yao ile kwa mujibu wa utaratibu kwani wamekubaliana na mikataba ipo. Kwa maana hiyo, wizara au Kamisheni husika haishughuliki na wao wamekaa kitako tu.

Suala hili kwa kweli linasikitisha na linaumiza moyo kusema ukweli kuwa wale wamekubaliana kwa mujibu wa utaratibu na wamefunga mikataba na leo wanafukuzwa kazi wananchi hawapati kwenye hii

hoteli ya juzi inayoitwa *DOING* au KIWI, hawapewi kazi wanafukuzwa, faida yetu nini Mhe. Spika? Kwa hivyo, kutangaza sera imekuwa balaa kwetu, yaani inageuka inakuwa utumwa. Mhe. Spika, suala hili linauma sana na linasikitisha sana. Mhe. Spika, naomba sana Mhe. Waziri ajipange vizuri maafisa wake sio na wala hawataki kufanyakazi kwamba mimi nina imani na yule mtu ambaye amedhalilishwa. *(Makofi).*

Mhe. Spika, nimshukuru sana Mhe. Waziri wanacho kitengo sawa na mahakama, basi hata kile hawapewi fursa na kile kitengo ni kizuri sana na yule bosi wa pale nampa hongera sana na Mwenyezi Mungu amjaalie ampe imani hiyo hiyo *wallahi* ndiye muokozi aliyebakia katika wizara yako Mhe. Waziri ni yule tu na wala hakuna mtu mwengine, na kesi tatu ameziendesha vizuri na amewatetemesha watu na wamelipwa haki zao kwa mujibu wa taratibu. Kwa hivyo, kitengo kile namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba akiangalie mafao yao wapewe kwa sababu ni sawa kama mahakimu wengine na kuna maposho mengine wanakosa kitengo kile. Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri, Kitengo cha Ushauri wa Kisheria kikisimamiwa na mkuu wake kisaidiwe kwa nguvu zote.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, unazo dakika 5 kumaliza hotuba yako.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, kuhusu suala la *SACCOs* sina tatizo nalo na ninamuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako kwamba azidi kulifanyia kazi kwa ajili ya kulitafutia fedha kwa nguvu zote, ili *SACCOs* zetu ziweze kuendelea zaidi na zipate sheria pamoja elimu ya utawala kwa ajili ya kuweza kuendeleza vizuri zaidi.

Vile vile niseme Mhe. Spika, kwamba Mhe. Waziri aliahidi katika bajeti iliyopita kuwa Benki ya Wanawake itakuwa tayari na alisema na bilioni za fedha anazo na bado nyengine kidogo ambapo zikikamilika basi benki hiyo itakuwa tayari. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho basi anieleze amefikia wapi na kama fedha hizo hana aseme na tutafute na Mhe. Waziri wa Fedha anaye ubavuni, tuhangaike haraka sana, kwani Benki ya Wanawake ni uokozi ili iweze kufanikisha. *(Makofi).*

Mhe. Spika, kwa haraka haraka nimalizie hizo dakika zangu 5 nisipigiwe kengele. Hivi sasa tunao watembezaji wa utalii na wengi ni wageni wa nchi yetu tufanyeni *research* jamani. Kwa kweli vijana wetu hivi sasa wanajisomesha lugha na mtu mmoja anazo lugha si chini ya tatu, lakini hatuwapi *priority* sijui kwa nini. Sasa tumeamka wenyewe na ninaomba sana Mhe. Spika, watembezaji ambao ni wa kigeni hatutaki hivi sasa, isipokuwa tupewe wenyewe Wazanzibari tutembeze na tumechoka kupandiwa ngazi sisi migongo yetu na watu wakatajirika wakaondoka na fedha na sisi wakatuacha maskini na hiyo ni mwisho Mhe. Spika.

Jambo jengine Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri aje anipe hesabu kwamba mahoteli yote ya Zanzibar, wageni wangapi wanaofanyakazi na wazalendo wangapi? Kwa hivyo, akinipa takwimu hiyo pengine nitaridhika au sitoridhika nayo. *(Makofi).*

Mhe. Spika, Mahakama ya Kazi bado hatujaitendea haki kusema kweli, kwa sababu *obvious* iko hali ambayo si nzuri kabisa Mahakama ya Kazi. Kwa mfano, jengo mpaka leo mimi sijui ilivyokaa na inanisikitisha sana, yaani sijui kama sikuambiwa hii hapa tena nipelekwe.

Mhe. Spika, naomba sana kwamba Mahakama ya Kazi na wao watendewe haki zao pamoja na maposho yao kwa mujibu wa sheria tuwape na iheshimiwe, jamii hii mahakama, mawaziri wengine wanakuwa hawaheshimu hizi mahakama hizi kwa sababu mtu tayari ameshakubalika arudishe kazini apewe mafao yake, lakini mtu anapigwa danedane mpaka leo Mhe. Spika, na nimeshasema wengi tu wamo wanahangaishwa.
Kwa mfano, yule ambaye alikuwa Wizara ya Afya mpaka leo anahangaishwa maskini ya Mungu, hivi tunakwenda wapi Mhe. Spika? Na wewe ndio unayesababisha yule mtu atiwe hatiani, yaani wizara inamsababisha atiwe hatiani, lakini mahakama inamtoa hatiani. Sasa wewe uliyesababisha wajibu unatakiwa umlipe fedha zake lakini huwezi na uliona utamu wakati wa kumuwekea kesi tu na kumlipa unashindwa.

Mhe. Spika, naomba nimalizie la mwisho kuhusu biashara za nje.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, umalizie kwa dakika 2.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, sawa. Siku moja Mhe. Waziri wakati nilipotoa hoja yangu kumwambia aah! Mhe. Waziri kuna Kamishna wako anahusika na jambo fulani, naomba unipe

uhakika wa hilo jambo. Lakini Mhe. Waziri alikwenda nje ya katika kunijibu jambo jengine, ina maana ile *hansard* bado haijakaa sawa. Mhe. Spika, inavyosemekana ni kweli Kamishna yule amekula fedha au hajala, kwa sababu hajaweka sawa na akarukia kuna kampuni mmoja ambayo alinitaja na mimi.

Mhe. Spika, namalizie kwamba kampuni hiyo ni kwamba wenzetu kule nje wana muda wa kuajiri watu na ile kampuni ilipata ajira 300 za Wazanzibari kwenda kule Muscat na yule mama alikuwa tayari ameshapata vibali vyote na kupitia Mhe. Waziri mwenyewe wa viwanda amempa baraka zote.

Lakini tunayo tabia hapa sisi Mhe. Spika, kuzungusha na hata hawa *investors* wengine tunawazungusha wakati mtu ameshakopa fedha zake kule nje na *interest* inakuwa kubwa. Sasa na huyu *delay time* yetu imefika pahala kule wameshachukuliwa watu wengi na hatimaye mwanamke ndio mwanamke kama unavyojua na kosa lake kubwa ni kwamba alichukua fedha mwanzo akazila zile fedha, na hilo nakubaliana nalo na wala halina tatizo kwa sababu amefanya kitendo hicho na mimi panapo uchafu mimi siwezi kukaa nao kooni ni nauseme tu. *(Makofi).*

Kwa kweli *process* ilikuwa tayari imeshakuwa kwenye *online*, lakini sisi wenyewe ndio tuliomsababisha na tukubali na hilo. Sasa sijui Mhe. Waziri atanijibu nini Mhe. Spika, kwa sababu nina ushahidi tosha na vyengine nimevitia humu kwenye mkoba wangu sijavitoa ili kuonesha dhahiri masuala yaliyopita.

Mhe. Spika, naheshimu sana muda wako na hata sijaingia kwenye *hansard* za Mhe. Waziri kuhusu maelekezo yake aliyoyasema hapo nyuma. Kwa hivyo, nasubiri wakati wa kupitisha vifungu nitayasema kwa ushahidi tosha kwa sababu yamo humu ambayo ni matamshi yake mwenyewe.

Mhe. Spika, Wazanzibari tunaonewa sana katika ajira. Kwa maana hiyo, maafisa wajipange kwa kuwaokoa Wazanzibari ili waweze kupata haki zao katika ardhi ya nchi yao. Mhe. Spika, ahsante sana na wala siungi mkono. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, nashukuru. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Kazija Khamis Kona.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia na niliomba kuchangia kwa siku ya Jumatatu na bado ninajiandaa, lakini hata hivyo nitachangia hivyo hivyo.

Mhe. Spika, kwanza nikupongeze kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Vile vile nimpongeze Mhe. Waziri kwa jitihada zake pamoja na watendaji wake, pia watendaji wake niwape pole sana, kwa sababu kazi wanazozifanya ni katika mazingira magumu mno. Lakini niiombe serikali kwa kuwa watendaji hawa kazi zao sana ni za kutoka nje kwenda *field*, basi niiombe serikali kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba wizara hii iwapatie vyombo vya usafiri kama vile pikipiki ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Vile vile nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho aje anisaidie ufafanuzi kiambatanisho Nam. 100 kutokana na makusanyo aliyoyakusanya, yaani yamefurutu ada. Sasa hapa nataka kujua Mhe. Spika, kwamba wizara je, imepata vyanzo vyengine au laa na kama imepata vyanzo vyengine vya kukusanya mapato hayo basi naomba aje anisaidie vyanzo hivyo.

Nikiendelea na mchango wangu kwenye ukurasa 28 kuhusu ajira za watoto Mhe. Spika, naomba kunukuu kidogo.

Ukurasa wa 28 kitabu cha hotuba ya Mhe. Waziri unaeleza hivi:-

> "Mradi wa Kupambana na Ajira za Watoto, mradi huu unagharamiwa na Jumuia ya Ulaya kupitia *Save The Children*. Utekelezaji wake unahusisha wizara zinazoshughulikia masuala ya kazi, elimu, ustawi wa jamii, pamoja na taasisi za kiraia (TAMWA, COWPZ, PIRO na KUHAWA). Lengo la mradi ni kuwanusuru watoto 5000 …"

Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri kweli katika wilaya zetu hizi kuna watoto 5000 tu wanaojihusisha na mazingira magumu na wizara yake imefanya utafiti gani hata ikagundua kwamba kuna watoto 5000 wenye mazingira magumu. Hata hivyo, wizara imegundua kwamba kuna watoto wanaojihusisha na ajira, ambao wako kwenye mazingira magumu na kati ya hao ni watoto 398 wamo katika ajira za watoto walioteuliwa katika ajira hizo kurejeshwa skuli pamoja na kupatiwa vifaa.

Mhe. Spika, hapa kidogo nimuulize kwamba watoto hawa amewagundua wako katika mazingira magumu mno na halafu wizara yake imewasaidia vifaa pamoja na sare za skuli. Lakini nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba hii bado haijatosheleza kwamba kuwapatia vifaa na sare za skuli. Kwa kweli jambo la msingi ni kuwa karibu nao, kwa ajili ya kubadilishana mazao kutokana na maisha yao ambayo ni magumu.

Sambamba na hilo naomba kutoa ushauri kwa kuwa kuna huu Mfuko wa Zakka usilengwe kupelekwa kwenye vikundi, kwa sababu baadhi ya watu wenye vikundi uwezo wanao lakini wamejiunga kwenye vile vikundi kwa ajili ya kuendeleza maisha yao. Sasa wakati huu ni Mfuko wa Zakka na sheria yake ni kwamba wapewe watu ni maskini pamoja na mafukara. Kwa hivyo, wakati wizara yake tayari imeshafanya utafiti na imegundua kwamba kuna watoto wenye mazingira magumu mno. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kwamba fedha hizi zielekee huko kwenye watoto wenye mazingira magumu na wala sio kupelekwa kwenye vikundi tunakosa na hawa wenye fedha hizi inakuwa hawapati faida ipasavyo, kwa sababu sisi tunapozitoa hizo fedha tunazilenga kwa madhumuni maalum lakini zinapelekwa kwengine. *(Makofi).*

Sasa Mhe. Spika, fedha hizi zote zipelekwe kwa wananchi wenye mazingira magumu au wenye kipato cha chini mno na sio zipelekwe kwenye vikundi. Vile vile natoa ushauri Mhe. Spika, kwa kuwa kuna Mfuko wa Rais ambao bado haujazinduliwa na Mhe. Waziri alituambia kwamba mfuko huu utazinduliwa na sisi atatushirikisha, basi naomba wakati wa kuzinduliwa mfuko huu na sisi atushirikishe ipasavyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kuwa kuna mfuko huu wa Rais na nimesikia fedha nyingi, hivyo na hizi fedha za Mfuko wa Rais zielekee huko kwenye vikundi na fedha zetu za zakka ziende kwa wananchi wetu wenye mazingira magumu, ili na wao waone kwamba serikali yao inawajali na inawapatia manufaa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kuwa sijajiandaa vizuri naomba niunge mkono hoja, ahsante sana. *(Vicheko/Makofi).*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana na umeunga mkono hoja. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Marina Joel Thomas

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuchangia hotuba hii ya bajeti kwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Pia napenda kumpongeza Mhe. Waziri kwa kuandaa hotuba hii ambayo nzuri pamoja na watendaji wake.

Mimi nitakwenda katika Idara ya Mikopo katika kitabu chake cha ripoti ya hotuba hii ukurasa wa 54 imeelezwa kwamba mikopo 193 imetolewa kwa Zanzibar nzima, 142 kwa Unguja na 51 kwa Pemba. Nikifungua katika hii jadweli huku kiambatanisho Nam. 7 ambacho kinaeleza utoaji na urejeshaji wa mikopo kupitia mfuko wa JK na AK imeelezwa kwa Unguja jumla ya waliokopa ni 531 na Pemba 751.

Katika maelezo ya kiambatanisho hiki fedha zilizokopwa kwa Unguja ni 1,075,264,831.55. Fedha zilizolipwa hadi Mei 2013, 603,435,932.00 na mbili, deni lililosalia hadi Mei 2013 ni 471,828,899.00, fedha zilizolipwa kuanzia Julai 2012 - Mei 2013 ni 41,459,871.00.

Hapa nilikuwa naomba ufafanuzi Mhe. Waziri katika kiambatanisho hicho Nam. 7 ambacho kinasema fedha zililipwa hadi Mei 2013 ni milioni mia sita na tatu. Lakini kuna *column* nyengine inasema fedha zilizolipwa kuanzia Julai 2012 - Mei 2013. Hapa ulipoeleza fedha zilizolipwa hadi Mei 2013 zinaonesha ni nyingi zaidi ambazo ni milioni mia sita na tatu mia nne thalathini na tano mia tisa thalathini na mbili wakati fedha zilizolipwa kuanzia Julai 2012, hadi Mei 2013 ni bilioni 41. Hapa nataka nipate maelezo fedha hizo zilizolipwa hadi Mei 2013 tangu lini. Kwa sababu umesema zimelipwa hadi Mei 2013 ni kiasi hichi, mia sita na tatu, mia nne na thalathini na mia tisa thalathini na mbili. Wakati huku umesema fedha zilizolipwa kuanzia Julai 2012 hadi 2013 Mei ni milioni arubaini moja, mia nne hamsini na tisa, mia nane sabini na moja, sasa nilikuwa naomba ufafanuzi.

Nitakwenda kwenye Mfuko wa Kujitegemea tumesema katika Wilaya ya Mjini katika kiambatanisho hicho, watu waliokopeshwa ni 36 na kikundi kimoja ndio kilichokopeshwa. Jumla ya milioni ishirini na sita mia nane ndio wamepatiwa kikundi hicho na watu hao thalathini na sita. Katika Wilaya ya Magharibi, watu waliokopeshwa thalathini na nane kwa kikundi kimoja na jumla ya milioni ishirini na nane mia moja ndio walizokopeshwa. Kaskazini 'A' 39 waliokopeshwa, lakini katika *column* ya kikundi kuna 0, lakini fedha walizopata ni milioni 23, Kaskazini 'B' halikadhalika.

Swali langu hapa nataka ufafanuzi Mhe. Wiziri. Wilaya zote hizo katika *column* zimeonesha zimepata fedha kwa watu lakini katika kupitia vikundi lakini Wilaya tatu za Kaskazini A, B na Wilaya ya Kusini katika *column* ya vikundi kuna 0. Hapa naomba nipate maelezo. Nasema hivi kwa sababu tukitoa mikopo kupitia vikundi inasaidia hata ile kufuatilia marejesho yake. Katika hapa inaonesha *column* ya vikundi kuna 0. Ina maana wamekopeshwa mtu mmoja mmoja sasa ufuatiliaji utakuaje kwa sababu ukifuatilia kwa vikundi inakuwa ni rahisi zaidi kuliko mtu moja moja.

Hata hivyo, kama wametoa hivyo ni mikakati gani walioweka kwa hawa ambao hawapo katika vikundi. Mikakati gani ambayo wameiweka ili kurahisisha fedha hizo zirudishwe kwa waliokopeshwa na hatimae ziwasaidie wale wote ambao wanahitaji mikopo hiyo.

Nitakwenda kwenye suala la ajira, kuna kiambatanisho ambacho kimeeleza waliopata ajira nje ya nchi kuanzia Julai, 2012 hadi Machi 2013. Takwimu inaonesha kuna nchi nne ambazo vijana wetu wamepatiwa ajira. Nchi zenyewe ni Oman, Dubai, Qatar na Djiboutia ambapo jumla ya Wazanzibari 215 wamepatiwa ajira. Hapa nilikuwa naomba ufafanuzi hawa ni Wazanzibari wetu ni wananchi wetu, kwa hivyo suala la maslahi, malalamiko, haki zao, fursa zao, pamoja na mafao yao, nyinyi kama Wizara mmejipanga vipi kuwafuatilia watu hawa. Watu hawa wapo nje ya nchi na hatujui mazingira gani ambayo wanafanyia kazi huko. Nilikuwa naomba maelezo jinsi ya ufuatiliaji juu ya hayo.

Nitakuja katika suala la ajira kwa taasisi binafsi. Hapa imeeleza kuna taasisi nyingi za binafsi zimeajiri vijana wetu ambapo taasisi kama 41 na vijana kama 1,529 wameajiriwa katika taasisi mbali mbali, kwa

mfano *Vera club, Swahili Beach Resort, Paradise Beach Bungalows*, *Marie Stope*, *Baraza Resort* na kadhalika.

Mhe. Waziri kama nitakosea nitaomba ufafanuzi. Hawa wanakatwa zile *ZSSF* na baadhi ya wafanyakazi au wananchi wengine wanakuwa hawafiki ule muda, pengine kafanya kazi kwenye hoteli miaka miwili, mwaka mmoja au miaka mitatu anafukuzwa kazi. Suala la haki zao hizi za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*) unalishughulikia vipi ili kuhakikisha wananchi wetu wanapata haki zao. *ZSSF* ina taratibu zake wa kulipa mafao yake. Kwa hivyo na hawa pengine hawatofika muda ambao *ZSSF* wamejiwekea. Naomba maelezo kwa sababu ni vijana wengi hawafiki ule muda, pengine anaajiriwa muda mfupi tu kishafukuzwa kazi, haki zao wanazipataje hawa?

Suala la mikataba ya kazi. Mhe. Waziri katika taasisi binafsi vijana wetu wanaajiriwa lakini katika hizi taasisi kila mmoja pengine ana taratibu zake za mikataba. Mhe. Waziri hapa nilikuwa nina ushauri, tukiwa na mikataba iliyokuwa mizuri hata lile suala la kuachishwa kazi wananchi wetu au vijana wetu linakuwa halitokei mara kwa mara. Nilikuwa nashauri kwamba ile mikataba iwe inafuatiliwa nijue kwamba inawasaidia wananchi wetu au vipi.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naunga mkono.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kuweza kuchangia mawili matatu juu ya bajeti hii ambayo imewasilishwa hapa na Mhe. Waziri. Mimi nianze kwa

kumshukuru Mhe. Waziri pamoja na timu yake ya watendaji kwa namna ambavyo wameweza kujipanga vyema na hatimae kuweza kuwasilisha bajeti yao ikiwa na muelekeo mzuri kabisa wa kuweza kusaidia maendeleo ndani ya nchi yetu.

Mhe. Spika, katika ukurasa 30 kifungu cha 27 ambapo hapa kuna maelekezo kwanza mafunzo haya yatasaidia katika kuandaa bajeti kwa mpango kazi wa wizara kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ambapo jumla ya programu nne zinazohusu shughuli kuu za wizara zimeandaliwa.

Mhe. Spika, mimi ningeliomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie ufafanuzi juu ya namna ya maandalizi ambayo yameandaliwa juu ya utengenezaji na uendeshaji wa ajira programu ya kwanza. Pia usimamizi na utekelezaji wa sheria za kazi na manufaa kwa wale walengwa ambao tunatarajia watakuwa wamepata. Pamoja na uwezeshaji wa wananchi kiuchumi sera, mikakati na uendeshaji wa masuala ya kazi na uwezeshaji kiuchumi. Nataka maelezo zaidi kuhusiana zaidi na hili kutokana na kwamba Zanzibar tumebahatika kuwa na mifuko mingi.

Pamoja na mifuko mingi ambayo tumebahatika kuwa nayo, tuna wimbi kubwa sana la vijana ambao hawana ajira. Vijana hawa wanahangaika kwa namna moja au nyengine kuhakikisha kwamba wanaweza kufanya shughuli ya halali ambayo itawasaidia ili waweze kuongeza kipato chao na kujiendeleza kimaisha. Ukiangalia utaratibu mzima wa mifuko hii mingi ambayo tunayo haiwanufaishi ipasavyo kabisa vijana wetu ambao ndio walengwa hasa wa masuala haya. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie hasa ile mikakati na kuona vijana hawa wafuate taratibu zipi ili waweze kuona kwamba wanasaidiwa na

mifuko hii ambayo ni mingi na wanaondokana na umaskini ambao unawakabili kwa namna moja au nyengine.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 51 kuna suala zima la Zakka. Katika mfuko huu ningetaka kupata ufafanuzi zaidi. Neno lililotumika hapa ni Zakka na vikundi vya Ushirika ni vitu ambavyo vina hitilafiana. Sasa sijui kama hili neno lilikuwa limetumika hapa kimakosa au ni malengo hasa ya nano hili, na maana halisi iliyokusudiwa katika Zakka ndiyo imekuja katika mtandao huu. Nilimuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie zaidi.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 56 hapa kuna mafungu ya pesa za AK na JK, nikiangalia katika viambatanisho huku hususan kiambatanisho Nam. 7 kama sikosei, kumezungumziwa juu ya fungu hili ambalo kuna fedha ambazo zimekusanywa kutokana na watu ambao wametumia mwanzo, fedha hizi ni shilingi bilioni arubaini na moja, milioni mia nne na hamsini na tisa, kati ya deni lililokuwa linastahili kukusanywa ambalo ni bilioni mia nne na sabini na moja. Ukiangalia tofauti hapa ni kubwa sana na ni muda mrefu tumekuwa tukipata muelekeo huu wa kwamba fedha hizi ili wengine waweze kuneemeka, inahitaji marejesho mazuri ya wale waliokuwa wamepewa mwanzo.

Ukiangalia utaratibu mzima wa urejeshaji wa hizi pesa inaonekana kwamba unakwenda katika staili ya taratibu mno. Sijui Wizara ina mpango gani na ina utaratibu gani wa kuweza kuhakikisha kama vile zilivyokuwa zikitoka na ni utaratibu kama ule unachukuliwa katika harakati za kuona zinarejeshwa ili na maeneo mengine yaweze kuneemeka zaidi.

Nikiondoka hapo nakuja kwenye ukurasa wa 77 ambapo hapa kuna suala zima la ajira. Katika eneo hili kuna namna ambavyo wizara imejipanga kwa malengo yake ya kiutekelezaji kwa *bullet* Nam. 1-5. Mimi nilikuwa nataka kuzungumzia kipengele hichi cha tatu, kushajihisha jamii kuchukua hatua juu ya mauala ya ajira kwa vijana.

Mhe. Spika, kwa mfano sisi wana jimbo la Kikwajuni, tunalo eneo ambalo tunatumia kwa sababu ya maslahi na kuwasaidia vijana. Nilitaka kujua ni namna gani wizara itaweza kusaidia na kuweza kuona kile kitengo chetu cha kuwasaidia vijana ndani ya jimbo letu kinanufaika katika taratibu zipi kwa namna ipi na njia gani zipitwe ili tuone vijana ndani ya jimbo letu la Kikwajuni wananeemeka pamoja na wananchi wote wa Zanzibar kwa ujumla.

Mhe. Spika, kidogo nataka kwenda katika vifungu, kuna maeneo mengi ya vifungu kama mwanzo tulipokuwa tumesema tulipokuwa tukichangia kule, haya tutakuwa tukisubiri wakati wa bajeti ya Wizara ya Fedha ndipo tuweze kupata ufafanuzi wa kina kwa baadhi ya vifungu kwa mawizara ambayo tayari mengine yameshapita. Lakini kuna vifungu ambavyo vipo, kwa mfano katika wizara hii ya Kazi na Uwezeshaji katika fungu Nam. 0301 Ofisi Kuu Pemba *bullet* Nam. 211116 posho, vikao na kamati. Naomba ime-*shut* sana kutoka milioni mbili laki tisa na hamsini elfu mpaka milioni ishirini na tatu laki tatu na thalathini na tano elfu. Tungelimuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie inaonekana pana ongezeko kubwa kwa namna fulani.

Eneo jengine katika hiyo hiyo 0301 chini huku katika viburudishaji katika *bullet* 220200 katika eneo la chakula na vinywaji. Mwaka jana Mhe. Waziri tulimuidhinishia shilingi milioni tano laki sita na sabini na tano lakini mwaka huu Mhe. Waziri ameomba shilingi milioni ishirini na moja, laki mbili na hamsini elfu. Tuliomba ufafanuzi kutokana na ongezeko kubwa hili ambalo Mhe. Waziri ameliomba.

Jengine tukija katika kifungu Nam. 0501 Idara ya Uendeshaji na Utumishi hapa katika *bullet* 212100, 212101 mchango halisi wa Mfuko wa Hifadhi (*ZSSF*), mwaka jana tuliidhinisha milioni ishirini na moja laki tatu na arubaini na tatu elfu. Lakini mwaka huu tunatakiwa kuidhinisha milioni sabini na thamanini na nane elfu. Kuna nini huku Wizara ya Uwezeshaji, kuna ajira nyingi mpya ambazo ni zaidi asilimia mia zimepatikana hata ikabidi kuna ongezeko hili au mishahara imekuwa sana. Tunaomba Mhe. Waziri atakapokuja atusaidie vile vile.

Tukiondoka hapo tunakwenda katika Kifungu hicho hicho cha Idara ya Uendeshaji na Utumishi ukurasa wa 337 katika *bullet* 220800, 'Matengenezo ya Zana'. Huku chini kabisa chini kwenye kifungu 220806, 'Gharama za Bima na leseni za njia'. Kifungu hichi kipo katika Wizara hii lakini wizara nyingi za serikali zimekuwa zina vifungu kama hivi ambavyo tulikuwa tunataka baadae tuje kufahamu. Kwa mfano mwaka janan tulipitisha milioni nne kwa sababu ya kutafuta leseni na mambo ya vibali vya njia. Mwaka huu tunatakiwa tupitishe milioni 14, kuna ongezeko kubwa la magari au gharama zimepanda maradufu zaidi, kwa sababu imepanda zaidi ya asilimia mia mbili tuweze kuidhinisha kwa sababu ya suala hili.

Mhe. Spika, kifungu 0502, ‘Idara ya Mikopo’, hapa inaonekana mwaka jana hatukuidhinisha pesa katika mtandao mzima katika maeneo yote hayo kutoka mwanzo huku kwenye mishahara mpaka tunakuja chini huku ambako tunakuja kufungia katika ununuzi wa mashine na zana nyengine, isipokuwa katika upande wa ruzuku ndio tumeweza kuidhinisha pesa katika mwaka jana na mwaka huu hakukuidhinishwa kitu. Sasa sijui kulikuwa kuna nini hapa au hichi kitendo ni kipya au vipi, nilikuwa nataka kupata ufafanuzi ili niweze kujua.

Baada ya maelekezo hayo Mhe. Spika, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Kikwajuni naunga mkono hoja kwa asilimia 70 na asilimia naziachia mpaka nipate maelezo yatakayonitosheleza ili nizimalizie. Ahsante sana Mhe. Spika.(*Makofi*).

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kutokana na hali hii inaonesha Waheshimiwa Wajumbe wanamuogopa Mhe. Waziri wa Kazi.
Mhe. Spika, kwanza nataka nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nikazungumza machache katika Wizara hii ya Kazi, Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi. Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Kwamtipura nitanguliza shukurani za dhati kwa Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kuifanya kwa kuanzisha na kuilea Wizara hii mpaka hivi sasa tumeanza kuwa na matumaini makubwa katika mambo mbali ya kuwasaidia vijana wetu kuwapatia ajira.

Mhe. Spika, tuwapongeze Katibu Mkuu pamoja na Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara hii kwa mashirikiano makubwa sana wanayotupatia pale tunapokwenda Wizarani kwa matatizo mbali mbali

ambayo yanawagusa moja kwa moja wananchi wetu. Katika wizara hii sitokuwa na mambo mengi kwa sababu ushirikiano wa Mhe. Waziri anaotupa aidha kwa malalamiko au mahitaji au maoni mbali mbali ya wananchi kwa kweli tunapokwenda wizarani tunayapatia ufumbuzi kwa haraka sana. Tunampongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake na tunamuomba aendelee na mashirikiano haya ili kwa kujenga taifa letu hasa katika kutengeneza mazingira yakuwapatia ajira.

Mhe. Spika, kuna baadhi ya wenzangu walisema kwamba Wizara hii ni mpya, kwa hiyo inahitaji kuwezeshwa zaidi ili kuweza kujengwa hii wizara yenyewe. Wizara hii ukiiangalia Mhe. Spika, kazi zake nyingi za ufuatiliaji, watendaji wake wana kazi kubwa ya ufuatiliaji. Tatizo lililokuwepo la uhaba wa usafiri. Tunamuomba sana Mhe. Waziri tuangalie sana katika haya mafungu yetu tunayoyapata kuangalia kuweza kutatua matatizo ya usafiri hasa kwa watendaji ili waweze kuwafikia wananchi wetu.

Mhe. Spika, wenzangu wamezungumza kuna baadhi ya mikopo ambayo iliyotoka kupitia vikundi mbali mbali. Mikopo hii inataka kufuatiliwa na kwa hivyo lazima kutahitajika vipando au usafiri utakaowawezesha wale watendaji kuweza kufuatilia ili na wale wananchi waweze kuongeza kupata taaluma.

Mhe. Spika, nataka nizungumzie kidogo suala la ajira ya watoto. Namuomba sana Mhe. Waziri awaagize watendaji wake kuendelea kufuatilia hasa hizi ajira za watoto. Utawakuta kuna watoto wadogo wanaendelea kufanya kazi ambapo wakati ule wanatakiwa waende katika maskuli wao muda mwingi wanautumia katika kufanya biashara ndogo ndogo mbali mbali ambapo mara nyengine huwa biashara hizo

wanatumwa na wazazi wao kutokana na kujikimu na maisha. Pamoja na kujikimu na maisha mtoto mdogo anatakiwa apate zaidi nafasi ya kusoma pamoja na muda wa kucheza ili kuweza kuijenga akili yake iweze kutengemaa katika kufuatilia masuala ya masomo.

Mhe. Spika, kuna eneo moja ambalo Mhe. Waziri moja kwa moja halihusiani na utendaji wa serikali lakini ni taasisi ambazo zipo chini ya usimamizi wa Wizara yake, hivi vyama vya wafanyakazi. Kuna malalamiko makubw,a kuna mwana mama mmoja alikuja juzi hapa Barazani kwa bahati mimi nikatafutwa nikaonana nae na amekuja na kilio chake. Huyu ni muajiriwa wa Chama cha Wafanyakazi kama sikosei kinaitwa CHODAU. Huyu tangu kuajiriwa hajawahi kulipwa mshahara wake. Kama Mhe. Waziri amefuatana na viongozi wa vyama vya wafanyakazi basi kilio hichi mimi nikiwa mwakilishi wa wananchi kwa kweli sijakifurahia sana. Nilitegemea kwamba hivi vyama vya wafanyakazi vingelikuwa vipo mbele zaidi kutengeneza maslahi ya wafanyakazi kuliko hata serikali.
Vyama vya wafanyakazi vimeundwa maalum ili kuisukuma serikali kuweza kudai haki na kutetea maslahi ya wafanyakazi. Leo inasikitisha sana kwamba leo huyu ni mtendaji tena ni sekretari katika chombo hichi ambacho ni chombo cha wananchi, Chama cha Wafanyakazi zaidi ya miaka saba hajawahi kulipwa mshahara. Hebu tujiulize mtu huyu anaishi vipi? Kwa kweli ameshapata usumbufu mkubwa kufuatilia haki zake, amekwenda katika vikao mbali mbali. Fikiria kwamba mtu anatoka Pemba anakuja hapa katika mikutano yao ya vyama vya wafanyakazi, anadai maslahi yake katika vikao halali, matokezeo yake anaandikiwa barua ya kusimamishwa kazi kwa sababu amedai haki zake.

Mhe. Spika, hili pamoja na kama nilivyosema kwamba hivi moja kwa moja sio vyema vya Serikali lakini Mhe. Waziri ana wajibu kuvisimamia ili kuweza na wao kutenda haki. Mimi nitashangaa sana ikiwa Chama cha Wafanyakazi kinadai haki za wafanyakazi wakati wao wenyewe wale waajiriwa wao hawawalipi. Mimi nadhani Mhe. Waziri hili ajaribu kutusaidia kuliingilia kati, amtafute Mwenyekiti wa hichi chama ili kuweza kulipatia ufumbuzi suala la mwana dada huyu. Kipindi hichi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani mama huyu ametoka Pemba baada ya kusikia Baraza la Wawakilishi liko kazini na kwa bahati mbaya kule Pemba, televisheni kuna baadhi ya maeneo haipatikani vizuri. Kwa hivyo ameamua kuja mwenyewe na alitaka kuingia ndani humu, nikamwambia humu huruhusiwi kuingia, humu maneno yako nipe mimi nitayasema.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri kabla ya Jumatatu kuja kutujibu masuala yetu au siku ya Jumanne basi alifanyie kazi *atleast* aje na jawabu itakayoweze kuturidhisha na kuona umakini wa Mhe. Waziri kama kweli na hivi Vyama vya Wafanyakazi anajaribu kuvisimamia vile vile.
Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nataka nikumbushie ahadi ni deni. Mhe. Spika, mwaka uliopita katika bajeti hii ya Wizara hii, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, nilizungumza sana na nikamshauri Mhe. Waziri wa Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa Fedha katika mfuko mkuu wa serikali kutengwa fedha maalum kwa ajili ya kuanzisha benki ya akinamama pamoja na vijana. Benki ambayo tunatarajia au tungelitarajia ingelikuwa na masharti mepesi kabisa katika upatikanaji wa mikopo ili kuweza kuwaendeleza wananchi wetu kiuchumi. Mhe. Spika, tunaishukuru sana serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wenzetu baada ya kilio cha muda mrefu cha Waheshimiwa

Wabunge, serikali ilikisikia kilio kile na sasa hivi kule wenzetu Tanzania Bara tayari kuna ile Benki ya Maendeleo ya Akinamama.

Kuna mwenzangu Mhe. Wanu juzi alizungumza alipokuwa akizungumza kuhusu suala la wizara ya Mheshimiwa mama yangu Mhe. Zainab Omar Wizara ya akinamama, alishauri kwamba liwekwe tawi hapa la ile benki ya maendeleo ya akinamama, sio tatizo lakini akinamama wa Zanzibar walipiga kura mbili. Walimpigia kura Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini vile vile walimpigia kura Rais wa Zanzibar pamoja na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo bado haki yao ya kimsingi kutoka kwa Rais wao mpendwa Dr. Ali Mohammed Shein kuanzishia benki akinamama, kwa kweli atakuwa amewaneemesha sana wananchi kiuchumi. Mimi kwa upande wa Mhe. Rais katika wazo hili naamini sina wasi wasi naye kwa sababu kwa kuona umuhimu na kuongoze ajira na kuwapatia ajira vijana wakiwemo akinamama ameanzisha wizara maalum *special* kwa ajili ya kushughulikia uwezeshaji wa kiuchumi. Naamini akipelekewa wazo hili la kutoa fedha katika mfuko mkuu wa serikali ili kuweza kuanzisha benki mimi naamini Mhe. Rais atalikubali kwa moyo mkunjufu suala hili.
Kama ninavyosema siku zote Mhe. Spika, suala la kusema tunatoa tu hii mikopo ya AK na JK kwa vikundi bado kwa kweli hatujaweka hasa ile *foundation* ya kuweza kuwasaidia vijana hasa katika shughuli zao za kibiashara. Mhe, benki ni chombo pekee ambacho kinachoweza kuwawezesha hao wananchi kwa sababu kama tunavyojua benki zile watakuwa wanaekeza fedha zao, fedha zile zitakuwa vile vile zinaelekezwa kwa hivi vikundi na fedha zile katika benki zinakuwa hazishi, zinakuwa *revolving fund* mfuko ambao unazunguka. Mimi nadhani Mhe. Spika, mwaka jana Mhe. Waziri aliniahidi kwamba atashirikiana na benki ya *CRDB* ili kuweza kutafuta utaratibu wa kuwawezesha wananchi katika hatua za mwanzo, kabla ile

kuanzisha hasa ile benki yenyewe ambayo itakayotoa na fedha za kodi za wananchi mfuko mkuu wa serikali. Sasa hizi hatua sijui labda Mhe. Waziri atakuwa amefikia wapi.

Lakini jengine Mhe. Spika, tumeona hapa katika kitabu imeelezwa hapa kwamba vibali vya hawa wageni vimeongezeka karibu mara dufu kutoka dola 150 mpaka dola 2000. Sasa hili hebu sijui lengo lake hasa lilikuwa nini kuwafukuza wageni au kuwapunguza wageni au kulikuwa na malengo gani hapa kidogo nitakuja kuhitaji ufafanuzi wa ziada.

Jengine Mhe. Spika, hili nilikuwa nataka ikiwezekana nije nijibiwe hata kama na Waziri wa Miundombinu, kuna suala ambalo juzi nililizungumza na kwa sababu ni suala ambalo linahusu ajira basi naliunganisha moja kwa moja kwa Mhe. Waziri kwamba sijui katika sheria au mikataba ya usajili wa meli za nje kwa kutumia jina la Zanzibar na kupeperusha bendera ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutumia jina la Zanzibar.

Kwa hivyo niliwahi kupata taarifa ile sheria nimejaribu kuitafuta sijaiona sasa Mhe. Waziri aje atusaidie kwa sababu kwa taarifa tuliyoipata kwamba katika kila meli katika mkataba inatakiwa alau wafanyakazi watano katika meli hizi zinazosajiliwa kwa kutumia jina la Zanzibar alau awe anatoka Zanzibar. Sasa suala hili sijui kama lipo au kama halipo nije nipate jawabu lakini kama halipo mimi nadhani kwa kuwa hawa ambao wanaosajili meli zao kwa kutumia majina ya Zanzibar mimi nadhani moja katika fursa ambayo wanayofaidika na sisi tunahitaji lazima vijana wetu waweze kufaidika na ajira hizo. Kwa hivyo Mhe. Spika, nitamuomba sana Mhe. Waziri kama kipengele hiki kipo sijui Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji

Wananchi Kiuchumi analifuatilia vipi suala la ajira ya hawa vijana wetu katika meli hizi za nje ambazo zinavyofanya kazi katika bahari ya kimataifa. Sasa hili nadhani nitakuja kupata jawabu na kama atakuwa hana uhakika kama nilivyosema basi kwa kuwa mawaziri wanafanya kazi kwa pamoja awasiliane na Wizara ya Miundombinu ili kuweza kujua kwamba sheria hii ipo na kama haipo basi lazima kufanywe marekebsho ili kiwepo kipengele hiki ili kuweza kusaidia kuondoa tatizo la ajira kwa upande wa Zanzibar.

Na mwisho kabisa Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba Wizara hii kwa kweli ni mpya na wanahitaji kuboreshwa na wanafanya kazi zao vizuri sisi ni wajibu wetu kuweza kuwatia moyo kwa pale ambapo wanapofanya vizuri.

Mhe. Spika, nataka nimalizie suala la ajira za mikataba. Hili suala bado ni tatizo na kama nilivyosema kwamba wenzetu hasa nchi za Asia Mashariki, ukiangalia katika magazeti mbali mbali utakuta kwamba zinatoka nafasi za kazi wanatangaza haya makampuni ya hapa kwetu au hizi *private sector* sidhani kama ajira zao wanatangaza. Kama ajira wenzetu wanavyotangaza utakuta mule mna vipengele hasa vinasema kwamba tunataka wafanyakazi aidha katika taasisi fulani, *priority* wale wazalendo katika nchi ile, ile inawekwa kipaumbele wale wazalendo wa nchi ile. Halafu sio wazalendo tu lakini vile vile kuna na maslahi ambayo yanatajwa katika yale matangazo. Kwa hivyo Mhe. Spika, utakuta mtu anaomba nafasi ya ajira kwa kupitia kwenye vyombo vya habari. Aidha magazeti au hivi vyombo vyengine kupitia katika mitandao mbali mbali.

Sasa hizi ajira zetu zinakwenda kificho-ficho kwa sababu ina maana kama hazitangazwi, samahani sana Mhe. Spika, sikukusudia kukutania lakini unajua Kiswahili kina maneno mengi ambayo ya sitiari, bora nitumie jina la zinakwenda chini chini bila ya kutangazwa. Sasa Mhe. Spika, mimi nadhani Mhe. Waziri angeliweka utaratibu na akatoa toleo hasa kwa taasisi zote binafsi wanapotaka kutoa ajira lazima watoe matangazo na katika yale matangazo waeleze na zile *incentives* ambazo zitakazowafanya watu wavutiwe katika ajira hizi na pale watakapotoa matangazo ndio pale ambapo lazima katika zile kampuni au taasisi mbali mbali ambazo wanaotoa yale matangazo ya ajira bila shaka lazima kutakuwa na mikataba. Sasa hii mikataba lazima iainishe wazi wazi mishahara yao, haki zao za likizo, haki zao za likizo za uzazi.

Kwa sababu Mhe. Spika, hasa akinamama wanapata tabu sana katika hizi taasisi binafsi mtu anapopata ujauzito akianza kutapika tapika na vitu vyengine, anasimamishwa kazi na wakati mwengine hata kama hakuwahi kutapika tapika pale wakati anapokwenda kujifungua ina maana ndio tayari amekwenda kujifukuzisha kazi. Sasa leo Mhe. Spika, kama ingelikuwa Zanzibar tuko wengi na tumetunga ile sheria ya kila mtu kuzaa mtoto mmoja basi pia ingelikuwa afadhali. Lakini sisi Mhe. Spika, dini yetu ya Kiislamu inatwambia kwamba ujitahidi wapishane tu miaka miwili miwili kama unaweza kuwatoa watoe lakini kwa kuangalia na hali ya mama kiafya vile vile. Hapa inapofikia pahala mtu anakwenda kujifungua anaachishwa kazi kwa kweli hii inakuwa sio haki. Mimi naomba sana Mhe. Waziri tutengeneze huo utaratibu kama nilivyoshauri wawe wanatoa matangazo lakini vile vile katika mikataba ielezwe vile vile hasa kwa wale akinamama ambao watakaopata ujauzito vile vile na zile haki zao za kunyonyesha na wengine kwa sababu ile likizo inakuwa ya muda mfupi ya kujifungua baada ya kujifungua anaruhusiwa kwenda kazini lakini ule muda wa kupata kunyonyesha. Tunashukuru sasa hivi serikalini utaratibu huo upo,

wafanyakazi wanaruhusiwa wanakwenda kunyonyesha halafu anarudi anakuja kuchapa kazi. Kwa hivyo Mhe. Spika, hayo ilikuwa ndio maoni yangu katika wizara hii na naendelea tena kumpongeza sana Mhe. Waziri lakini vile vile aje atusaidie tu zile ajira za Qatar sijui zimekwishia wapi. Kwa sababu unajua vijana wetu kila siku simu Mheshimiwa vipi Qatar, paspoti tayari Qatar bado, sasa hili nafikiri likiweza tukilipatia ufumbuzi nadhani Mhe. Waziri bajeti yake haina matatizo sana.

Baada ya hayo machache kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura wamenambia nimpe shukurani Mhe. Waziri na tunaunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri kwa asilimia 100. Ahsante sana.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, na mimi naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia leo siku ya Ijumaa kupata nafasi hii fupi ya kuchangia hotuba hii ya bajeti ya mwaka 2013/2014 ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Mhe. Spika, kwanza nitoe pongezi za dhati kwa Mhe. Waziri ambaye kwa leo siku ya Ijumaa sitokosea kumwita Shekhe kwa namna alivyowasilisha kitabu chake kikubwa kwa dakika chache sana kuliko Mhe. Waziri yeyote aliyewasilisha bajeti yake hapa kwa mwaka huu wa fedha.

Pili Mhe. Spika, nianze kwa kusema wizara hii Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika ni wizara mpya lakini ni muhimu sana katika wizara zetu 16 tulizonazo, kwa sababu inajihusisha moja kwa moja na maisha ya wananchi na hasa vijana katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini kwa mpango wa kujiajiri wao wenyewe. Naipongeza sana Wizara kwa kuanzia Mhe. Waziri na kupitia

watendaji wake kwa namna wanavyowashughulikia wananchi katika kuwasaidia katika matatizo yao ya kiuchumi. Wanapitia katika vikundi mbali mbali, wanatoa mikopo na misaada mbali mbali na wanaelekeza maelekezo mbali mbali kiasi ambacho mabadiliko yameonekana kabla ya kuweko wizara hii na hivi sasa ilipo.

Moja Mhe. Spika, ya kazi kubwa anayofanya Mhe. Waziri na wizara yake kuona kuwa wananchi na hasa vijana wanajikwamua katika hali ngumu ya kimaisha ni kutoa mikopo, inatolewa tokea kwa watu binafsi na kunatolewa mikopo kwa vikundi maalum na wanafanya ukaguzi kuonesha kuwa mikopo ile inatoa tija na pia kutoa maelekezo pale inapostahiki. Pamoja na yote hayo Mhe. Spika, na uzuri wa kitabu kilivyo na juhudi ya Mhe. Waziri na watendaji wake hata hivyo naomba kidogo kupata ufafanuzi katika kitabu chake kwa yale mambo ambayo kidogo sijayafahamu katika hali halisi ili wizara hii pengine iweze kufanya kazi yake kwa ufanisi zaidi kuliko hapa ilipo.

Kwa sababu hiyo Mhe. Spika, pamoja na kuwa imeshazungumzwa sana lakini kila mtu na mbinu zake, naomba nianze pale pale Idara ya Mikopo ambayo iko katika ukurasa wa 53 wa kitabu hiki na majadweli yake ambayo yapo ukurasa 107. Sasa Mhe. Spika, kwa mujibu wa maelezo ya kitabu ilivyo ni kuwa wizara ina mifuko miwili inayotoa mikopo kwa wananchi ni mfuko wa kujitegemea na mfuko huo ni wa AK, JK. Katika mfuko wa kujitegemea kwa muda wa mwaka alivyoeleza mwenyewe ukurasa wa 4 kiambatisho namba 4 ukurasa 107 ni kuwa huu unahusiana na utoaji wa mikopo kwa kipindi cha mwaka 2012/2013.

Sasa Mheshimiwa katika utoaji huu jumla ya fedha iliyotolewa kwa Unguja na Pemba ni milioni mia moja na hamsini sita na kati ya hizo Unguja ni milioni mia moja na kumi na mbili na Pemba ni milioni arubaini na nne. Ninashukuru kiambatisho kimegawa mikopo hii kiwilaya katika Wilaya zote kumi. Sasa hapa mimi ufafanuzi nilionao ninaomba kutokana na mikopo hii kwa kisiwa cha Unguja chenye Wilaya sita; kuna Wilaya ya Kati imepata mkopo wa milioni nane tu wakati ni kidogo sana kweli ukilinganisha na Wilaya nyengine ambazo kuna Wilaya ya Mjini miliono ishirini na sita, kuna Wilaya ya Magharibi milioni ishirini na nane, kuna Wilaya ya Kaskazini "A" milioni ishirini na tatu, kuna Wilaya ya Kaskazini "B" milioni kumi na moja na Wilaya ya Kusini milioni klumi na nne. Nikitaka kujua kwa nini hii Wilaya ya Kati ikapata mkopo kidogo sana kweli kweli. Ukiangalia kama Wilaya imepata milioni ishirini na nane wao wakapata milioni nane ni jambo ambalo linahitaji maelezo, pengine inaweza kuwa ni sawa lakini kwa mimi kwa kuona nambari tu hapa naomba kupata maelezo kuhusu Wilaya hii.

Kwa Pemba Mhe. Spika, ninavyofahamu na ndio inavyoelezwa na tunavyoamini kuwa katika Wilaya nne za Pemba Wilaya ya Micheweni ndio Wilaya maskini kabisa kuliko Wilaya zote na tunatoa mkopo kwa makusudi ya kuondoa umaskini, makusudi ya kuwasaidia wananchi wetu kimapato ili waweze kujiendeleza. Lakini Wilaya hii ya Micheweni imepata mkopo wa shilingi milioni nne na laki mbili tu, wakati kuna Wilaya ya Mkoani milioni kumi na tano na kadhalika. Ningeliomba kupata maelezo Wilaya maskini kama hii ambayo kwa mimi ningetarajia wapate mkopo mkubwa kwa sababu wananchi *in general* maskini, hata watoto wao wamefanya ajira za watoto ambazo Mhe. Waziri anapingana nazo kutokana na umaskini walionao ilikuwaje ikawa mkopo wao ni mdogo sana, hiyo ni kwenye mikopo.

Na kwa utoaji wa mkopo kupitia mfuko wa AK, JK kuanzia Julai mwaka 2012 hadi Juni, 2013 ni jumla ya shilingi za Kitanzania milioni arubaini na saba na milioni hizi arubaini na saba zimegaiwa kwa Wilaya nne tu za Unguja. Naomba kujua Wilaya mbili za Unguja na Wilaya nne za Pemba kwa mwaka huu wa kuanzia Julai, 2012 hadi Juni 2013 ni mwaka mzima hawakupata mkopo huu wa AK, JK au pengine kama kuna mahala imeandikwa katika kiambatisho hiki, sijaiona naomba maelezo Mheshimiwa.

Jengine Mhe. Spika, ni kuwa kuna jadweli hapa ambayo ni jadweli nambari saba na jadweli hii inahusiana na utoaji na urejeshaji wa mikopo kupitia mfuko wa JK, AK, hadi Juni 2013 kwa Unguja na Pemba. Mhe. Spika, ninashukuru kwanza hii jadweli imeeleza Wilaya, idadi waliyokopa, fedha zilizokopwa, fedha zilizorejeshwa, fedha iliyobakia na fedha iliyorejeshwa baada ya hapo yaani kuanzia Julai 2012 hadi 2013.

Sasa tukiangalia hapa tuna mfano Kaskazini "B" hawa walikopeshwa shilingi za Kitanzania milioni mia moja na sitini na sita, laki tatu na thamanini na nane mia tano na sabini na tano na senti 35. Wakalipa milioni thamanini na nane na elfu kumi na sita mia mbili na kumi na nane na deni lilobakia ni milioni sabini na nane, laki tatu na sabini na mbili mia tatu na hamsini na saba, katika deni hili la shilingi sabini na nane milioni na ushei kama nilivyoeleza kwa kipindi cha Julai, 2012 hadi Mei 2013 walirejesha shilingi milioni tatu tu katika sabini na nane. Je, kwa sababu hawakufuatiliwa vilivyo kwa sababu kuna wengine ninashukuru wamerejesha vizuri sana kweli kweli. Kwa hivyo nataka nijue hao waliopewa pesa nyingi sana kuliko wote yaani milioni mia moja na sitini na sita kwa nini wakarejesha kidogo kiasi hicho.

Halafu jengine Mheshimiwa ninalopenda kuelewa ni kuwa na pia kuna Wilaya ya Mjini walipewa fedha nyingi sana tu milioni mia mbili na kumi na tisa wakalipa mia moja na kumi na moja zikabaki milioni mia moja na nane na kidogo, lakini na wao ziada walirejesha tisa tu kutoka milioni mia moja na nane. Kama fahamu zangu ndivyo ilivyo naomba na hili nipate maelekezo ni ufuatiliaji au tuseme kuna sababu gani, huku ni Unguja.

Na kwa upande wa Pemba Mhe. Spika, kama nilivyosema ni kuwa kama walivyoeleza wenyewe katika kitabu walipita Pemba na Unguja kuwaomba watu warejeshe fedha yao, lakini Wilaya ya Micheweni ambayo ilikuwa na wakopaji 49 fedha walizokopa zikiwa ni milioni arubaini na nne na laki tano na wakalipa milioni thalathini na mbili na thamanini na saba elfu mia mbili na sabini na nane, zikabakia hamsini na mbali milioni laki nne na kumi na mbili elfu mia saba na ishirini na mbili wakati huu wa ziada yaani kuanzia Julai, 2012 mpaka Mei, 2013 hawakulipa hata senti moja. Ni kuwa hawakwenda kudaiwa watu hawa au vipi. Nasema hivi kwa sababu hii pesa ikirejeshwa ndipo Wizara inapopata nguvu za kukopesha wengine na wako watu wengi wa kukopesha. Kwa hivyo hili naomba pia nipewe maelekezo.

Wilaya nyengine ya Chake Chake ilikopeshwa watu jumla ya 88 fedha iliyokopeshwa ni shilingi milioni mia mbili na ishirini na sita laki nane hamsini, fedha iliyorejeshwa hadi Mei 2013 ni milioni mia moja na ishirini na laki tisa na ishirini mia tisa na thamanini na tisa na wana deni la milioni mia moja na laki tisa na ishirini tisa na shilingi kumi na moja. Lakini hii ya ziada kuanzia Julai, 2012 hadi Mei 2013 wamerejesha milioni nne tu laki mbili na sabaini na tatu na sitini na tisa sijui kwa nini na wao wakarejesha fedha hii.

Kwa hivyo inaonekana pengine kutoka Wilaya hadi Wilaya kuna tofauti ya watu wanavyojikaza katika kuwapitia hawa watu kurejesha fedha kwenye hii mikopo naomba nipate maelezo hayo.

Jengine Mheshimiwa nikuwa Wizara yetu, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika inawahimiza watu kujiajiri na ninashukuru vijana wetu wanawake na wanaume wanajitafutia maisha kwa njia hii ya halali kabisa ya kujiajiri. Na unapofanya ajira ya biashara ya kuuza, ya kutembeza, siku zote utatafuta pale penye watu ili biashara ile itoke. Kwa bahati mbaya kutokana na nchi yetu kimazingira ilivyo na hali ngumu ya maisha vijana wetu kwa makundi ili waweze kujipatia maisha wamejiajiri katika ajira tofauti za kuuza biashara ndogo ndogo. Katika msimu huu wa Ramadhani wakati kuna sikukuu na tuna utamaduni wa Wazanzibari ikifika siku kuu watu wavae vizuri japo siku mbili tatu uonekane mwezi mtukufu wa Ramadhan umepita biashara ya vitambaa inakwenda katika hali ya kazi kabisa, na kwa sababu watu wetu maskini wanapenda sana kununua vitambaa ambavyo vinanunulika ili watoto wao waweze kuenea. Kwa bahati mbaya au nzuri watu hao kwa kujitafutia maisha kwa makusudi wanajikusanya katika miji hasa Unguja Darajani na Pemba katika sehemu nyengine za miji.

Mheshimiwa lililotolea mpaka juzi ni kuwa wafanyabiashara hawa wanapata adhabu kubwa sana, wanafanya kazi katika nchi yao kazi ya halali wanajitafutia maisha wengine wana wake na watoto, hali za majumbani za kimaskini na huu ndio msimu wetu wanapata dhiki sana. Wanafukuzana na maaskari, wanapigwa na maaskari, wananyang'anywa mali zao imekuwa adha leo wanapigwa na kesho wanakuja tena kwa sababu hawana tena vya kufanya. Mimi ninamuomba Mhe. Waziri anieleze vizuri kwa sababu ndio mfumo wake kuwa watu wajiajiri, wajitafutie maisha na biashara kama haijanunuliwa hapana maisha

ni hasara tupu na haya ndio yanayowafika. Ili waweze kuendelea na ule mfumo wa kujiajiri Mhe. Waziri ana mpango gani hasa wa kuona kwamba vijana hawa wamejengewa jengo zuri la kisasa kama ilivyo duniani, hata hapo Bara wamefanya vijana hawa wakusanyike mahala ambapo ni panapostahiki na wanafanya kazi yao ya uhalali na waondokane na balaa hii wanayoipata kila siku ambayo inafanywa na Baraza la Mji ili kuweka usafi mji pamoja na kuwa pana taka zinazonuka kila siku zinachelewa pale *Darajani Stand*.

Mheshimiwa pili kwa kupitia kwako namuomba Mhe. Waziri azungumze na Waziri anayehusika na vitendo hivi kwa mwezi huu wa Ramadhan wale vijana wachiwe alau wajipatie riziki, hii ni nchi ina wenyewe na Katiba yetu inasema Serikali hii ni ya wananchi, kwa hivyo wananchi wasionekane kuwa wana dhiki na kwa vile kule mikandaani si kwa pahala pakuuzwa vitambaa ni pahala pa kuuza samaki tu, hebu na sisi turudi kwa kuwahudumia wananchi wawekwe mahala ambapo stahiki kwa Unguja na Pemba ili huo mji uwe safi lakini na biashara zao ziende na maisha, yaende yasitokee tena mambo ya kupingana baina ya Waziri na Waziri, huyu anahimiza, huyu anatia adabu. Hilo ni moja.
Mhe. Spika, jengine ninaloomba kuzungumza ni kuwa Mhe. Waziri kasema katika kitabu chake kuwa ana mpango wa kupatiwa fursa za ajira za heshima kwa wananchi wanaume na wanawake. Kwanza ninampongeza kwa kusema ajira za heshima. Mhe. Spika, tukiangalia katika nchi yetu sasa imezidiwa na wasomi wengi kuliko uwezo wa Serikali kuweza kuwaajiri. Wafanyabiashara wadogo wadogo ni wengi, Wazanzibari na wasiokuwa Wazanzibari na wasiokuwa Watanzania kiasi ambacho hakuna tena biashara ndogo ndogo za kufanya mtu kujiendeshea maisha. Biashara za viwanda nakadhalika, uwezo huo ni wa wachache wao hawana, lakini tumewasomesha na wameelimika. Kwa hivyo basi kwa sababu kulikuwa na

mpango kwa hawa vijana wetu wasidhurure ovyo wa kwenda nje ya nchi na mpango ule ulifeli kutokana na kuwa haukuwa na maandalizi mazuri pale mwanzo. Mimi ningelimuomba Mhe. Waziri atupe maelekezo wasomi hawa tulionao na uwezo wa kuwaajiri hatuna na kwa Zanzibar wote kwa kazi ya kufanya kuyaendesha maisha bila ya kuwezesha, kwa maana ya kuwezeshwa kufanya mambo ambayo hawafanyi wengine ni mdogo. Hivyo ana mpango gani wa kuona kuwa vijana hawa wametafutiwa ajira nje ya nchi ajira ambayo itakuwa ni yenye heshima na ajira ambayo ni ya kulinda utamaduni wa Zanzibar ili wao waweze kuendesha maisha yao, waweze kusaidia familia zao na kuweza kuinua uchumi wa nchi yao kama wengine walioko nje ya nchi.

La mwisho Mhe. Spika, ni kuwa ningelimwambia tu Mhe. Waziri kuwa anajitaidi sana kutoa misaada kwa vikundi mbali mbali, lakini vikundi vimeibuka zaidi ya uwezo wa Mhe. Waziri, kutokana na hiyo fedha anayoipata. Kwa hivyo kuna watu wameibua miradi hasa hii miradi ya ufugaji wa samaki ambayo inahitaji msaada kwa vyovyote vile na wameshakwama njiani. Mimi ningeliomba nitoe ushauri kwa hili, wale wote wanaojiingiza katika miradi hii kwa kufuata agizo la Serikali kwa kupitia Mhe. Waziri, ni wengi na kwa sababu uwezo wa kuwasaidia wote haupo, ningelimuomba Mhe. Waziri alau afanye kwa makusudi kuwa na takwimu kutoka jimbo hadi jimbo mambo yaliyopo awe na mpango wa makusudi kuwapitia hawa watu kila wakati ili kutoa maelekezo wasifeli waone kuwa japo kuwa hawajapata msaada lakini wawe wanapitia waendelee na Mwenyezi Mungu akimpa uwezo inshallah aweze kuwasaidia watu hawa.

Na la mwisho kuliko yote nimepewa ujumbe niufikishe kwa Mhe. Waziri, kwanza nimsifu alipokuja Pemba kutoa zakka alikwenda kutembelea mradi mmoja wa *SACCOS* uliopo katika Jimbo langu la

Mtambwe, alipofika pale kwa namna alivyoiona ile halisi jinsi ilivyo, yeye mwenyewe aliahidi kutoa misaada ambayo sihitaji kuutaja hapa mwenyewe anaelewa. Kwa hivyo, namueleza tu Mhe. Waziri, wale watu tayari pale ulipowakuta wameshaendelea zaidi hivi sasa na wanaomba uwasaidie ule msaada waliokuomba ili wazidi kujikwamua kiuchumi.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na naiunga mkono bajeti hii asilimia mia kwa mia.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa dhati kabisa kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, mwalimu wangu, swahiba wangu Mhe. Haroun Ali Suleiman. Mhe. Spika, na mimi nishukuru kwa dhati na nimpongeze Mhe. Waziri kwa namna ambavyo amekuwa akionesha ushirikiano wa dhati katika kuwawezesha wananchi na vijana wa nchi hii kwa kweli Mhe. Waziri, ni wa kupigiwa mfano kwa namna ya utendaji wake wa kazi yeye pamoja na watendaji wake. Kwa sababu anajua nani wenye wananchi, wenye wananchi ni sisi Wawakilishi ambao tunawawakilisha wananchi. Kwa hivyo mara nyingi huwa anatumia busara za kufanya kazi zake kwa kuwashirikisha Wawakilishi wa wananchi katika kuwapatia huduma mbali mbali, nalo ndio leo linaonesha dhahiri pale tunapofika pahala ukasema majadiliano yanaendelea, kwa sababu kila Mwakilishi ameridhika na utendaji kazi wa Wizara hii na ndio maana tutatafuta hata namna gani ya kutafuta wapi tuchangie na wapi tuseme, lakini kwa sababu ni wajibu wetu na panapo mazuri na mapungufu hatuachi. Kwa hivyo na sisi tunaomba tuendelee kuchangia Mhe. Spika.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nataka nichangie kama maeneo mawili matatu. Kwanza kwenye ukurasa wa 19 katika eneo zima la elimu kwa vijana. Niipongeze kwa vijana, nipongeze kwa Wizara kwa kuweza kusomesha vijana karibuni 901 katika fani za ujasiriamali pamoja na katika fani ya namna ya kuweza kumudu kufanya shughuli za kibiashara. Mhe. Spika, lengo ni zuri, dhamira bora lakini bado pamoja na mambo ambayo yamefanywa katika taasisi hii, pamoja na kuwapatia elimu vijana hawa bado kuna matatizo mawili matatu ambayo yamejitokeza katika eneo hili.

Mhe. Spika, unapomsomesha mtu, akishapata elimu basi huwa anatarajia mambo mawili ayapate. Aidha apate kazi kutokana na elimu yake au apate mtaji ambao utaweza kumsaidia kutokana na elimu aliyoipata ili aweze kujiajiri, lakini kama utampa elimu tu na tukafikia hapa kwamba aah! tumewapa elimu vijana 901 kama hatukuwatafutia namna ya wale ambao tumewapa elimu ya ujasiriamali na biashara ya kuweza kumudu maisha yao basi bado elimu ile itakuwa haifanyi kazi, itakuwa mtu ana elimu ndani ya *pocket* anahangaika lakini faida ya kuitumia ile elimu hana.

Mhe. Spika, kwa sababu ya kusema hivyo hivi karibuni tu Mhe. Waziri amesomesha vijana wa kikundi kinachoitwa *KNN Co-operative*, vijana hawa wamepata mafunzo ya namna ya kuendesha biashara binafsi au biashara ndogo ndogo na elimu hii imetolewa na Wizara pamoja na Shirika la Kazi Duniani (*ILO*). Kwa bahati nzuri vijana hawa walikuwa na vijana wenzao wa Tanzania Bara. Sasa kwa ule upande mmoja wa Tanzania Bara vijana wale tayari taasisi za kule Bara zimeshawapatia mitaji na mifuko ya kuweza kujiajiri na kufanya shughuli za kibiashara, lakini kwa upande wetu bado vijana hawa hawajapata *supporter* ya kutosha ili kuweza kujiajiri kutokana na elimu waliyoipata. Nimuombe Mhe. Waziri kikundi hichi cha *KNN Co-operative* akiangalie kwa jicho la huruma na kuona namna gani anaweza kutoa ushirikiano nao

kwa sababu ya namna moja, wanaweza wakasaidia mitaji lakini kwa sababu ya elimu waliyokuwa nayo pia wanaweza wenyewe vijana, Wizara ikaweza kuwatumia kwa kusomesha vijana wenzao katika maeneo mbali mbali ya majimbo yetu.

Mhe. Spika, sasa ninataka nizungumzie pia katika suala la ajira kwa vijana. Mhe. Spika, bado tunakuwa tunapata tabu sana na nafikiri hapa labda Mhe. Waziri pamoja na Serikali niwaombe au tuwaombe kuna haja ya kujipanga katika mazingira mazuri. Wizara zetu Mhe. Spika, zinakuwa zina muingiliano na kuna mambo kidogo sisi wengine yanakuwa hatuyafahamu sio sisi tu, lakini hata na vijana wetu na hata ripoti zinapokuja pia zinakuwa zina migongano. Kuna Wizara yetu ya Wanawake na Watoto na kuna Wizara ya Uwezeshaji, katika suala la ajira kwa vijana kuna mambo huwa yanagongana-gongana.

Mhe. Spika, kuna suala hili la mashamba ya kilimo cha mauwa, akija Waziri wa Wanawake na Watoto analizungumzia suala hili halijaleta mafanikio, akija Waziri wa Uwezeshaji ndio hivyo hivyo, sasa unajua hili suala kama lingelikaa *specific* katika Wizara moja, mimi nafikiri hata yale malengo kwa vijana wetu tunakuwa tunaweza kuwapa wepesi wa kuona namna gani ili katika kutatua masuala mazima ya kuweza kujiajiri katika masuala ya kuanzisha haya mashamba, vyenginevyo Mheshimiwa itakuwa mtu akenda huku anaambiwa aah! huku uwezo hakuna, akenda huku anaambiwa nenda Wizara hii, sasa kidogo linakuwa linatupa mashaka sana.

Mhe. Spika, chengine ambacho ninataka nikizungumzie na kwa bahati nimeshakuwa ninakipigia kelele sana ni suala zima la utoaji wa fedha za vikundi. Nasema Wizara inajitahidi pamoja na Serikali na yale

yale niliyoyazungumza mwanzo kwamba Waziri huwa anajitahidi kutaka ushauri kwa Waheshimiwa Wawakilishi katika namna ya kusaidia vikundi vya ushirika katika maeneo yetu na kwa kweli mimi kwa upande wangu nashukuru mashirikiano yamepatikana vikundi ambavyo vimefarijika na wananchi kama alivyosema Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura na Jimbo la Kwahani nao wamemshukuru Mhe. Haruna kwa kuweza kuvisaidia vikundi hivi kupata mikopo midogo midogo ya kuweza kujisaidia.

Mhe. Spika, kubwa ambalo ninataka kulizungumzia hapa ni kwamba nimuombe Mhe. Waziri kutafuta namna mbadala ya utoaji wa fedha za vikundi, kwa sababu tunavisaidia vikundi vipate pesa ili waweze kujiajiri kuondokana na umaskini. Lakini tatizo tunakuwa tunaangalia kuvipa vikundi utitiri ili kujenga sifa kwamba aah! vikundi hamsini Jimbo la Kwahani au vikundi ishirini kwa Jimbo la Kwamtipura, lakini kila tutachowapa kama tutaangalia vikundi viwili tukiviwezesha ule mtaji ambao utakuwa mkubwa ni imani lile lengo na dhamira la kuondosha umaskini litafikiwa, si lazima kila kikundi kipate. Sasa tunakuwa tunawapa pesa ndogo ndogo, unakipa kikundi shs.1,000,000/= watu 30 hata ule mtaji wenyewe au ule mradi wa kufanya unakuwa una ugumu. Bora fedha zile zikakusanywa kuwapa vikundi vitatu kama shs.10,000,000/= au shs.15,000,000/= kikapewa kikundi kimoja au vikundi viwili milioni saba saba, imani yangu watapata mafanikio hata na wao wanaweza wakazalisha kitu wakasaidia hivyo vikundi vya wenzao. Sasa ule utitiri wa kutoa pesa ndogo ndogo kwa kweli mafanikio yanakuwa hapana na matokeo yake kama hatukuwa makini na fedha kama haikuweza ku-*rotate* basi ni hatari hata ile fedha yenyewe kutokupata faida na mtaji ukakatika. Sasa nimuombe Mhe. Waziri aangalie namna mbadala baada ya kwenda katika hali ya utitiri basi tukusanye fungu lililokuwa kubwa tuvipe vikundi vichache, imani yangu waliobakia watakuwa na

moyo wa subira kwa sababu jitihada za Wizara kama nilivyosema zinaonekana na sisi Wawakilishi tumejenga matumaini na mifuko inayotolewa na hatuna mashaka na Mhe. Waziri katika utendaji wa kazi.

Mhe. Spika, nataka nitoe wazo kwa Mhe. Waziri kwa sababu ya uwezo wake na upeo aliokuwa nao sisi hatuna mashaka nae, nitoe wazo kwa kumsaidia. Mhe. Spika, ukiachilia mbali suala ambalo anajitahidi kutafuta fedha za hii mifuko ya vikundi vya ushirika kupitia taasisi za serikali yetu ya ndani pamoja na taasisi za nje, nimuombe aanze kupiga mbio basi kutafuta namna ya kuweza kuanzisha viwanda vidogo vidogo. Mhe. Spika, fedha ni sehemu nyengine lakini ni viwanda vidogo ni sehemu nyengine ya kusaidia ajira kwa vijana wetu.

Mhe. Spika, sasa kuna mambo mengi na Mawaziri wameshatembea nchi nyingi na wameshaona mengi sana, sisi wengine huku hatujafika China, hatujafika sijui nyengine wao wanafika kuona miradi ya watu ambao wanaanzisha viwanda vya kufuga samaki, viwanda vya kusindika matunda. Sasa haya mambo mengi, nasema kwamba kama tutakuwa tunayaanzisha na kama Mhe. Waziri atajaribu kuangalia katika eneo hili basi tunaweza kupunguza ile nguvu ya ajira ukiachilia mbali ile ajira ambayo tunaisubiri ya kupata mikopo na kuanza biashara ndogo ndogo. Nimuombe Mhe. Waziri atafute namna ya kuweza kutafuta viwanda vidogo vidogo ambavyo vinaweza kusaidia vijana wetu, tunaweza tukapunguza hilo tatizo la ajira katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa sababu ya uharaka haraka na kwa sababu ya umahiri wa hotuba ya Mhe. Waziri, namna alivyofanya uchambuzi na namna kama nilivyosema mwanzo ya ushirikiano ambao alioutoa kwa

Wawakilishi tunakuwa tunakosa sehemu kubwa sana ya kutoa mijadala yetu katika Wizara hii na nina imani ile michango midogo ambayo tunaitoa basi kwamba nina imani kwa umakini wa Mhe. Waziri, ataichukua na kuifanyia kazi.

Kwa kumalizia Mhe. Spika, Mhe. Waziri ana ahadi ambayo tumezungumza mimi na yeye katika hali ya kawaida, lakini leo ahadi hiyo ninataka nimwambie kwamba naomba anitamkie atakapokuja kufanya majumuisho yake nilimtaka kwa uswahiba wa yeye mwalimu na mimi mwanafunzi wake aliyenisomesha kutoka 1982 mpaka 1985 kwenye Skuli ya Haille Sellassie aje avitembelee vikundi vya Jimbo la Kwahani yeye moja kwa moja ili aweze kunipa matumaini tuweze kutoa michango kwa wananchi, ili kuweza kujenga uimara wa vikundi vyetu katika majimbo yetu. Ni imani kwamba ombi langu siku ya leo atanikubalia baada ya hayo nasema naunga mkono hoja hii kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwahani.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kupata fursa hii ya kuwa leo mfunga dimba kwa majadiliano haya ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa mchana huu kupata fursa hii kuchangia mawazo yangu machache. Pia nikupongeze wewe kwa umahiri wako katika uongozi wako wa Baraza. Aidha nimpongeze Mhe.Waziri kwa kusoma kwake vizuri sana kama alivyosema msemaji mmoja kwamba kitabu hiki ni kikubwa kuliko vitabu vyote, lakini pia kimetumia muda mfupi kuliko vitabu vyote. Kadhalika nawapongeza watendaji wake waliomsaidia kazi hizo za kukifanya kitabu kikubwa lakini pia

Waziri kaja katumia muda mfupi. Ningelimuomba Mhe. Waziri awape darsa Mawaziri wenzake taaluma hii aliyoitumia yeye ili na wao watumie muda mfupi katika kuwasilisha mambo. Lakini watu wa Kusini tuna mambo fulani hapo, kwa hiyo katumia ukusini wake kama nilivyo Mkusini mimi.

Mhe. Spika, hotuba hii kwa ujumla wake ni ajira kwa wananchi wetu, vikundi vya ushirika lengo lake ni ajira, kuna dira ya ajira, idara ya vijana yote haya lengo lake ni kuwatafutia vijana au watu wa nchi hii ajira. Kwa hiyo kimsingi Wizara hii kazi yake ni kuwahudumia wananchi kuwatafutia ajira ili wakwamuke na huu ugumu wa maisha tulionao. Mhe. Waziri, wewe una kazi ngumu kuliko Mawaziri wengine wengi, ingawaje Wizara yako inaonekana kuwa ni ndogo na imekuja kijuujuu, lakini kwa kuwa ndio inahusiana hasa kuwapatia watu wajira na kilio cha vijana wetu ni ajira ajira ajira. Kwa hivyo wewe umepewa jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa unapunguza au kuondoa kabisa hili tatizo la ajira ama kupitia Serikalini, sekta binafsi na njia nyengine zozote halali za vijana wetu kuweza kujiajiri.
Mhe. Spika, Zanzibar ni nchi ndogo kadhalika kwa sababu ni ndogo na watu wake ni kidogo, lakini udogo wao kulingana na matatizo ya nchi wengi wa vijana wana matatizo ya ajira. Sasa ajira ni sehemu ya maisha, Wizara hii katika sehemu zake mbali mbali kila sehemu inapanga ajira hususan kwa vijana. Kwa hiyo vijana ni lazima waandaliwe, waelimishwe na waelekezwe namna ya kujipatia ajira kwa sababu Serikali kwa kweli haina uwezo wa kuwaajiri kila wanayemsomesha, lakini iwe na uwezo wa kumuelekeza kila anayesomeshwa namna ya kujipatia ajira. Moja wapo ya Wizara hii na kukusanya watu katika vikundi vya ushirika, kuwapa taaluma ili wafanye hizo kazi za ushirika na hatimae kuwasadia ili waweze kujiendesha wenyewe. Kama alivyosema Mhe. Mohammed Haji aliyemaliza kile ambacho Serikali inataka kuchangia katika vikundi vya ushirika, kikundi kilichokuwa hakina watu wengi ni watu 20 au 30, kikundi

hicho tunawapa ruzuku ya shs.1,000,000/= au shs.1,500,000/= au hata shs.3,000,000/= wazifanyie nini, na watu wetu kama hawakusimamiwa badala ya kuendesha ile shughuli waliokusudia hatimae hii pesa wananulia change. Kwa hivyo utakutia hivi vikundi viko lakini havijijuu, wanangoja ruzuku watumie wapate ruzuku nyengine watumie ni lazima hivi vikundi tuvipe taaluma ya kutosha

Mhe. Spika, kipindi kilichopita tulivyokuwa kwenye Baraza Mhe. Waziri aliwapa taarifa baadhi ya Wawakilishi kuwa tumpatie angalau kila mtu vikundi viwili vya ushirika katika jimbo lake, ili akenda Pemba na sisi atatwita angalau vile vikundi ambavyo tumempa sisi basi hiyo zakka aliyokwenda kutoa pengine na sisi itufike. Mimi binafsi niliandaa vikundi vyangu viwili, nikampa Mhe. Waziri, kwa bahati taarifa ya kuja kule Pemba nikaipata, nikajikweza na vijana wangu, kufika kule kama si Mhe Mwakilishi hata kwenye ukumbi nisingeliingia, kwa sababu baadhi ya vikundi vyangu nilivyovipeleka havipo. Mhe. Waziri ilikuwa tayari kumbe kaandaa vikundi vyake na wakereketwa wenzake kule sisi ilikuwa anatupiga shere tu. Kwa kweli mimi nilitumia busara ya utu uzima lakini yeye mwenyewe ndiye katuambia na halafu katupiga chenga, ilikuwa Mhe. Waziri hana haja ya kutuambia tuviandae vikundi kwa sababu vikundi tayari tumeshaviandaa. Kwa hivyo hili kwa kweli sikufurahi sana, sikufurahi kukosa, sikufurahi kwamba niende na kumbe hakuna kitu.

Mhe. Spika, niende sasa kwenye ajira za binafsi na kama alivyosema Mhe. Marina kuna vijana wanafanya kazi katika taasisi mbali mbali ambazo si za Serikali na hatimae ama wanaancha kazi au wanafukuzwa kazi kabla ya kutimia ule umri wa miaka 60 na vijana hawa wakawa fedha zao ziko kwenye mfuko wa hifadhi. Sasa kwa kuwa mtu tayari kafukuzwa kazi zile pesa alizoziweka kule ni za kwake kwa nini mfuko

haumlipi, kwa sababu hata akifukuzwa kazi kwa njia yoyote ile, kafukuzwa alichowekeza ni cha kwake. Sasa mtu kafukuzwa kazi ana umri wa miaka 45 angoje miaka 60 wala fedha hizo haziendelei kwa nini asipewe haki yake. Kwa hivyo ningeomba sheria hii ya mfuko wa hifadhi ifanyiwe marekebisho kwa wale watu ambao wameeekeza na kwa bahati mbaya taasisi wanazotumikia zimewafukuza kazi hata kama taasisi ya Serikali iwe kafukuzwa kazi kwa njia yoyote ile, hata ikiwa ni ya utovu wa nidhamu lakini alichoweka wakati huo ilikuwa ana nidhamu. Kwa hivyo kile alichoweka ni haki yake apatiwe mwenyewe, baadhi ya mambo haya huwa yanawadhalilisha kwa kweli wafanyakazi.

Mhe. Spika, Idara ya Ushirika ina jukumu la kuwakusanya vijana katika hivyo vikundi vya ushirika na kuwapatia taaluma. Mhe. Waziri hivi vikundi ni vingi mno sijui ni vikundi vingapi hasa vilivyosajiliwa na vingapi ambavyo vipo tu kijuu juu havijapata usajili ili tuweze kuvishajihisha navyo wapate usajili ili ikitokea hii zakka ya Mhe. Waziri na wao waweze kuipata, kwa sababu bila ya kusajiliwa, zakka hii ya vikundi itakuwa wewe haikufiki wala sadaka itakuwa ni kikundi ambacho kipo tu. Kwa hivyo wale ambao wanaanzisha vikundi na bado havijapata usajili tuwaelimishe ili na wao wapatiwe taaluma ili waweze kupata misaada serikalini.

Mhe. Spika, serikali inatushajihisha watu wajiajiri wenyewe lakini baadhi ya wakati Serikali inachukua fimbo kinyume nyume. Mhe. Spika, nakusudia kwamba inashawajihisha watu wajiajiri lakini baada ya kujiajiri mara nyengine wanawabughudhi, kwa sababu tunasema vyengine na halafu tunafanya jengine. Hotuba zetu zote ni nzuri kama mtu yuko nje ya Zanzibar akasikia maneno ya Serikali waliyosema ataona kwamba Zanzibari wapo pepo ya dunia, lakini ataona loo! wanasema nini hawa na wanafanya nini. Kwa

hivyo ningeiomba Serikali ifanye vile inavyosema, isisema vyengine ikafanya vyengine kutudanganya. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla sijaahirisha kikao hiki nimeombwa niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe wanawake wabakie wana mkutano wao mdogo watapeana taarifa, kwa hiyo Waheshimiwa Wajumbe wanawake mnatakiwa mbakie kuna mambo yanatayarishwa.

(Saa 6.00 mchana Baraza liliahirishwa hadi tarehe 22/07/2013 Saa 3.00 za asubuhi)